ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Kiembesamaki
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake

52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma Jimbo la Bumbwini

53.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake

79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndg. Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tisa – Tarehe 11 Aprili, 2012

(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe, kabla ya kuanza shughuli zetu hapo nje pana ndugu zetu wamekuja na mabango sikuwahi kuyasoma, lakini nafikiri mabango yanayohusiana na masuala ya mambo ya muungano mchakato ambao unategemea kuendelea katika Tanzania ya kutafuta na kuandika katiba mpya si muda mrefu ujao. Ambapo hata tume inayohusika na kukusanya maoni hayo tayari imeshateuliwa.

Tumewapa taarifa ndugu zetu Askari pale nje kwamba basi wabaki kwa usalama pale nje wasikiuke barabara kuingia ndani ili kuhakikisha kwamba ndani katika eneo letu la kazi hamtakuwa na fujo ya aina yoyote, askari tumewaweka *stand by,* lakini tumewaelekeza kwamba wasitumie nguvu ili isije ikatokea fujo na ikatuharibia usalama katika eneo letu lakini pia katika Zanzíbar, niliona nitoe taarifa hiyo ili waheshimiwa wajumbe pamoja na wasikilizaji wetu na wafanyakazi kwa ujumla tubakie tukiwa watulivu na tuendelee na kazi zetu bila ya kuwa na mashaka yoyote.

Naomba kutoa taarifa hiyo.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mwanasheria Mkuu: Taarifa ya Serikali kuhusu Maombi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuongezewa Eneo la Uishio wa Nchi Baharini (*Extensión of Continental Shelf)*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Hoja ya Serikali juu ya Ripoti ya Baraza la Manispaa ya Mji wa Zanzíbar.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 26

Jumuiya ya Afrika ya Mashariki

Mhe. Mbaouk Mussa Wadi (Kny: Mohammed Said Mohammed) - Aliuliza:-

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Zanzibar haishiriki katika Jumuiya hiyo kama nchi inayojitegemea, na katika taratibu za Jumuiya hiyo yapo mambo manne tu ambayo ni ya Muungano. Mengine yote si ya Muungano kwa utaratibu wetu hapa Tanzania.

(a) Je, Zanzibar itawezaje kuyasimamia yenyewe kama nchi, kwenye Jumuiya hiyo mambo yasiyokuwa ya Muungano.

(b) Je, matatizo na kero za muungano haziwezi kuwa ni kikwazo kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 26 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Katiba ya Jamhuri ya Muungano imeainisha kuwa Mambo ya Nje ni moja kati ya Mambo ya Muungano . Kwa msingi huo, ushirikiano wa Kikanda unahesabiwa kama moja ya Mambo yanayoshughulikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nakubaliana na Mheshimiwa Mwakilishi kuwa katika shughuli za Ushirikiano wa Kikanda kuna mambo Ambayo si ya Muungano kama vile Elimu ya msingi na kati, kilimo n.k. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikishirikishwa kikamilifu katika mambo yote ya ushirikiano wa

Kikanda. Wataalam wetu wanashiriki katika kamati za kitaalam pia Makatibu Wakuu wanashirikishwa katika vikao vya Makatibu Wakuu na hata Mawaziri wanahudhuria katika mikutano ya Baraza la Mawaziri, lakini si hapo tu hata Rais wa Zanzíbar anaalikwa katika viokao vya viongozi wa kuu wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Napenda kumuhakikishia Mheshimiwa mwakilishi kuwa maslahi ya Zanzibar yanalindwa ipasavyo katika ushirikiano wa Kikanda Ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama.
Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba baadhi ya kero za Muungano ni kikwazo katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki hasa ule mchakato wa *first tacking* na hili limeelezwa na Tanzania kwamba lisiharakishwe suala hilo, watupe fursa sisi Tanzania tuweke sawa baadhi ya mambo yetu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu suala lake amekiri kwamba baadhi ya kero za muungano zinaweza kuwa kikwazo kwa Jumiya ya Afrika ya Mashariki, kwa kuwa tumekuwa na mlolongo wa muda mrefu wa kero za muungano na kwa kuwa sasa tunaingia kwenye Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, Hanoi kwamba Wazanzibari wataendelea kutoongea.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Kezo za Muungano tunajitahidi kuzishughulikia kupitia kamati zetu za mawaziri wa pande zote mbili, Mawaziri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar na Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, vikao hivi kwa upande wetu vinaongozwa na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais na upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano unaongozwa na Waziri Mkuu chini ya uenyekiti wa Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais, kuna mambo mengi tumeshapiga hatua na mengine bado yanatukwaza lakini bado mazungumzo tunaendelea nayo kuna mafanikio mengi tumeshayapata moja ni lile la deni la umeme, lakini pia hata baadhi ya kodi makubalino tunakuwa tunajua tu kwamba yapo matatizo ya utendaji, lakini kimsingi mambo kadhaa tumeshakubaliana.

Sasa ni kweli kama nilivyosema na nilivyokiri kwamba sisi wenyewe kama Tanzania tumeiambia Jumuiya ya Afrika ya Mashariki wasiharakishe lile shirikisho, kwamba bado sisi kama Tanzania tuna matatizo kwa hivyo twendeni taratibu tuweke sawa mambo yetu halafu tena tuje tuungane.

Mhe. Spika: Kidogo marekebisho chini ya uenyekiti wa Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, wewe ulisema Makamo wa Kwanza.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize suala moja Mhe. Waziri kama ifuatavyo.

Kwa kuwa suala hili la kero za muungano ni suala ambalo linazungumzwa kwa muda mrefu tokea awamu zilizopita hasa ya Rais William Benjamín Mkapa na kwa kuwa awamu hii ya Rais Jakaya Mrisho Kikwete ambayo takriban imeshachukua miaka karibu saba, ambapo Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete aliunda utaratibu huu wa kukutana na kutatua hizo kero za Muungano. Kwa kuwa kro hizo bado zinaonekana hazijaweza kutatuliwa katika muda huu wote. Je, Mhe. Waziri unahisi ni tatizo gani hasa linalosababisha kero hizo zisiweze kutatuliwa haraka ili tukaanza kuendelea mbele na kushughulikia masuala mengine.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe, Salmin Awadha Salmin ametaka maoni yangu sasa kwa maoni yangu Mhe. Spika, mazungumzo yanaendelea na kama nilivyosema tumekuwa tukipiga hatua kwa hatua lakini kuna matatizo mengine ni magumu yanahitaji viongozi wa nchi waingilie kati. Kwa mfano suala la mafuta sisi hapa tumetoa barua yetu mpaka kwa waziri Mkuu lakini jawabu mpaka leo hatujalipata, sasa haya naamini kwa mtizamo wangu mimi lazima viongozi wakuu washiriki kutukwamua tulipo, hili waziri Mkuu aliahidi kwamba yeye ataipeleka mbele suala hili.

Kwa hivyo mimi namuomba Mhe. Salmin yeye akiwa ni mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Tawala Chama cha Mapinduzi basi atusaidie na yeye kama ni kiongozi wetu upande wa Chama cha Mapinduzi Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo tunamuomba atusaidie kulisukuma mbele au kuyasukuma mbele matatizo haya.

Nam. 102

Eneo la Biashara Ndogo Ndogo Saateni

Mhe. Hija Hassan Hija - Aliuliza:-

Eneo la Saateni lilitengwa makusudi na Baraza la Manispaa kwa ajili ya wafanyabiashara wadogo wadogo ili kuepusha msongamano eneo la Darajani.

(a) Je, ni kweli kuwa eneo hili limebeba zaidi ya wafanyabiashara 6,000 ambao wamesajiliwa na kila mmoja amekata leseni ya kuanzia Shs. 80,000/=.

(b) Je, eneo hilo linaingiza kiasi gani kwa mwaka, kama kodi.
(c) Ni changamoto zipi zinazolikabili Baraza la Manispaa katika eneo hilo.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe, Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 102(a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Eneo la Saateni kwa sasa lina jumla ya wafanyabiashara 182. kati ya hao wenye maduka ni 31 na wafanya biashara wadogo wadogo ni 151. Kwa mujibu wa taratibu za biashara katika eneo hilio, wafanyabiashara wadogo wadogo hawakati leseni ila wanalipa ada ya TZShs. 500 kwa kila siku moja na kwa kila mfanyabiashara mmoja. Viwango vya leseni ya mwaka kwa wafanyabiashara wa maduka katika eneo la Saateni ni kuanzia TZSh. 50,000/= hadi TZS 100,000 kwa kutegemea na ukubwa wa duka.

b) Kwa mwaka wa fedha wa 2010/201, eneo la Saateni limeingiza jumla ya TZSh. 15,210,300. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, hadi kufikia Februari 2012, eneo hilo limeingiza jumla ya TZSh. 8,726,200.

c) Changamoto zinazolikabili Baraza la Manispaa katika eneo hilo ni kama zifuatazo:-

   i) Wafanya biashara wadogo wadogo kutokana na biashara zao ni za kuhamahama hivyo wanatumia mwanya huo kukwepa ada wanazotozwa.

   ii) Uvamizi wa wafanya biashara holela katika eneo la mbele ya Saateni ambapo pametengwa kwa kuegesha magari.

   iii) Kukosekana kwa uzio wa matofali katika eneo hilo utakaoweza kuimarisha usalama na mali za wafanyabiashara kutokana na uvamizi unaofanywa na wanaotumia madawa ya kulevya.

   iv) Mahitaji ya kujenga kituo cha Polisi kukabiliana na wahalifu wanaofika katika eneo hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

Mhe. Waziri anasema kwamba mapato yanayopatikana pale mwaka jana yalikuwa Shs. 15 milioni na 2011/12 hadi sasa ni Shs. 8 milioni, hivi Mhe. Waziri haoni kwamba mapato hayo ni mzaha na hayaelekei kabisa kwa jinsi ya malengo ya serikali yalivyokusudiwa mapato haya ni madogo. Kwa sababu milioni 8 kwa kipindi hicho ni mapato ambayo kwa kweli si mapto ya hadhi ya eneo lile.

Lakini pili zipo taarifa kwamba kuna wafanya biashara pale wamemiliki milango mingi na wakiwa na leseni moja, hili Mhe. Waziri unalijua na kama unalijia unasemaje.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Hija Hassan Hija kama sikosei ni Mjumbe wa kamati ya PAC sasa katika kutembea tembea na haya mahisabu amegundua hayo mimi sipingi, lakini ninchotaka kusema basi na mimi umenipa changamoto nikafuatilie nione tatizo ni nini kwa nini yakawa madogo. Kwa hivyo nachukua changamoto uliyonipa Mhe. Hija nitaifanyia kazi.

Kwa kweli kwa hilo suala la Pili silijui na namshukuru kwa kunipa taarifa hiyo sasa hili nitafuatilia kwa undani na kuona kama wapo wanaomiliki hao wanaitumia vipi na wanatulipa kodi, kumiliki mlango mmoja au miwili si neno lakini wanaitumia na wanalipa kodi, unajua wafanyabiashara walivyo sasa na hili naahidi Mhe. Spika, nalo nitafutilia kwa makini sana nione kama wapo hao na utaratibu gani uliopo halafu nitaleta majibu rasmi.

Mhe. Salmin Awadha Salmin: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza Suala moja la nyongeza.

Mhe.Spika, kwa kuwa Mhe. Waziri amekiri kwamba eneo la Saateni limetengwa makusudi na Baraza la Manispaa kwa ajili ya wafanya biashara ndogo ndogo ili kuepusha msongamano wa eneo la Darajani, na kwa kuwa baadhi ya wafanya biashara wamekaidi agizo la Manispaa la kuondoka katika eneo hilo la Darajani na kusababisha bado msongamano kuendelea kuwepo.

Je, Baraza la Manispaa litachukua hatua gani ili kuhakikisha ile dhamira ambayo imeikusudia ya kuwaondosha wafanyabiashara pale kwa ajili ya kuondosha msongamano hasa katika Skuli ya Darajani ambapo wanafunzi wengi hupata matatizo na hupata shida wakati wa masomo,

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ni kweli kwamba kuna wafanya biashara wadogo wadogo ambao wale niliosema leo wanakaa hapa kesho wanakaa pale na wapo Darajani pale, tumejitahidi kutumia siasa na tutaendelea kutumia siasa sio nia ya serikali yetu kutumia nguvu kwa watu wetu, lakini ikibidi watu wasiofuata taratibu na sheria basi hiyo itakuwa ni hatua ya mwisho. Lakini tumeshazungumza na Mhe. Waziri wa Biashara Viwanda na Masoko kwa sababu wale ni wafanya biashara na wao ndio sekta yake Mhe. Waziri, na sisi kama Tawala za Mikoa lile ni eneo letu tu.

Kwa hivyo tutakaa pamoja na wao jambo la kufurahisha hata wale walioko Saateni waliokwisha kwenda wametuandikia barua Wizara kutuomba kwamba na wale wenzao basi waende kule nafasi ipo, kama si hivyo hata wao wamesema kwamba kama wale hawaji basi na wao watarudi. Hiyo naamini wamzungumza kwa nia safi kwamba na hawa walioko huku waende.

Sasa Mhe. Spika, nasema kwamba nimeshazungumza mara nyingi hapa kwamba tunawaomba sana kwa busara wenyewe wale ambao wako katika maeneo yasiyokubalika basi waondoke na waende kwenye sehemu ambazo zimekubalika, si jambo zuri mbele ya skuli watoto wa shule pale wanapata shida ya lupita na mambo mengine, juzi mmoja alisema wengine wanajisaidia pale si jambo la kufurahisha. Kwa hivyo tutajitahidi kutumia busara na hekima pamoja na viongozi wetu tuone kwamba wale watu wanaondoka na wanakwenda mahala kunakohusika.

Nam. 15

Hospital ya Chake-Chake

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Hospitali ya Chake-Chake inategemewa sana na wananchi wa Pemba kutokana na pahala ilipo kijiografia.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuifanyia ukarabati mkubwa Hospitali ya Chake-Chake kutokana na dari za baadhi ya wodi kuoza.

(b) Serikali ina utaratibu wa kuzifanyia matengenezo hospitali zake kila baada ya muda gani.

(c) Kwa kuwa Serikali iliamua kupeleka wauguzi Kisiwani Pemba ili kuondoa uhaba wa wataalamu hao, imekuwaje tatizo la uhaba wa wauguzi liendelee na kusababisha wagonjwa wanaolazwa katika hospitali hiyo kutumia dawa bila ya kuzingatia ratiba, kama wanavyopangiwa na madaktari kutokana na uhaba wa wauguzi.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako swali lake nambari 15 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Ni kweli tunafahamu hali ya hospitali ya Chake Chake inahitaji kufanyiwa ukarabati kila baada ya muda au yanapotokea mahitaji ya kufanya hivyo. Katika mradi wa ADB katika awamu ya Pili ya kuboresha huduma za afya Zanzibar hospitali ya Chake Chake inategemewa kufanyiwa marekebisho makubwa. Kwa batí mbaya ADB mara hii imeelekeza fedha zake kwa kuimarisha Wizara ya Miundo Mbinu Utawala Bora na Wizara ya Elimu.

Wizara imelazimika kutafuta wafadhili wengine kwa ajili ya matengenezo makubwa ya hospitali hiyo.

(b) Serikali ina utaratibu wa kuzifanyia matengenezo hospitali zake kila pale inapobidi. Kuna kifungu cha fedha katika kila kamati ya uongozi wa afya Wilaya ili kukidhi haya hiyo. Kamati hiyo huangalia majengo wanapofanya shughuli za ufuatiliaji na kuandika mahitaji yake na kutengeneza kwa mujibu wa mfuko wao na idadi ya vituo vyenye matatizo au hospitali zaenye matatizo ya aina hiyo

(c) Mhe. Spika, tunasikitika kidogo kumueleza mjumbe kwamba kifungu cha © cha suala lake hakina uhusiano na Vifungu vya (a) na (b). Hata hivyo naomba kueleza kwamba serikali kuamua kupeleka kwa wafanyakazi Bemba haimaanishi kwamba tatizo limekwisha, uhaba wa wafanyakazi wenye uwezo na wenye taaluma inayotakia ungalipo kwa sababu waliopelekwa ni kidogo kuliko mahitaji yanayohitajika kwa Bemba na Unguja.

.Nasikirika tena Mhe. Spika, kwamba hatuoni uhusiano wa kifungu cha (d) kwa kupelekwa wafanyakazi Bemba na upewaji wa dawa kwa wagonjwa, hata hivyo naomba kumjibu kwamba ni utaratibu wa kawaida kwa wagonjwa kuchukua dawa zao kutoka *Phamacy* yaani kitengo cha dawa au kama hazipo hununuliwa nje ya hospitali na kukabidhiwa mgonjwa ikisha kufahamishwa yeye mwenyewe au jamaa yake jinsi ya kutumia dawa hizo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mzuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

a) Mhe. Waziri mwaka Jana ulifanya juhudi kubwa kupeleka wauguzi Bemba kwa wingi ni sababu gani zilizosababisha kwa kasi wauguzi hao kurudi kwa hivi sasa.
b) Kwa kuwa madaktari bingwa wanalalamika juu ya tatizo la wagonjwa kutumia dawa bila ya kuzingatia ratiba kutokana na tatizo hilo la upungufu wa wauguzi, vigezo gani unavyotumia kuona walioathirika mpaka muda huu.

Mhe. Waziri wa Afya: Mimi sikubaliani nae kwamba wamerudi kwa kasi Unguja, taarifa tulizokuwa nazo kutoka kwa wafanyakazi wetu na wakubwa wetu Pemba ni kwamba waliorudi ambao wengine hawakurudi Unguja wamekimbia kwa kutafuta maslahi kwengine, suala ambalo ni tatizo la kitaifa hawazidi ishirini. Kwa hivyo kwa jumla kazi ile imefanikiwa kwa kiasi cha asilimi tisini, lakini moja katika sababu iliyowafanya warudi ni kwamba iliahidiwa na Wawakilishi hapa kwamba nitakapowapeleka watawasaidia nyumba.

Nasikitika kusema kwamba sio wawakilishi wengi walioweza kutusaidia kwa hilo, kwa hivyo matokeo yake ikawa ni Wizara kukodi nyumba binafsi na kuwalipia watu wale nje ya katiba yetu.

Lakini bado tumelisimamia hilo na tumefanikiwa kwa kiasi hicho kwa hivyo si kweli kama wamerudi wengi kwa kasi, wale waliotoweka wametoweka kwa njia zao na hilo ni suala la kitaifa. La Pili kuhusu madaktari na kutolewa dawa hili naona sio suala la kawaida, mgonjwa yoyote anapotibiwa na daktari hupewa utaratibu wa kutumia dawa sasa sioni uhusiano kwa sababu nasi hayupo mgonjwa ale dawa ovyo, labda iwe ni matatizo maalum na Maradi maalum.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, hospital iza Pemba zimegawika katika madaraja hospitali ya Mkoani na Wete inaelezwa na serikali ni kwamba ni hospitali za Mikoa, hospitali ya Vitongoji Cottage pamoja na Micheweni ni hospitali katika ngazi ya Wilaya. Swali langu je, hospitali ya Chakechake ipo katika daraja gani.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa mujibu wa daraja zetu hospitali ya Wete, Chake na Mkoani ni hospitali za Wilaya zinazostahiki kupandishwa daraja ziwe za Mkoa. Hospitali za *Cottage* ya Micheweni, Kivunge, Makunduchi na Kitongoji zinaitwa *cottage* hospital tunatakiwa tuzipandishe daraja ziwe za wilaya.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, baada ya majibu mazuri ya ufafanuzi ya Mhe. Waziri naomba nimuulize kama ifuatavyo:

Amekiri kwamba hospitali ya Wete, Chake na Mkoani ni za Wilaya na zinakusudiwa kupandishwa daraja na vile vile *cottage* zitapandishwa daraja ili ziwe za Wilaya, lakini ahadi hiyo aliitoa kwenye bajeti iliyopita, sasa hivi imebakia miezi miwili kumaliza bajeti iliyopita. Je, upandishaji huo unakusudiwa mwaka gani.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, ni kweli kwamba kulikua na ahadi hiyo lakini sikusema kwamba hospitali zote zitakua za Mkoa baada ya miezi 12 ni katika mfumo wa utaratibu wa kuzibadilisha ili kuongeza huduma ziwe karibu na wananchi. Katika utaratibu huo tumepiga hatua sana kwa hospitali ya Makunduchi ambayo kila mara hua naitolea mfano hapa kwamba kwa sasa huduma zote zinazohusu matibabu ya kina mama haziji mjini, upasuaji unafanywa pale, kutiwa damu kunafaywa pale na kumekua na utaratibu pale Makunduchi kuna simu ipo pale hospitali na wamepewa wananchi takriban wa Wilaya nzima kwamba wanapokua wana matatizo wa-*beep* tu na *ambulance* inawafuata.

Kwa sababu hiyo tumefanikiwa vizuri kwa muda wa miaka miwili sasa hivi hajafariki mgonjwa kutoka Wilaya ya Kusini kwa sababu ya uzazi. Aliyefariki ni mgonjwa mmoja na kwa sababu alicheleweshwa kufikishwa hospitali.

Katika utaratibu huo huo juzi tumetia saini mkataba na wale waliotufanikisha suala hilo kwa Makunduchi na sasa tupo Hospitali ya Mkwajuni. Ikitoka Mkwajuni tunaelekea Pemba kwenye Hospitali za Vitongoji. Pale Mkwajuni nimeshamfikisha mwenyewe mkubwa ambaye ni meneja mpya kwa hospitali ya Kivunge ambaye atasimamia uongozi na kuimarisha hospitali ile. Kwa hiyo hatua ya kuzitoa kutoka *Cottage* kwenda Wilaya inaendelea vizuri na zile za Wilaya kwenda mkoa zipo katika utaratibu wa mipango yetu.

Nam. 16

Utafiti wa Maabara ya Sayansi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inachangia kiasi gani kwa mwaka katika maabara ya utafiti iliyopo Wawi Pemba.

(b) Tangu kuanzishwa kwa maabara hiyo Serikali inanufaika vipi na utafiti unaofanywa kwenye kituo hicho.

(c) Kuna malalamiko kwamba Serikali imekua haitoi mchango wake kwa kuzingatia muda muafaka wakati Wizara ya Afya inaidhinishiwa fedha na Baraza kila mwaka kwa ajili ya taasisi ya utafiti ikiwemo maabara hiyo.

Mhe. Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 16 lenye vifungu (a) (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

(a) Wakati ilipoanzishwa maabara hii miaka 11 iliopo serikali ilitakiwa kuchangia milioni 30 kwa mwaka ili kuendesha taasisi hii. Kwa vile ni mradi wa Wizara umewekwa kwenye *programme* maalum ya miradi wizara na serikali hua inatoa kiasi maalum cha fedha kadiri bajeti inavyoruhusu. Hata hivyo SMZ inalipa mishahara ya wafanyakazi katika taasisi hii kwani ni waajiriwa wa serikali.

(b) Manufaa makubwa yamepatikana tangu kuanzishwa kwa taasisi hii.

(i) *PHL- IDC* ni maabara ya rufaa kitaifa kwa utambuzi wa ugonjwa wa kifua kikuu na kuhakiki ubora (*quality Control)* kwa wagonjwa wa kifua kikuu wenye kutiliwa mashaka na vipimo vya kawaida havikuonesha vizuri.

(ii) Kwa kushirikiana na mradi wa malaria (ZMCP) maabara inahakiki vipimo vyote vilivyoonekana na vimelea vya malaria *(malaria positive)* na asilimia kumi ya vipimo vilivyoonekana havina vimelea *(malaria negative*).

(iii) *PHL – IDC* ni maabara tegemezi kwa kuangalia maradhi ya kuambukiza hasa kipindupindu kisiwani Pemba.

(iv) Kupitia mradi wa maji salama *(Safe Water Project)* ambao taasisi inashirikiana na ZAWA kuna visima vilivyo hakikiwa ubora wake na vilivyojengwa upya kwa manufaa ya jamii husika.

(v) Maabara inayafanyia uchunguzi maji *(Biological Analysis)* kutoka vyanzo mbali mbali na kuishauri ZAWA juu ya kuyasafisha ili yawe safi na salama.

(vi) Tafiti za maskulini ziliweza kuibua miradi juu ya minyoo na kichocho na ilisaidia wananchi ikiwemo Kutoa dawa za minyoo na kichocho kwa wanafunzi mashuleni na wananchi katika sehemu husika.

(vii) Mwaka huu taasisi imepata mradi wa kuisaidia hospitali ya Chake Chake kwa vitendea kazi na mafunzo kazini kwa wafanyakazi wake.

(viii) Taasisi kupitia mradi wa IDCF wanasaidia mradi wa mama na mtoto katika kituo cha Gombani kwa majengo. Dawa na huduma za ufuatiliaji kinamama na watoto vijijini.

(ix) Kitengo cha upasuaji wamepata vifaa, vitendea kazi na mafunzo kupitia IDCF.

(x) PHL – IDC kupitia miradi yake mbali mbali kunatoa ajira mbali mbali za muda mfupi na mrefu kwa wananchi visiwani na Tanzania kwa jumla wanaosaidia kufanya utafiti.

(c) Tangu kuanzishwa kwa maabara hiyo serikali inanufaika kwa sababu maabara hii sasa inajulikana. na *World health organization* kama ndio *the best research institute* kwa mara ya kwanza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu marefu sana ya Mhe. Waziri nataka kujua kile kitengo ni muhimu sana. Je, wizara yake inasaidia kiasi gani kwa mwaka.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwenye swali mama nimeeleza hivyo. Lakini naomba niwaeleze waheshimiwa wajumbe wa Baraza hili kwamba taasisi ile takriban sasa inajiendesha wenyewe bila hata kuhitaji pesa za serikali. Nilitegemea Mhe. Jaku kama kawaida yake atakuja na suala hilo. Hizi hapa nina taarifa za hesabu za miaka mitano iliyopita.

Mwaka wa 2007 shirika lile au lebo ilikua na nakisi ya milioni 34 wakati huo serikali ilikua kila mwaka inalipa fedha kidogo kidogo.

Mwaka huu wa 2012 ina *surplus* ya milioni 89, kwa hivyo taasisi inayojitegemea, kila miaka ilivyopita ilikua serikali inatoa fedha kidogo kidogo mpaka ilipofika hadi ikaona kwamba sasa inajitegemea kwa hivyo serikali sasa hivi haitoi fedha zaidi, isipokua wafanyakazi wote wa serikali pale wanalipwa na mishahara kutoka serikalini.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza namshukuru Allah kwa kutupa uhai na uzima, naomba nimuulize Mhe. Waziri pamoja ya kua na majibu yake marefu na mazuri swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b).

(a) Kwa kua taasisi ile amethibitisha katika jibu lake mama kwamba ni kitengo kilishokwisha thibitishwa na WHO kwamba in *the best research institute* kwa maradhi hayo. Kuna taarifa kwamba tafiti ambazo zinatolewa na Wizara ya Afya hapa Zanzibar, hazielekezwi zaidi kule lakini zinaelekeza vituo vyegine nje ya Zanzibar. Je, habari hiyo ni ya ukweli, kama ni ya ukweli kwa nini tafiti hizo zisielekezwe kule Pemba katika kituo hichi ambacho kimekua *valid best* na zikaekelekezwa nje ya Zanzibar.

(b) Taasisi hii amesema katika jibu lake kwamba tayari inajitegemea kiuendeshaji kifedha. Je, kiuwezo wa maamuzi wizara inaiweka pahali gani taasisi hii, iko *independent* au inategemea maamuzi kutoka Wizarani zaidi.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwanza naomba nishukuru kwamba Mhe. Rashid Seif amepata nafuu na leo tunae Barazani.

Mhe. Spika, swali hili la tafiti nimeeleza kwamba tafiti nyingi hasa za Idara ya Maji, Maradhi ya kichocho na maradhi mengine yanayohusiana na Wizara yanapelekwa pale. Mimi sina hakika kama kuna *research* nyengine zinapelekwa kwengine, pengine labda angetoa mfano lakini ninavyojua kwamba sisi tunaitumia sana kwa shughuli hizo za tafiti.

Kwa taarifa ya Baraza hili mashirikiano ya taasisi ile na Jumuia ya Kimataifa ni kubwa sana. Hivi sasa walikua wanakamilisha mradi mmoja kwa kuhakikisha jinsi ya matumizi ya kuzuia kichocho hasa kwa watoto wadogo katika maeneo ya Pemba kwa sababu ndio kwenye maji yanayotuwama na maeneo ya kwetu Kaskazini Kinyasini na Kitope suala hilo linaendelea hivi sasa na Chuo Kikuu cha Marekani (Georgia) inafanywa pale.

Miradi ya malaria wakikwama watu wa Idara yetu ya Malaria wanakwenda pale. Idara ya Maji wanapotaka kuhakikisha matatizo ya maji ya usafi wanakwenda pale. Kwa hivyo kwa kiasi fulani tunaitumia sana nje na ndani ya nchi yetu.

Suala la pili ni kwamba mimi ninavyoamini kwamba lebo ile haiingiliwi na Waziri wala Wizara, takriban inajitegemea wenyewe. Hesabu hizi nilizoletewa ni hesabu zilizoletwa na wenyewe bila ya kuingiliwa na Wizara. Suala kubwa sana tunapoweza kuingilia ni pale kunapohitajika kwa waajiri wa serikali kwa sababu bado inabaki ni taasisi ya serikali. Kila mradi unakwenda pale kutoka nje unalazimika kutoa si chini ya asilimia 10 ya gharama ya mradi huo. Na sisi Wizara hatutii mkono wetu, masuala yao na *account* zao na hizi zote wanafunga wenyewe. Sisi kama wizara tunasimamia kwa sababu ndio wizara mama.

Nam. 74

Ujenzi wa Chuo cha Amali – Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Mhe. Salim Abdulla Hamad – Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliahidi katika kampeni ya Urais kwamba kwa kipindi cha 2010 – 2015 kitajengwa Chuo cha Mafunzo ya Amali cha Mkoa wa Kaskazini Pemba katika Jimbo la Mtambwe.
Je, ujenzi huo umefikia hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 74 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kua Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliahidi katika kampeni za kugombea Urais kwamba kituo cha Mafunzo ya Amali cha Mkoa wa Kaskazini Pemba kitajengwa katika jimbo la Mtambwe. Kituo hicho kitajengwa kupitia awamu ya pili ya mradi wa elimu mbadala utekelezaji wake kwa pamoja kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Mkataba wa makubaliano wa utekelezaji wa mradi huu umeshatiwa saini na utatekelezwa kwa muda wa miaka mitano. Baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:

Ujenzi wa kituo hicho haujaanza kwa vile mradi haujakamilika rasmi kutokana na kutokamilika baadhi ya taratibu za kibenki. Ujenzi huo tunatarajia kufanyika baada ya miezi 15 kabla ya kazi ya ujenzi kuanza. Wizara itatangaza zabuni ya kupata mshauri mjenzi ambaye atafanya kazi ya utayarishaji wa michoro na mara michoro itakapokamilika wizara itatangaza zabuni ya kumpata mkandarasi atakayejenga kituo hicho na vituo vyengine.

Taratibu za kisheria za manunuzi ambazo zitatumika zitachukua muda wa mwaka mmoja na miezi mitatu hadi kukamilika na mkandarasi wa ujenzi. Nakushukuru sana Mheshimiwa.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa majibu niliyoyapata kuhusu suala hili. Kwanza nitoe pongezi kwa Mhe. Asha Bakari Makame kwa kua alikua ni mfuatiliaji mkuu wa ujenzi wa shule hii. Lakini kwa bahati mbaya lile aneo alilopendekeza halikufaa na tukatakiwa tutafute eneo jengine na tukapata eneo pale Bwagamoyo. Kuna taarifa za baadaye zilijitokeza kua Chuo hichi huenda kikajengwa katika eneo la Mzambarauni kiasi ambacho mpaka Mhe. Mwakilishi kaingizwa kua kahusika katika kuwaondoa Mzambarauni kupelekwa Bwagamoyo. Ningelimuomba Mhe. Waziri anipe ufafauzi hasa kama ikiwezekana kujengwa hichi kituo kitajengwa wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, mimi na Mheshimiwa wa jimbo la Mtambwe, tulikaa tukapanga twende tukatizame ni eneo gani katika jimbo la Mtambwe litakua muwafaka. Kwa sababu Mhe. Rais aliahidi licha ya kua kituo kile ni cha Mkoa, lakini aliahidi kukijenga ndani ya jimbo la Mtambwe. Mimi sikuwahi kwenda katika ziara ile lakini Naibu Katibu wangu alikwenda ziara ile na wakenda wakaona sehemu ambayo kasema Mhe. Mwakilishi na sehemu nyengine.

Sehemu ambazo tumezitembelea kwa sasa ni sehemu hii ya Daya, sehemu ya Bwagamoyo na Mzambarauni. Mpaka hivi sasa Mheshimiwa Wizara haijaamua hasa kituo hichi kitajengwa wapi. Daya tumekuona, Bwagamoyo tumekuona na Mzambarauni tumekuona. Tunakaa pamoja na Afisi ya Mkuu wa Mkoa, kwa sababu kituo hichi kimekusudiwa ni cha Mkoa na tutatarajia kujenga kituo cha Elimu Mbadala Ungi, wanafunzi ambao watatoka Ungi ndio wanafunzi wale wanaojiunga na kituo hichi kwa Mkoa mzima. Ni lazima tutizame sehemu mwafaka ambayo itakua ni katikati ya jimbo hili la Mtambwe kwa wanafunzi wetu ambao watatoka kwenye kile chuo ambacho tutajenga Ungi au katika sehemu nyengine za Mkoa wa Wete wa Kaskazini Pemba basi isiwe ni vigumu kwao kukifikia.

Namuomba Mhe. Salim Abdalla Hamad astahamili kidogo baada ya muda si mrefu, atajua tutampelekea ripoti kituo hichi tutajenga katika eneo gani kati ya haya maeneo matatu ambayo tumekwenda tukayakagua.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza napenda nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake. Naipongeza serikali kwa nia thabiti ya kuanzisha elimu ya ufundi na kuthibitisha kwamba kuna utanuzi wa hivyo vyuo ambavyo vitaendelea kukidhi mahitaji ya wananchi wetu.

Mhe. Spika, tokea kuanzishwa vyuo hivi vya mafunzo ya amali ni kipindi sasa hivi. Na kwa kua hata jiko Mhe. Spika, likijengwa vikombe vyengine huvunjika na sahani nyengine zikavunjika. Je, vyuo hivi ambavyo vipo sasa hivi wizara ina mkakati gani na muda gani wa kuongeza zana katika vyuo hivi ili isijeikawa ni nyimbo ya Skuli ya Kengeja, skuli ya ufundi lakini inasomesha maneno.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni bahati mbaya sana Mhe. Spika, Mhe. Rashid juzi hakuwepo wakati nilipokua nikijibu swali la vyuo vya Amali na namna gani ambavyo tunafikiria kuviendeleza. Kwa faida yake Mheshimiwa hiki hakitokua chuo cha nadharia, tumejipanga uzuri hata mfano wa hicho chuo ambacho kakitolea mfano Chuo cha Kengeja nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba tayari tumepeleka fedha pale kwa ajili ya kununua vifaa. Hivi vyuo vyetu vya amali basi kama ambavyo nilitoa majibu juzi tutahakikisha kwamba vinapatikana vifaa vyote ili ile dhana nzima ya Wizara ya Elimu ya kutaka vijana wetu wakitoka kwenye vyuo vile waweze kujitegemea wenyewe kwa kazi zao ndogo ndogo iweze kufikiwa.

Nam. 57

Mitihani ya Form II na STD. VII

Mhe. Hija Hassan Hija – Aliuliza:-

Mnamo mwezi wa Novemba 2011 wanafunzi wa Zanzibar wa F.II na Std VII wamefanya mitihani yao na kutarajia matunda yao hivi karibuni.

(a) Je, wanafunzi waliofanya mitihani ni wangapi.

(b) Ni walimu wangapi wameteuliwa kufanya kazi ya usainishaji wa mitihani hiyo, Unguja ni wangapi na Pemba ni wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-
Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake Nam. 57 lenye vifungu (a) na (b) kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wanafunzi wa skuli za Zanzibar waliofanya mtihani katika mwezi wa Novemba 2011 wa darasa la saba walikua ni wanafunzi 23,798 kati ya wanafunzi 15,556 walikua wa skuli za Unguja na wanafunzi 8,242 walikua ni skuli za Pemba. Pia wanafunzi waliokua wanafanya mtihani kidatu cha pili walikua ni wanafunzi 19,666 kati yao wanafunzi 13,266 walikua ni wanafunzi wa skuli za Unguja na wanafunzi 6,400 walikua ni wa skuli za Pemba. Kwa jumla wanafunzi 43,464 kati yao wanafunzi 28,822 walikua wa skuli za Unguja na wanafunzi 14,642 walikua ni wa skuli za Pemba waliofanya mtihani wa darasa la saba na kidatu cha pili.

Mhe. Spika, walimu walioshiriki katika usahihishaji wa mitihani walikua ni walimu 333 kwa mitihani ya darasa la saba walikua kati yao walimu 325 walikua ni kwa skuli za Unguja na walimu wanane (8) wa skuli za Pemba. Kwa upande wa mitihani ya kidatu cha pili walimu 417 walishiriki katika usahihishaji wa mitihani, kati yao walimu 401 alitoka skuli za Unguja na walimu 16 walitoka skuli za Pemba. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Namshukuru sana Mhe. Waziri kwa kunipa ufafanuzi wa takwimu za walimu walioshiriki kwenye mitihani hii.

Mhe. Spika, karibu walimu 800 walishiriki kusainisha mitihani hii darasa la saba na form II kwa Unguja na Pemba. Kati ya hao ni walimu 24 tu ndio waliotoka Pemba. Nina hakika wingi wa walimu hao 800 walikua ni Mkoa wa Mjini Magharibi.

(a) Kwa nini Wizara yako Mhe. Naibu Waziri, inawatenga walimu wa Pemba na walimu wa Mikoa ya Unguja Kaskazini na Unguja Kusini na ikaona umuhimu wa kuchukua walimu wa mjini tu.

(b) Ikiwa Wizara inafanya hivi ile dhana ya walimu wa Pemba na walimu wa Mkoa Kusini Unguja na Kaskazini kwamba hawana imani na matokeo ya wanafunzi wao si sahihi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo na Amali: Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija kasema kutokana na takwimu hii ambayo nimeitoa inaonesha kua walimu wa Pemba tunawatenga. Ninalotaka Mhe. Spika, kumuhakikishia Mheshimiwa mwakilishi na Baraza lako tukufu kua walimu wa Pemba hatuwatengi. Kinachotukwaza Mhe. Spika, ni bajeti yetu ya wizara kuwatoa walimu Pemba kuja Unguja ni gharama mara mbili au tatu ya walimu ambao tunachukua kusainisha. Mwalimu akitoka Pemba anahitaji nauli yake ya kwenda na kurudi, anahitaji posho yake ya safari kwa siku ambazo atakaa asainishe. Vile vile anahitaji ile posho ya usainishaji ambayo inatolewa kwa walimu wote.

Kwa hivyo, hilo Mhe. Mwakilishi alione kwamba ni tatizo ambalo tunalo hapa ni bajeti, lakini nimuahidi Mhe. Mwakilishi kila hali ya bajeti itakavyokuwa nzuri basi tutaweza kuwachukua walimu kutoka Pemba. Mhe. Spika, na kwa sababu yeye mwenyewe ni Mjumbe katika Kamati ya Wanawake na Ustawi wa Jamii moja ya taasisi zake ambazo anazifuatilia ni Wizara ya Elimu.

Mhe. Spika, jambo moja ambalo amelibaini kwamba sio walimu wa Pemba ambao hatuwachukui sana, lakini hata kutoka katika Mikoa mengine ni kuwa walimu ambao tunawachukua ni walimu wa Mkoa wa Mjini Magharib kutokana na kuwa walimu hawa ukiwachukua watakachokihitaji ni ile posho ya usainishaji tu hawahitaji nauli ya kwenda wa nauli ya kurudi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi hilo alione na asione kama tuna ubaguzi kuhusu suala hili, asione kama tunawagua wa Pemba, au tunawabagua wa Kusini na Kaskazini sote ni wa Zanzibar na nia yetu ni kufanikisha adhma hii.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba sababu iliyofanya wasichukue walimu wengi Pemba ni ufinyu wa bajeti. Je, ni kiasi gani walimu hao wanacholipwa kwa kufanya kazi ya kusahisha mitihani.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza walimu mbali ya ile posho ya kawaida ambayo tunawalipa kwa usainishaji ni kati ya 125,000/= mpaka 150,000/= inategemea namna ambavyo mwalimu atasainisha lile rundo la karatasi ambazo atasainisha.

Mhe. Spika, vile vile mwalimu huwa tunamlipa chakula na malazi hii hatumlipi *cash* kwa sababu kawaida hawa wasainishaji tunawaweka pahala pamoja kwenye kambi na hawatakiwi kutoka. Kwa hivyo, huwa tunawahudumia chakula na malazi, lakini kama mwalimu tumemtoa Pemba mbali ya chakula na haya malazi huwa tunamlipa na sh. 30,000/= za mkononi, mbali ya hizi za usainishaji nilizozisema mwanzo.

Nam. 21

Kuanguka Nguzo Za Umeme Kengeja

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Malengo makubwa ya kuwepo Shirika la Umeme Zanzibar (*ZECO*) ni kutoa huduma ya nishati ya umeme na kuzingatia usalama kwa wateja wake Unguja na Pemba.

Mhe. Waziri, inakuwaje kwa muda mrefu sasa nguzo za umeme zimeanguka katika Skuli ya Kengeja na kutishia usalama wa wanafunzi katika eneo hilo, bila ya kufanyiwa matengenezo, wakati uongozi wa skuli umetoa taarifa mapema kunakohusika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Aliuliza:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 21 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza nikubaliane na wewe kuwa lengo la wizara yangu kupitia Shirika la Umeme ni kutoa huduma ya nishati ya umeme na kuzingatia usalama kwa wananchi wa visiwa hivi, hivyo hitilafu yoyote inayojitokezea ya umeme nashauri itowe taarifa katika sehemu inayohusika. Katika kujibu swali mama ni kwamba nguzo zilizoanguka skuli ya Kengeja zimesharekebishwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

a) Je, kuna utaratibu gani wa kupeleka mafundi kila Mkoa ili kurahisisha kazi hii kutokana na usumbufu wanaoupata wananchi.

b) Kuna *line* za zamani ambazo zina *line* ya kopa, je wizara yako ina mpango gani wa kurekebisha suala hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, ni kweli kwamba pana *line* ambazo za waya wa kopa zisizokuwa na ngozi, pamoja na marekebisho ambayo tumeyafanya ya kubadilisha nguzo zilizokuwa mbovu, lakini pana *line* ambazo hazina ngozi. Kwa hivyo, wizara yangu kupitia Shirika la Umeme tayari inalishughulikia suala hili kwa nyaya hizo na kuweka zenye ngozi ambazo zitakuwa zina uwezo wa kuchukua kiwango kikubwa cha umeme. Mhe. Spika, kwa sababu nyaya zilizokuwepo ni nyaya za Nam.25 kwa hiyo tutaweka waya wa 50 ambao utakuwa una usalama zaidi kwa wananchi.

Mhe. Spika, utaratibu huu wa kuweka mafundi kila Mkoa Unguja na Pemba tayari tumeshauanza na kwa sasa hivi kwa Kaskazini Unguja tumefungu kituo cha umeme gamba na Chake Chake na Mkoani kwa Pemba. Kwa hivyo, tunategemea mpaka itakapofika 2013 basi Zanzibar kila Mkoa itakuwa tumeshawaweka mafundi rasmi litakapotokea tatizo lolote la umeme waweze kulitatua bila ya wafanyakazi wengine kuondoka Mjini na kuwafuatilia mashamba.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kuweza kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri hivi sasa katika shirika lako ni kwamba nguzo hakuna. Je, wizara yako ina mpango gani wa kuweza kuleta nguzo nyengine ambazo zilizokuwa hazina dawa za *chemical*.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nguzo tunazo za kutosha kwa muda huu na zipo Shirika la Umeme, nguzo ambazo zenye kiwango ambazo zinatoka Afrika ya Kusini. Lakini pale zitakapopunguza nguzo hizo basi wizara yangu imejipanga vizuri kwa kuagizishia nguzo nyengine kabla ya kumalizika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa inafahamika kwamba kazi kubwa ya Shirika la Umeme ni kutoa huduma kwa wananchi. Na kwa kuwa inafahamika sasa kwamba shirika limejiweka zaidi kibiashara. Je, ni upi msimamo wa serikali juu ya mabadiliko haya ya kisera kwa shirika.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lengo kuu ni kuhakikisha kusambaza miundombinu ya umeme kila kijiji Unguja na Pemba. Katika kujipanga

serikali kupitia wizara yangu ili kuliimarisha suala hilo ni kutafuta wawekezaji na kuweka umeme mbadala na hilo tayari nimejibu katika suala lilopita kwamba tumejipanga vizuri na itakapofika wakati basi sote tutapata taarifa.

Nam. 95

Kukiukwa Utekelezaji wa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu

Mhe. Raya Suleiman Hamad – Aliuliza:-

Mhe. Waziri kwa nini barabara pamoja na majengo yanayojengwa wakati huu hayazingatii matakwa ya sheria ya watu wenye ulemavu ya kuzingatia matumizi ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali Nam. 95 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya miradi ya maendeleo na hata ya barabara inajengwa pasi na kutoa umuhimu unaostahiki kwa jamii ya watu wenye ulemavu. Kama sote tunavyofahamu suala la watu wenye ulemavu ni suala la mtambuka na ni imani yangu kwamba serikali itaendelea kulifanyia kazi ili kuona jamii hii nayo inapatiwa ufumbuzi katika masuala hayo. Aidha, kwa upande wa miundombinu hasa barabara tunatarajia uchambuzi na uchunguzi unaoendelea chini ya ufadhili ya Benki ya Dunia kwa barabara zote zinazoingia Mjini Unguja suala hilo litazingatiwa kwa umuhimu unaostahiki.

Mhe. Spika, kwa upande mwengine napenda nitoe wito kwa madereva na watumiaji wengine wa barabara kuheshimu sheria ili kufanikisha utekelezaji wa matumizi ya barabara na kuheshimu sheria za barabarani kwa watu wenye ulemavu likiwemo suala la matumizi ya fimbo nyeupe.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri ni lini mtarekebisha kanuni zetu na kujua kwamba kuna watu ambao wanaohitaji barabara na majengo kwa kupita kwa miguu au kwa vyombo na mambo mengine, naiomba wizara yako itujuilishe lini wataweka sheria hizo ili ziweze kukidhi haja kwa watu hao.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, suala alilouliza Mhe. Mwakilishi linahusiana na taasisi mbili, taasisi ya kwanza ni kile kitengo chetu cha Idara ya Usafiri na Leseni katika idara hii sheria yetu Nam. 7 ya 2003 ya masuala ya usafiri tayari suala hili limeshazingatiwa na ndio maana katika jibu mama tukaeleza kwamba tunawataka watumiaji wa barabara wakiwemo madereva kuheshimu sheria za vivuko kwa maana ya zebra pamoja na matumizi ya fimbo nyeupe.

Mhe. Spika, upande wa pili tumeeleza kwamba tuna ufadhili wa *World Bank* anatufanyia *study* na tuliingia nao mkataba mwaka jana chini ya kampuni ya *ICT* na *APEX* ya Dar es Salaam study hii imechukua muda wa mwaka mmoja tunatarajia katika mwezi huu wa April watatuletea majibu. Mhe. Spika, mategemeo yetu kwamba *study* hii itakapokuja itaweza kuonesha kuwa ile fursa ya pembezoni mwa barabara kuweza kujenga njia ambazo wataweza kupita watu wenye ulemavu, watumiaji wa baiskeli na watumiaji wa miguu nalo litazingatiwa katika *study* hiyo mpya ambayo tunatarajia kupata majibu yake katika mwezi wa April wa mwaka huu.

Nam. 31

Utanuzi wa Bandari ya Mkokotoni

Mhe. Panya Ali Abdalla – Aliuliza:-

Mhe. Rais wa Zanzibar katika ahadi zake za kampeni za uchaguzi 2010 alitamka kuwa bandari ya Mkokotoni kuifanya iwe ya kisasa ili iweze kutoa ajira na kuongeza pato la taifa.

a) Je, Mhe. Waziri wizara yako ina mpango gani wa kushughulikia ujenzi wa bandari hiyo ili kuhakikisha mapato ya serikali yanapatikana na kutimiza ahadi ya Mhe. Rais.
b) Mhe. Waziri itachukua muda gani mpaka ujenzi huo kuanza.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu kupitia Shirika la Bandari la Zanzibar katika mipango yake ya muda mrefu ya uimarishaji wa bandari ya Unguja na Pemba ina mpango wa kuijenga bandari ya Mkokotoni ili iweze kutoa huduma kwa vyombo na mizigo inayoingia bandari hapo pamoja na kuwasaidia wananchi wa maeneo husika.
Mhe. Spika, katika kipindi tofauti shirika limeweza kuzijengea na kuimarisha gati za Wesha na Wete kwa kutumia uwezo wake wa ndani, na bandari ya Mkokotoni inategemewa kujengwa kwa kutumia uwezo wa ndani wa shirika au ufadhili wa nje pale tutakapompata. Mhe. Spika, ujenzi wa bandari hiyo itaanza mara tu shirika litakapopata uwezo wa kifedha au kupatikana mfadhili kama tulivyoeleza awali.

Mhe. Spika, katika kutimiza adhma hii Shirika la Bandari limeiomba Kampuni ya Road and Bridge ya China kufanya utafiti wa kina wa namna bora ya ujenzi wa bandari hiyo pamoja gharama zitakazoweza kukidhi ujenzi wa bandari hiyo.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana kuniruhusu niulize swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa bandari ya Mkokotoni inaonekana kukua kwa kasi. Je, serikali haioni iko haja yakuipa kipaumbele ujenzi huo ili kuweza kuzuia uvujaji wa mapato ya serikali pamoja na kupata wananchi wetu ajira.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba bandari ya Mkokotoni inakuwa kwa kasi inawezekana ikawa kichecheo cha ajira na pato kwa serikali. Lakini Mhe. Spika, sote tunavyotambua kwamba katika kipindi hiki mkakati wa serikali ni kuimarisha bandari yetu kubwa ya Malindi kama tunavyotambua kwamba mpango wa serikali tuko mbioni kutafuta ufadhili ili kuweza kujenga bandari nyengine kubwa itakayoweza kukidhi mahitaji haya na mengine ili kuweza kuongeza pato la serikali yetu. Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba tutakapoweza kukamilisha mradi wa bandari kubwa ya maruhubi suala hili la Mkokotoni nalo litapatiwa ufumbuzi.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali kwamba hivi sasa tayari tumeshapata wenzetu hawa wa Kampuni ya Road and Bridge ya China wanaendelea kufanya *study* wacha tuwasubiri pengine *study* yao inaweza ikaja na matunda mazuri na kuweza kupata ufadhili wa kuweza kujenga gati hii ya Mkokotoni sambamba na ile adhma ya serikali ya kujenga gati kubwa ya Maruhubi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu bandari ya Mkokotoni imeahidiwa kujengwa kwa siku nyingi na bandari hii bado ujenzi wake haujapewa tarehe za kuanza. Mhe. Spika, kwa sababu bandari ya Mkokotoni ni sehemu moja ambayo kuwa inaingiza vyombo vingi kutoka Tanga, kule kunakuwa kunakwenda vitanda, makabati na vifaa vyengine ambavyo kuwa vimeingiza mapato katika serikali.

Je, Mhe. Naibu Waziri kucheleweshe kujengwa kwa bandari hiyo haioni kama mapato ya serikali ya kuingiza kodi zinavuja. Na je, kama hazivuji ni kiasi gani kinapatikana kwa mwaka katika bandari hii ya Mkokotoni.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano katika usimamizi wetu wa kazi kuna bandari takriban ni bandari tano tunazozisimamia Zanzibar, lakini bandari hizo zote bandari yetu kubwa ni ile ya Malindi. Mhe. Spika, tunachokiamini sisi kwamba tukiimarisha bandari ya Malindi pato la serikali litakuwa kubwa litakaloweza kusaidia kupata fedha ili kuweza kujenga hizo bandari ndogo ndogo.

Mhe. Spika, pasi na kuimarisha bandari yetu ya Malindi hiyo dhana ya kutaka kujenga na kuimarisha hizo bandari ndogo ndogo tutashindwa kuifikia. Hivyo, basi namuomba Mhe. Mwakilishi atupe muda wa kuendelea kuimarisha bandari yetu kubwa ya Malindi ili kuongeza pato kwa serikali yetu na kujiimarisha kwa shirika hili ili kuweza kupata fedha zitakazoweza kusaidia uimarishaji wa bandari hizi ndogo ndogo ikiwemo ya Wesha, Wete pamoja na hiyo ya Mkokotoni.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, pamoja na kuwa Mhe. Naibu Waziri amesema kuwa tuimarishe bandari ya Malindi iingize pato katika nchi na kupata uwezo wa kushughulikia bandari nyengine.

Ni vizuri lakini Mhe. Naibu Waziri hajui kuwa ile kutokuwepo na bandari kubwa upande wa pili wa Zanzibar kule Pemba kunachangia mapato mengi kupungua kwa sababu serikali ilisema kuwa bandari ya Mkoani itakuwa ni mlango wa kimataifa wa kuingilia, nayo haishughulikiwi ikawa katika visiwa hivi viwili tuna bandari kubwa mbili ambazo pia zitasaidia katika lengo alilokusudia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, dhana ya serikali ni kuimarisha miundombinu na uimarishaji wetu wa bandari hizi unaenda sambamba naamini Mhe. Mwakilishi yeye mwenyewe atakuwa shahidi namna ya bandari ya Mkoani matengenezo yanaendelea na uimarishaji wa vifaa vinavyotumika.

Mhe. Spika, napenda kulithibitishi Baraza lako tukufu kwamba mipango ya Shirika la Bandari watakapoweza kukamilisha vifaa vyao ambavyo wanavyo hivi sasa katika bandari ya Malindi mtazamo wao wa pili ni kuimarisha vifaa katika bandari ya Mkoani. Mategemeo yetu kwamba watakapoweza kupata vifaa hivyo kwa bandari ya Mkoani yale malengo ya serikali ya kufungua mlango kwa bandari ya Mkoani vyombo vikubwa utakuwa umetimia. Mhe. Spika, pamoja na hayo hivi sasa bandari ya Mkoani tayari imeshaanza utaratibu wa kupokea meli kubwa kama tulivyopokea meli kubwa ya watalii miezi miwili iliyopita.

Nam. 49

Fedha za Timu ya Taifa ya Zanzibar

Mhe. Nassor Salim Ali – Aliuliza:-

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi kuhusiana na michango ya fedha zilizochangwa kwa ajili ya Timu ya Taifa ya Zanzibar, ambayo Mgeni Rasmi alikuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mr. Dr. Ali Moh'd Shein.

(a) Je, Wizara inajua ni kiasi gani cha fedha zilizochangwa katika harambee hiyo.

(b) Je, Wizara inawaambia nini wapenzi wa mpira wa miguu Zanzibar kuhusiana na timu yao ya Taifa (*Zanzibar Heroes*) kushiriki mashindano hayo kama watoto yatima na huku wakijua timu yao imechangiwa fedha kwa ajili ya kushiriki vizuri katika mashindano hayo ya *Challenge Cup 2011.*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli kumekuwa na malalamiko mengi juu ya fedha zilizochangwa na Kampuni ya *Future Century* kwa niaba ya *ZFA* na kwa lengo la kupata fedha za kuihudumia timu yetu ya Taifa yaani *Zanzibar Heroes*. Kazi hiyo ya kuchangia fedha ilifanywa kwa nia njema kabisa na ndio maana kwa uzalendo wa wananchi wetu pamoja na wadau wengine walijitokeza kuichangia *Zanzibar Heroes* ambapo mgeni rasmi alikuwa ni Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Ali Moh'd Shein. Baada ya maelezo hayo, naomba kujibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inatambua kiasi cha fedha zilizoahidiwa na kukusanywa katika harambee hiyo ni jumla ya shilingi 67,981,100/-. Fedha hizo zimetumika kuihudumia timu hiyo ya Taifa ikiwa ni pamoja na kuigharamia maandalizi ya timu kwa ajili ya mashindano ya kombo la Kagame yaliyofanyika mjini Dar-es-Salaam.

b) Mhe. Spika, wizara yangu inawahakikishia wapenzi wa mpira wa miguu kwamba mikakati mbali mbali inaandaliwa kwa mashirikiano kati ya *ZFA*, baraza la Michezo na Wizara ili kuhakikisha kwamba timu yetu ya Taifa yaani *Zanzibar Heroes i*nashiriki vyema katika mashindano yote ya kimataifa kwa kujitahidi kuondoa kasoro zitakazojitokeza katika mashindano hayo kwa lengo la kutoifanya timu hiyo kuonekana kama yatima inaposhiriki mashindano hayo.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, wadau wengi wamekuwa wakilalamikia hii *future century* lakini katika harambee ile kuna wadau wengine ambao kuna taasisi za binafsi pamoja na za serikali ambazo zilitoa ahadi za kuichangia timu hii ya taifa. Je, ni mipango gani iliyochukuliwa kwa kufuatilia wale wadau na taasisi ambazo waliahidi kuchangia timu hii ya taifa.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli katika harambee ile ilipatikana kiasi hicho ambacho kimetajwa kwenye majibu mama, lakini kwa kawaida pale kinachotamka sio kwamba ni *cash* vyengine vinakuwa viko mikononi mwa watu bado hawajatoa, wengine wanaahidi na wengine hali ndio kama hiyo. Kwa hivyo, matokeo yake utakuta matumizi yalikuwa makubwa zaidi kuliko kile ambacho kimeahidiwa pale. Kwa hivyo, mpaka leo kuna wengine hawajatoa hata hivyo naamini wizara itafuatilia kwa wale ambao waliahidi na hawajatoa ili kufanikisha masuala haya, ahsante sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, mbali na michango inayochangwa katika timu ya taifa je serikali imejipanga vipi kuchangia timu za Wilaya ambazo zimeshindwa kushiriki katika mashindano yao.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ni kweli lakini hivi sasa kweli wizara imechukua hatua nyingi yakuzungumza na wafadhili na hivi sasa tumepata si chini wafadhili watatu ambao wako tayari kuizigharamia mechi hizo, kwa hivyo, namuomba Mhe. Mwakilishi aweko subra mambo yako njiani, ahsante sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipatia fursa ya kuuliza swali dogo sana la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa mashindano ya *challenge* ni miongoni mwa mashindano makubwa sana katika Afrika Mashariki, na kwa kuwa chombo kinachosimamia michezo Zanzibar (*ZFA*) inaonekana wazi kwamba kimezongwa na mizozo kiasi ambacho wameshindwa hata kusimamia Kombe la Mapinduzi pale waliposimamisha ile kamati ya mdau mkuu wa michezo katika nchi hii Mhe. Raza, na kwa kuwa matayarishao ya Timu ya Taifa yanatumia kwa kiasi kikubwa fedha za walipa kodi. Je, kuendelea kuwaachia *ZFA* matayarisho ya timu yetu ya taifa huku tukishiriki tu bila ya kuleta upinzani na ushindi ambapo ndio matarajio ya taifa letu, si kuharibu fedha za walipa kodi wetu. Hilo moja.

Pili, ni lini uongozi wa wizara hii inayoshughulika na mambo ya michezo utafanya marekebisho pale *ZFA*, ili tupate yale tunayoyahitaji tusitarajie kuvuna nanasi wakati tumepanda mchongoma. Ni lini watafanya marekebisho ya *ZFA* ili tupate kile kitu tunachokihitaji katika nchi hii.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, jana katika swali Nam. 48 wizara ilijibu kwa ufasaha mkubwa masuala ya migogoro na mivutano iliyomo ndani ya Chama cha Mpira wa Miguu Zanzibar (*ZFA*). Na tukaeleza kwamba hivi sasa wizara imeipa kazi Baraza la Michezo kushughulikia taratibu nzima zinazohusiana na migogoro iliyopo na tukajibu kwamba, kwa mamlaka aliyonayo waziri anayeshughulikia michezo kupitia sheria na kanuni mbali mbali ikibidi hatua ngumu zitachukuliwa ili kuondoa migogoro hiyo.

Kwa hivyo, ninalomuomba Mwakilishi atupe nafasi ndogo wakati Baraza la Michezo linamalizia shughuli zake za kiutawala, tunaamini kwamba tutapata mafanikio. Sasa mafanikio basi hatua tunazochukua ili kuhakikisha kwamba Chama cha Mpira wa Miguu cha Zanzibar kimekuwa chama ambacho kitaleta ustawi wa soka hapa nchini.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Naibu Waziri, Waziri wa Habari pamoja na Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa majibu. Waheshimiwa Wajumbe nafikiri kuna makoseo kidogo katika *order paper* hii, kulikuwa na shughuli inayohusu Waziri wa Kilimo na Maliasili ya uanzishwaji wa Taasisi ya Kilimo, ambayo ndani ya *order paper* haionekani kama shughuli ile haikumalizika na inabidi iendelee.Basi kwa nafasi niliyonayo na kwa uendeshaji bora wa shughuli za Baraza naomba sasa tuendelee kwa kumuita Mhe. Waziri wa Kilimo kufanya majumuisho ya ule mswada ambao umewasilishwa jana ambao tuliahidi kuwa majumuisho yatafanyika mara baada ya kipindi cha maswali. Mhe. Waziri karibu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho juu ya mswada ambao jana tuliupitia na tunaendelea nao hivi leo. Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho ya michango ya Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuhusu Mswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Zanzibar.

Mhe. Spika, pia naomba niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe kwa kuuchangia vizuri mswada huu. Napenda kuwahakikishia Wajumbe kuwa michango yao, maelekezo na ushauri wao tumeupokea na tutaufanyia kazi ipasavyo kadiri ya uwezo utavyoruhusu kwa utekelezaji mzuri wa majukumu ya kazi na maendeleo ya Taasisi ya Kilimo Zanzibar.

Mhe. Spika, naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mhe. Salmin Awadh Salmin, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Wajumbe wake wa kamati hiyo ya Baraza la Wawakilishi kwa michango yao na maelekezo. Na tena nasema tunaahidi kwamba wizara itafanya kazi maelekezo na ushauri uliotolewa kwetu sisi.

Mhe. Spika, naomba tena nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote waliochangia ikiwa pamoja na waliochangia kwa maandishi. Mhe. Spika, naomba niwataje kwa majina wachangiaji wafuatao ambao walichukua nafasi yao adhimu ya kutoa mchango kwenye mswada wangu huo wakiongozwa na:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin
2. Mhe. Saleh Nassor Juma
3. Mhe. Hassan Hamad Omar
4. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
5. Mhe. Shawana Bukheti Hassan
6. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak
7. Mhe. Asha Bakari Makame
8. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi
9. Mhe. Panya Ali Abdalla
10. Mhe. Suleiman Hemed Khamis
11. Mhe. Mohammed Haji Khalid
12. Mhe. Asha Abdu Haji
13. Mhe. Hija Hassan Hija
14. Mhe. Salim Abdalla Hamad
15. Mhe. Fatma Mbarouk Said
16. Mhe. Rufai Said Rufai
17. Mhe. Ashura Sharif Ali
18. Mhe. Abdalla Juma Abdalla
19. Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Na wale ambao walipata fursa ya kuchangia kwa njia nyengine (kwa maandishi) yupo Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, Mhe. Ussi Jecha Simai, Mhe. Nassor Salim Ali na Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako sasa naomba kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kama ifuatavyo. Wengi wa wajumbe waliochangia waliipongeza serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili na kuunga mkono uamuzi wa serikali wa kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar. Mhe. Spika, nachukua fursa hii kuwahakikishia wajumbe kuwa maoni na maelekezo yao tunayachukua na kuahidi kuyafanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, wajumbe wengi waliochangia waligusia suala la upatikanaji wa pembejeo za kilimo. Mhe. Spika, suala la pembejeo limetekelezwa kama tulivyoeleza katika bajeti yetu aidha wakati Mhe.Waziri wa Kilimo alipokuwa akijibu maswali. Mhe.Waziri alieleza kwa ukamilifu hatua zilizochukuliwa kufanikisha suala hili. Hata hivyo, kilichojitokeza ni kwamba wakulima wengi wamejitokeza zaidi ya lengo lililowekwa, wizara tayari imeshachukua hatua za dharura kufanikisha suala hili.

Mhe. Spika, miongoni mwa maeneo ambayo Waheshimiwa Wajumbe walitoa maoni na maelekezo kwa msisitizo ni kuhusu suala la usafi, suala la bajeti ndogo kwenye masuala ya utafiti. Pia kutilia mkazo utafiti kwa masuala ya mazingira na vianzio vya maji na utafiti juu ya udhibiti wa wadudu waharibifu na maradhi ya mimea kama vile muhogo, migomba na kadhalika. Pia utafiti juu ya uangamizaji wa nzi wa matunda, utafiti juu ya uvuvi endelevu, utafiti juu ya masuala ya misitu na utafiti juu ya matumizi bora ya ardhi.

Mhe. Spika, kwa kuendelea ni kwamba pamoja na maelezo ya jumla napenda kujibu hoja moja moja za wajumbe kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, kuhusu kuingiza neno “uvuvi” kila penye neno “kilimo”. Naomba kuwaarifu Wajumbe kwamba katika mswada huu kifungu cha pili kimefafanua kuhusu tafsiri ya neno “kilimo” ambayo pia imejumuisha suala la uvuvi. Pia Mhe. Spika, napenda kukubaliana na hoja za Waheshimiwa kwamba kuna haja kubwa ya kufanya utafiti katika maeneo ya misitu na kuangalia sababu zinazopelekea upotevu wa misitu. Misitu yetu imekuwa ikipotea kwa kasi kubwa sana. Vile vile suala zima la kuzifikisha taarifa za utafiti mapema kwa walengwa, wizara italifanyia kazi ipasavyo.

Pia Mhe. Spika, suala la uzamiaji baharini kuwa hili halihusiani na sheria hii ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo. Hata hivyo, naomba kuwaarifu wajumbe kwamba suala hili liko mikononi mwa sheria ya uvuvi ambayo ndiyo inayotoa masharti ya kuzamia.

Pia nakubaliana na ushauri wa Waheshimiwa Wajumbe wa kufanya utafiti katika maeneo ya maweni ambayo ndio asilimia kubwa ya ardhi ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, pia napenda kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wajumbe kuhusiana na migongano inayoweza kutokea katika utekelezaji wa sheria hii hasa kwa vile sheria hii zaidi inahusiana na masuala ya utafiti tu na sio suala la kusomesha. Ama suala la kutajwa wizara zaidi ya moja katika sheria hii suala si tatizo kisheria, wizara hizi zitafanya kazi kwa mujibu wa utaratibu unavyoonesha kwenye sheria husika na wala hakuna mgongano wowote utakaojitokeza kwa sheria hizi. Utaratibu huu unatumika katika sheria nyingi nchini na hata kwenye sheria ya uhakika wa chakula na lishe.

Mhe. Spika, suala la wataalamu kukaa ofisini, wizara tayari kwa upande wake imeshalichukulia hatua. Hata hivyo, wizara itaendelea kulishughulikia suala hili kama Waheshimiwa Wawakilishi walivyoelekeza, na tayari Idara ya Kilimo imeshahamishiwa Kizimbani badala ya kuwepo mjini.

Mhe. Spika, suala la utafiti kwa kila kanda, tayari utafiti wa aina hii umefanyika kwa kushirikiana na wataalamu kutoka Uingereza. Ripoti kamili ya utafiti ambayo inajulikana kama *farming system zones* ipo na wizara inaendelea kuitumia, na utafiti wa aina hii unaendelea kufanywa kulingana na mahitaji.

Mhe. Spika, suala jengine linaloendelea ni kuhusiana na suala la muhuri wa taasisi kutumiwa na Mkurugenzi au mtu mwengine atakayepewa ruhusa na mkurugenzi, hili ni jambo la kawaida kufanyika. Mara zote iwapo kiongozi mmoja anaondoka kwenda safari au kwa shughuli nyengine mtu anayekaimu ofisi huachiwa dhamana kwa mujibu wa utaratibu, kwani anayekaimu ni lazima atekeleze majukumu. Kwa hivyo, ikiwa pamoja na kutuma na kujibu barua na shughuli zote zile kwa mujibu wa taratibu za utumishi.

Suala jengine Mhe. Spika, ni kuhusu utafiti wa mbegu. Wizara inalishughulikia kikamilifu, mara nyingi tatizo kubwa ni sehemu au eneo linalolimwa mbegu hizo, kama nilivyoeleza hapo juu kuwa utafiti wa kikanda unaeleza zao gani, pande, na maeneo husika. Wizara itachukua hatua ya ziada kuwaelimisha wakulima kuhusiana na suala hili.

Kwenye sheria hii katika kifungu cha 5(1) (f) kimeeleza utaratibu wa uanzishaji wa vituo vidogo vidogo vya utafiti katika maeneo ambayo itaonekana kuna haja ya kufanya hivyo kwa lengo la kuendeleza kilimo chetu. Kuhusu suala la wakulima kusaidiwa nyenzo za kilimo hili tayari shirika limeshafanya kazi kwa ukamilifu. Suala hili limefanyiwa kazi, kwani katika msimu huu wa ukulima wa mpunga wakulima wamepatiwa huduma za matrekta, mbolea na mbegu kwa njia ya ruzuku. Lengo kuu likiwa ni kuwasaidia wakulima hao. Hata hivyo, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wawakilishi kuwa serikali itaendelea kulifanyia kazi suala hili kadiri wakati utavyoruhusu.

Mhe. Spika, suala la rasilimali watu.Hili limeonekana uzito wake na kwa mujibu wa sheria hii hata viwango vya elimu vimeainishwa ili kuhakikisha kwamba kazi za utafiti zinatekelezwa kikamilifu na kiutaalamu. Aidha, hivi sasa tayari taasisi imeshapeleka wafanyakazi zaidi ya kumi masomoni katika ngazi tofauti kuanzia diploma mpaka *degree* ya tatu.

Kuhusiana na utafiti shirikishi, Mhe. Spika, kifungu cha 5(1) cha sheria hii tayari kimeelekeza rasmi utaratibu na utafiti shirikishi. Mhe. Spika, upatikanaji wa nyenzo, vitendea kazi, mbegu, wanyama na pembejeo nyengine tayari wizara imejipanga kwa hilo na imeshaaza kuwasiliana na taasisi mbali mbali za nje na ndani katika kusaidia suala hili.

Suala la maabara ya uchunguzi. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Zanzibar inayo maabara zaidi ya 300, maabara hizo zinafanya uchunguzi wa udongo, wadudu, mimea na maradhi. Kuhusu suala la Mjumbe kutoka *SUZA*, ingawa katika kifungu cha 6(1) (b) sheria imeelekeza kwamba mjumbe mmoja atatoka katika taasisi ya elimu ya juu inayoshughulika na utafiti. Hii inabainisha kuwa anaweza kutoka *SUZA* au taasisi nyengine yoyote ile. Hata hivyo, ili kuondoa utata pendekezo la wajumbe kuwa mjumbe huyo atoke *SUZA* bado tutaendelea kulifanyia kazi na kujaribu kulichunguza.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mbegu za kienyeji, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo tayari inazo mbegu za aina mbali mbali za mazao tofauti. Taasisi hiyo inazo mbegu za kienyeji kama vile migomba, muhogo, mbogamboga, viazi

na nyenginezo, lakini mbegu hizo zitahifadhiwa na zinaendelea kufanyiwa utafiti na zile zinazofanyika vizuri katika mazingira yetu zitagawiwa kwa wakulima kwa ajili ya kuziendeleza.

Mhe. Spika, kuhusu upatikanaji wa taarifa za utafiti za taasisi kwa watu waliokuwa nje ya Zanzibar. Taarifa hizo zinapatikana katika Tovuti ya wizara yenyewe ya Wizara ya Kilimo. Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa na sasa basi niwahoji wale wanaokubaliana na hoja wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba, Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza Zima ili kuupitia Mswada kifungu kwa kifungu. Naomba kutoa hoja.

KAMATI YA BARAZA ZIMA

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo

Kifungu cha 1 - Jina fupi na kuanza kutumika
Kifungu cha 2 - Ufafanuzi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 3 - Kuanzishwa kwa taasisi
Kifungu cha 4 - Muhuri wa taasisi
Kifungu cha 5 - Kazi na uwezo wa taasisi pamoja na marekebisho yake
Kifungu cha 6 - Kuanzishwa na muundo wa Baraza pamoja na marekebisho yake

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nazungumza kifungu hiki na hasa kifungu cha 6(1) (b) ambapo kutakuwa na wajumbe wane, na wawili kati ya hao walisemwa ni wanawake, nikasema kwamba wanawake si tatizo, lakini tuseme basi kwamba lazima mjumbe mmoja atoke *SUZA*.

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu amesema kwamba kuna kifungu kinachosema kwamba mjumbe huyo atatoka kwenye taasisi ya utafiti. Tuna mazoea kwamba Zanzibar serikali yetu mara nyingi inatumia wataalamu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na hatupati faida ya Chuo Kikuu chetu cha Zanzibar. Kwa hivyo, bado mimi namuomba Mhe. Waziri akubali kwamba kwenye Baraza hili katika taasisi hii lazima mjumbe mmoja tumtoe *SUZA* sio mtaalamu mwengine, tuseme *SUZA* ndio ombi langu.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu hicho cha 6(1) (b) kati ya wajumbe wa nne angalau wawili anasema watoke sehemu ya wanawake. Hilo nasema ikiwa wanao uwezo wa kuingia basi hakuna sababu ya kuwazuia wasiingie.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu hapa ilikuwa kwamba kifungu cha 6(1) (b) sehemu ya nne ya kirumi kuna wajumbe wanne ambao watateuliwa na Mhe. Waziri, na akasema kwamba wawili kati ya hao lazima wawe wanawake, nikasema sina tatizo, lakini kwa hofu ambayo tumeijenga kibinafsi mara nyingi hatupati mchango wa Chuo Kikuu chetu cha *SUZA*, kuja kuwatumia wataalamu wetu. Kwa hivyo, nilichosema hapa kwamba lazima Mhe. Waziri anikubalie kuwa mjumbe mmoja kati ya hawa wanne awe mke au mume tuseme kwamba lazima atoke *SUZA* ili Wazanzibari wapate mchango wa *SUZA* kwenye Baraza hili la utafiti.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mimi sioni kisa cha kufanya upendeleo. Kwa sababu kina mama uwezo wanao lakini tusiende kwenye *SUZA* tu, twende katika vyuo vyote ambavyo tunavyo hapa, wanao uwezo tuwachukue awe mwanamke awe mwanamme, lakini sio Chuo cha *SUZA* tu aa, sasa vyuo vyengine vitakuwaje, tuvivunje?

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri hoja ya Mhe. Mjumbe ni kwamba katika hawa wajumbe wanne basi kutoka taasisi ile ambayo inahusu mambo ya utafiti anasema taasisi hiyo iwe ni *SUZA* atoke huko ndio anayotaka yeye isemwe moja kwa moja. Majibu hapa umesema kwamba suala hilo litazingatiwa kuhusu mjumbe wa aina hiyo kuweza kutoka kwenye *SUZA*.

Sasa yeye anasema kwa kuwa mara nyingi tunakosa kutumia wataalam wetu basi itajwe moja kwa moja kwamba mjumbe huyo atoke *SUZA*. Nafikiri Mhe. Mjumbe ni sawa. Sasa unasemaje katika hilo Mhe. Waziri.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, nafikiri bado sina usemi wowote tusianze kubagua.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi namheshimu sana Mhe. Waziri kwa sababu ni mwenzangu sana. Lakini hapa hatuangalii kubagua tunachosema sisi wajumbe wako unapotutuma hata Kamati yangu ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii wataalam wa *SUZA* wanalalamika kwamba hivyo nchi hii imejenga *SUZA* kwa faida gani, kwa nini hata utafiti wa mdudu wa embe achukuliwe Dar es Salaam, sisi wataalam wa *SUZA* tuna faida gani.

Kwa hivyo, ninachofanya mimi tumwambie mtu wa *SUZA* atupe mtaalam mmoja na hawa wataalam wengine mnaowatafuta tushirikiane kufanya utafiti, lakini Wazanzibari wanataka waone mchango wa *SUZA* kwa utafiti wa nchi ni upi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri anikubalie katika hili na nilimuomba mwanzo kwamba afanye busara tuseme kwa sababu yeye amesema kwamba itatoka katika utafiti. Kwa uzoefu wetu atakuja mtaalam kutoka nchi yengine ataajiriwa *SUZA* wanalalamika, *SUZA* ni mali yetu Wazanzibari kwa nini hatuwapi nafasi nao tukaona mchango wao. Mimi namuomba sana Mhe. Waziri anikubalie kwamba taasisi ya utafiti hii mjumbe mmoja tumtoe *SUZA* kama *SUZA* awe mwanamke au mwanamme lakini atoke *SUZA*.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Mwenyekiti, hili suala limeshamalizika tutakaa na Mhe. Mwakilishi nafikiri tutaangalia hali halisi yeye anakovuta na mimi ninakovuta lakini tutaweza kulitatua hili suala. Kwa mujibu anavyosema yeye tutaangalia huko mbele tunakokwenda je, hivi vyuo vyengine lazima tuwe tunajaribu kuitazama hali nzima ya vyuo isiwe tunakitazama chuo kimoja tu. Maadam ni mzalendo amesoma hapa amepata shahada yake huwezi ukamzuia wakati nafasi ipo. *SUZA* atakwenda na kama kuna mwengine pia atakwenda. Kwa hivyo, asiwe na wasi wasi kama akitaka kati ya wanne tumeshasema kati ya wanne wawili wawe wanawake *gender*. Hiyo inatosha lakini tusiseme tena kwamba lazima kiwe chuo hichi, vyuo viko vingi hapa hapa na wanaosoma ni watoto wetu tusiwe na desturi ya kutaka kubagua kwamba hichi cha *SUZA* tu.

Tunashughulikia mambo ya utafiti tusianze tena kuanza mapema tukasema hawa ndio hawa sio. Tunataka kufanya utafiti tufanye utafiti *very serious* na wala tusichague mtu kwa sababu ya fulani na fulani, tunataka watoto wawe *very competent* na vyuo ambavyo vitakuwa maadam tunasema ni Mzanzibari kapata sio lazima atoke *SUZA* lakini na chuo chengine chochote basi tumpe kazi hii.

Mhe. Mwenyekiti, *gender* nakubaliana nayo kwamba kati ya wanne angalau wawili wawe wanawake. Lakini tukija kwenye suala la uwezo basi tuwaweke wale wenye uwezo tusiseme kwamba maadam hii ni nafasi ya *SUZA* ambapo kuna vyuo vyengine vimetoa watu *very competent* kuliko kile tukasema aaa hii ni nafasi ya *SUZA* tu peke yake tutazame kwa upana wake.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri hoja ya Mhe. Waziri nimeifahamu kama hivi inavyofuata ili labda tufikie pahala tuelewane vizuri. Hapendelei tujifunge na *SUZA* peke yake kwa ajili ya kutafuta mtu mtafiti aliye bora. Tunaweza tukenda kwenye taasisi nyengine ya utafiti isiyokuwa *SUZA* kama kuna mtu aliye bora zaidi. Nadhani ndio anachokusudia Mhe. Waziri.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa busara zako na Mhe. Waziri. Kifungu hichi kina wajumbe wanne, watatu tuwawekee hawa ambao wataonekana wazuri zaidi, mmoja atoke *SUZA* ili Wazanzibari waone mchango. Kwa tulivyo hapa maana yake Wazanzibari watoe fedha watafute watu wanne nje ya nchi wakati ndani tunao.

Labda Mhe. Waziri anambie hatuwaamini *SUZA*, kama hatuwaamini maana yake tumeteleza, lakini mimi naamini kwamba *SUZA* tunao uwezo. Sasa mimi namuomba Mhe. Waziri hawa watatu tumuachie atafute hao wataalam wa nje ili na mtu mmoja wa ndani awepo tushirikiane. Lakini kutoa fedha kwa wataalam wa nje wote bila ya kupata mchango wa wataalam wa ndani ambao mimi naamini wapo hii hatuwafanyii haki wataalam wetu. Lakini kama Mhe. Waziri anaona *SUZA* hawana maana akanambia kwamba hawana uwezo kwa hivyo tuendelee. Mimi siamini kama hawana uwezo, naamini wana uwezo tunao pale wazuri, juzi nilikuwa China na maprofesa pale kutoka *SUZA* wazuri Wazanzibari leo kwa nini tusiwape nafasi moja kati ya hizi nne.
Mhe. Mwenyekiti, uzoefu mimi kamati yangu inakwenda mara zote tafiti ndogo ndogo pale zinafanywa na watu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam lakini *SUZA* tunao wataalam wazuri. Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri anikubalie hii moja tuwagaie *SUZA* na hizi tatu tuwaachie hizo nafasi nyengine za kutoka nje.

Akinikatalia namuomba aende lakini hayo madhara yake maana yake *SUZA* hatuifanyii haki, Wazanzibari hatufanyii haki.

Mhe. Mwenyekiti: Hivi tunai-*recast* vipi ili kuchukua hoja zote mbili. Kwa sababu nadhani zote mbili zina umuhimu, kuzingatia kwamba tupate wataalam wa ndani ina umuhimu, lakini kuzingatia kwamba tupate mtaalam aliye bora zaidi pia ina umuhimu ambaye inawezekana asiwe kutoka taasisi zetu za ndani. Tunai-*recast* vipi ili iwe inakidhi yote, nafikiri ndio kinacho umuhimu hapa, labda tusaidiane kuhusu hapa.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani tumesikia busara za Mhe. Waziri na pia *concern* ya Mhe. Hija Hassan Hija. Lakini bado tunabakiwa na lile suala la msingi kwamba hii ni taasisi ya utafiti tena wa kilimo. Kwa hivyo, tatizo liliopo ni kwamba unaweza ukaiweka *SUZA* lakini *SUZA* yenyewe pengine isiwe na hiyo *faculty* ya kilimo au isiwe na mtu mzuri *distinguished* wa kilimo akawepo katika taasisi nyengine ambayo pengine sio *SUZA*. Ndio ile busara ya Mhe. Waziri na hizi zote ni taasisi zetu.

Kwa hivyo, mimi labda kwa kulihakikishia hilo nadhani lile suala la kile kijifungu kinachozungumzwa ile (b) tungeiacha vile vile kwa sababu hii ni *mandate* ya Waziri. Kama ataona kuna mtu pengine kutoka *SUZA* ambaye mzuri atasaidia anaweza akaingia hapa. Lakini mimi nadhani kwa ajili ya kui-*refine* ili pengine kuileta karibu zaidi SUZA au taasisi zetu labda ile ya *roman (i)* tungei-*refine* kwamba Mwakilishi kutoka Taasisi ya Elimu ya Juu Zanzibar inayoshughulika na utafiti ili kuhakikisha kwamba hiyo taasisi yenyewe ya elimu ya juu basi ni iliopo Zanzibar.

Labda tungeongeza lile neno Zanzibar ingeikaribisha zaidi *SUZA* lakini pia kutoa nafasi itakapotokea kwamba kuna mtafiti mzuri zaidi kutoka katika taasisi nyengine ya elimu ya juu. Kwa sababu *SUZA* ni katika *ownership* kwamba ni chuo cha serikali, lakini zote zilizopo Zanzibar bado ni zetu za Zanzibar vile vile kama nchi. Kwa hivyo, mimi nadhani tui-*refine* ile ya *roman (i)* ili ionekane kwamba tunakusudia iwe ni taasisi ambayo ipo Zanzibar badala ya kuiweka *SUZA* peke yake.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nadhani busara za Mhe. Mwanasheria Mkuu na mimi namheshimu sana naomba tuendelee kwa kuweka neno Zanzibar kwa maana ya mtaalam huyu atoke Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, tunafanya marekebisho kwenye *roman (i)* Mwakilishi kutoka Taasisi ya Elimu ya Juu Zanzibar. Mhe. Waziri nafikiri sawa sawa.

Kifungu cha 6 - Kuanzishwa na Muundo wa Baraza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 7 -Kazi za Baraza pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 8 -Vikao vya Baraza na Mwenendo wake pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 9 -Uteuzi wa Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 10 -Kazi za Mkurugenzi pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 11 -Uteuzi na Kazi za Afisa Utafiti Mkuu wa Kilimo pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 12 -Kuanzishwa kwa Kamati ya Kitaalam pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 13 -Kazi za Kamati.
Kifungu cha 14 -Taarifa Kuwasilishwa kwenye Taasisi.
Kifungu cha 15 -Masharti yanayohusiana na Ugunduzi.
Kifungu cha 16 -Ugunduzi na Ubunifu.
Kifungu cha 17 -Fedha za Taasisi.
Kifungu cha 18 -Uwekezaji wa Fedha za Taasisi.
Kifungu cha 19 -Makisio ya Bajeti ya Mwaka pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 20 -Hesabu za Taasisi.
Kifungu cha 21 -Taarifa ya Mwaka.
Kifungu cha 22 -Ukaguzi wa Hesabu.
Kifungu cha 23 -Uwezo wa Waziri kutunga Kanuni pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 24 -Makosa na Adhabu pamoja na marekebisho yake.
Kifungu cha 25 -Makosa ya Jumla.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati yako ya Baraza Zima imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu pamoja na marekebisho yake wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo

(Kusomwa kwa mara ya pili)

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya 2012 usomwe mara ya pili. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wale wanaokubaliana na mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulikubaliwa na kupitishwa)

Mhe. Spika: Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe pamoja na Mhe. Waziri kwa kazi hiyo nzuri.

KAULI ZA MAWAZIRI

Taarifa ya Serikali kuhusu Maombi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kuongezewa Eneo la Uishio wa Nchi Baharini

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Wataala*, nakushukuru na kukupongeza wewe mwenyewe kwa uongozi wako makini kwa Baraza letu. Uongozi wako umesaidia kujenga demokrasia na umakini ndani ya Baraza ambayo ndio iliyopelekea leo nisimame mbele ya Baraza hili tukufu kutoa taarifa hii rasmi ya serikali.

Pili, niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango na maoni yao katika usimamizi sio tu wa chombo chetu lakini pia katika uendeshaji wa nchi yetu.

Mhe. Spika, katika kikao kilichopita cha Baraza la Wawakilishi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa ahadi mbele ya Baraza hili tukufu ya kulitafakari suala la maombi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongezewa eneo la uishio wa ardhi baharini *(Extension of Continental Shelf).* Aidha, serikali iliahidi kwamba baada ya kulitafakari suala hili itatoa taarifa mbele ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, pamoja na ahadi hiyo ya serikali Mhe. Ismail Jussa Ladhu alitoa hoja mbele ya Baraza hili tukufu ya kutaka shauri hilo lizungumzwe na Baraza kwa vile ni jambo muhimu na la dharura. Katika hoja yake hiyo alipendekeza wakati serikali itakapolizungumza shauri hili izingatie baadhi ya mambo yaliyoainishwa katika hoja yake hiyo. Kufuatia hoja hiyo Baraza hili tukufu liliamua kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, aliwahoji Waheshimiwa Wajumbe:

"Waheshimiwa Wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba masuala haya yakazingatiwe na serikali na baadae kutuletea taarifa kama tulivyokubaliana mwanzo, ikichanganya pamoja na lile suala la kuiomba serikali isimamie yale maazimio ambayo yalikuwepo kama ni

pendekezo la ziada wanyanyue mikono.. (Hoja iliamuliwa na kuafikiwa).” Huo ni ukurasa wa 74 wa *Hansard.* Mwisho wa kunukuu.

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Kikao cha Baraza la Mapinduzi cha tarehe 14 Januari, 2012 kilitafakari shauri hilo pamoja na Azimio la Baraza kufuatia hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Kufuatia mazingatio hayo serikali inawasilisha taarifa hii kama ilivyoahidi.

Mhe. Spika, kwanza tunafahamu kwamba dhana ya ukanda maalum wa kiuchumi baharini *(Exclusive Economic Zone – EEZ)* na dhana ya Uishio wa Nchi katika Bahari *(Continental Shelf)* pamoja na mfumo mzima wa sheria za ndani na za kimataifa zinazoongoza suala hili ni dhana ya kitaalam sana na vile vile ni mpya kwa kiasi fulani. Kwa sababu hiyo kwanza naomba nitangulie kwa kutoa ufafanuzi kwa urefu kidogo kuhusu dhana hizo ili Waheshimiwa Wajumbe wapate faida ya kufahamu vyema kiini hasa cha shauri hili.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa makubaliano ya kimataifa ya sheria za bahari nchi yenye kupakana na bahari *(Coastal State)* ina haki ya matumizi ya bahari kwa sehemu tatu. Kwanza, ni sehemu ya maji ya kitaifa ya bahari yenye upana wa maili za bahari (nautical miles) kumi na mbili (12NM). Katika eneo hili nchi husika ina mamlaka yote ya kiutawala sawa na nchi kavu.

Pili, ni eneo la ukanda maalum wa kiuchumi *(Exclusive Economic Zone)* lenye upana usiozidi maili za baharini mia mbili (200 NM). Kimsingi hili ni eneo la bahari ya kimataifa lakini nchi husika ina haki ya kipekee ya kuvuna mali na rasilimali zote ziliomo na kuchukua hatua za kiulinzi na za kimatumizi ya rasilimali hizo lakini nchi haina mamlaka yoyote ya kiutawala sawa na eneo la bahari ya nchi.
Eneo hili pia hutambuliwa kuwa ni eneo la bahari ya kimataifa lakini watumiaji wake wanatakiwa kuheshimu mamlaka ya nchi husika kuhusiana na uvunaji, ulinzi na uhifadhi wa rasilimali ziliomo.

Tatu, ni eneo la uishio wa ardhi ya nchi baharini *(Extended Continental Shelf)*. Kitaalam inaaminika kwamba eneo la nchi kavu baada ya ufukwe mara nyingi ardhi ya nchi hiyo haiishii kwenye ufukwe wake huzama kwa maili nyingi kuelekea baharini. Kwa kuwa ardhi hii iliyozama na ile iliyobaki kuwa ni ya nchi kavu ina jiolojia (mfumo wa miamba) ya aina moja, ni dhahiri kwamba kwa pamoja rasilimali ya ardhi iliyozama na iliyobaki kihistoria ni milki ya nchi hiyo moja.

Kwa wastani, muishio huu wa ardhi baharini hukadiriwa kuwa hizo maili mia mbili (200 NM). Ndio maana kumekuwa na dhana kwamba *EEZ* na Muishio wa Ardhi Baharini *(Continental Shelf)* ni kitu kimoja. Lakini kuna nchi ambazo muishio wa ardhi yake baharini ni zaidi ya maili 200. Hapo ndipo nchi hiyo hupewa fursa ya kudai muishio huo wa ardhi baharini kwa maili 150 zaidi au zisizozidi 150.

Katika eneo hili nchi ina haki sawa na zile zilizonazo ndani ya eneo la ukanda maalum wa kiuchumi isipokuwa nchi nyengine nazo zimepewa haki kubwa zaidi ya matumizi ya eneo hili. Kwa mfano, haki ya kuvua na kutandika nyaya za chini ya bahari. Aidha, eneo hili kwa mujibu wa ibara ya 86 ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria za Bahari ya 1982 ni sehemu ya bahari kuu *(high sea)* tofauti na *EEZ* ambayo haitambuliwi kuwa ni sehemu ya bahari kuu ingawa ni sehemu ya maji ya kimataifa.

Mhe. Spika, ili kufahamu vyema dhana hii ni vyema pia kuelewa taratibu za kupata au kutambuliwa kisheria kwa nchi kuwa mmiliki wa maeneo ya bahari tuliyoyataja. Kwa upande wa eneo la bahari ya nchi *(territorial waters)* ni kwa nchi yenyewe tu kuitambua mipaka yake hiyo na kukubaliana na majirani zake ili kuuondoa mzozo wa mipaka. Baadhi ya nchi kufuatisha hatua hiyo kwa kupitisha sheria ya mipaka yake ya bahari *(territorial waters delimitation law).*

Kwa upande wa eneo la *EEZ* nchi husika baada ya kuitambua na kusawazisha masuala ya maingiliano ya mipaka na jirani zake, hupitisha sheria ya kuitambua na kuiainisha mamlaka yake kisheria ndani ya eneo hilo. Kwa upande wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utaratibu huu wa kuitambua na kuitangaza mamlaka ulifanyika kupitia Sheria ya *EEZ* ya mwaka 1989.

Mhe. Spika, kwa upande wa eneo la uishio wa ardhi baharini utaratibu wake wa kulipata ni tofauti kabisa, kwani ni lazima nchi itimize vigezo vya kitaalam kama vifuatavyo:

Kwanza, lazima sehemu ya mwambao wa nchi husika iwe imeingia baharini kimaumbile *(natural submarine prolongation of the land mass of the coastal state).*

Pili, lazima uwepo uthibitisho wa kitaalam wa mipaka ya eneo hilo ulioambatanishwa na michoro ya maumbile ya miamba, taarifa za kijiolojia *(geodetic data)* na taarifa nyengine muhimu ambao umewasilishwa kwa maandishi kwa mamlaka husika ya Umoja wa Mataifa kama inavyoelekezwa na ibara ya 76 (9) ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria ya Bahari.

Tatu, lazima nchi husika iwasilishe madai rasmi ya uhalali wake wa eneo hilo kwa chombo mahsusi cha Umoja wa Mataifa kilichopewa dhamana ya kushughulikia utambuzi wa eneo hilo.

Nne, madai hayo lazima yawasilishwe ndani ya muda maalum uliowekwa kwa nchi zote na ndani ya muda mahsusi uliowekwa kwa kila nchi. Hivyo, ni dhahiri kwamba utaratibu wa nchi kudai muishio wa ardhi baharini kuitwa ni upanuzi wa eneo la *EEZ* ni mazoea tu lakini ukweli halisi na wa kitaalam ni kwamba kinachofanyika ni kudai sio kuomba ongezeko la muishio wa ardhi ya nchi husika baharini na wala sio kuongeza eneo la *EEZ* kwani hakuna kitu kama hicho katika Sheria za Bahari.

Mhe. Spika, usimamizi wa masuala ya bahari kuwa Madai ya Ongezeko la Muishio wa Ardhi Baharini ambao ndio tuliutaja hapo mwisho uko chini ya Kamisheni ya Ukomo wa Muishio wa Ardhi Baharini *(Commission on the Limits of the Continental Shelf - CLCS)* iliyo chini ya Divisheni ya Masuala ya Bahari na Sheria ya Bahari *(Division for Ocean Affairs and the Law of the Sea - Doalos)* ambayo kwa kifupi tumeieleza.

Mhe. Spika, kamisheni hii ndio msimamizi wa utekelezaji wa kifungu cha 76 aya ya 4 mpaka ya 7 ya makubaliano haya ambazo ndizo zinazoruhusu madai ya nyongeza ya muishio wa ardhi ya nchi baharini. Kwenye utekelezaji wa zoezi hili kamisheni hii ilitoa agizo kupitia hati yake Nam. DOALOS/07-01406 ya tarehe 14 Agosti, 2007 kuzitaka nchi zote wanachama ambazo hazijatangaza nia ya kudai nyongeza ya mwisho wa ardhi zao baharini ziwe zimearifu sekretarieti ya kamisheni hiyo, azma hiyo sio zaidi ya tarehe 30 Novemba, 2007. Nchi 27 ziliitikia wito huo, ikiwemo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kadhalika kwa hati yake nambari FPLOS/INS/20 ya tarehe 16/01/2008, kamisheni ikatoa ratiba ya muda wa kila nchi kuwasilisha maombi yake, kwa mujibu wa ratiba hiyo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ilitakiwa iwe imewasilisha maombi yake kabla ya Mei 2009, ilifanya hivyo tarehe 05 Mei, 2009 na ikatakiwa iwasilishe rasmi andiko la madai yake ifikapo tarehe 13 Mei, 2011.

Mhe. Spika, kutokana na sababu mbali mbali ikiwemo tishio la uharamia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa barua nambari CGA336/358/1/77, ikaomba iongezewe muda hadi tarehe 13 Novemba, 2011. Hata tarehe hiyo pia haikuwezekana na hatimaye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikapewa muda wa mwisho wa tarehe 17 Januari, 2012.

Miongoni mwa sababu za utaratibu huu, ni kuratibu maombi ya nchi zinazozunguka eneo moja na pia kuiwezesha kamisheni kujipangia ratiba ya kukamilisha kabisa, kusikiliza madai ya nchi wanachama. Miongoni mwa maombi yaliyopokelewa, kuna nchi kadhaa za Muungano wa aina mbali mbali, lakini kwa nchi zote hizo maombi yaliyopokelewa ni kupitia kwa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa sio nchi au himaya zilizoungana. Nchi kama Canada ambayo iliwasilisha Disemba, 2003, Uingereza kama United Kingdom of Great and Northern Ireland na Urusi mwaka 2001 ni miongoni mwa nchi hizo.

Mhe. Spika, maelezo yaliyotangulia hapo juu yanadhihirisha mambo yafuatayo.

1. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haiombi kuongeza EEZ yake, bali inadai kuongeza mwishio wa ardhi yake baharini.
2. Nchi nyingi zinazopakana na bahari bila ya kujali hali zao za kiuchumi, kijamii na kisiasa, zimeona haja ya kudai nyongeza hii ya mwishio wa ardhi zao baharini. Hivyo, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haikukosea kufanya hivyo.
3. Mawasiliano yote ya Umoja wa Mataifa juu ya masuala haya hufanywa na nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, walioridhia makubaliano ya kimataifa ya sheria za bahari na sio himaya au dola moja moja nje ya Muungano wao.
4. Muda wa madai ya upanuzi wa mwishio wa ardhi baharini una ukomo na kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumevumiliwa sana hadi Januari, 2012 kutoka Mei, 2011. Haya ni madai sio maombi, kwa hivyo hayana namna ya kusitishwa, utaratibu uliopo hautoi fursa hiyo.
5. Eneo linaloombwa kuongezwa sio la nchi yoyote, nchi isipokubaliwa au hata ikijitoa basi litaendelea kubaki kuwa ni la mataifa yote.

6. Kwa nchi zilizoungana mikataba na maridhiano yao ya ndani juu ya mipaka ya kila mmoja wao haibadilishwi na ongezeko la mwishio wa ardhi baharini, ongezeko lenyewe ndani ya Muungano wao, litatafsiriwa kwa mujibu wa mchango wa kila mmoja kwenye nyongeza hiyo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo hatuna budi sasa kuangalia hoja mbili muhimu kama zifuatazo.

1. Je, maombi haya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuongezewa ukomo wa mwishio wa baharini, ni kwenda kinyume na maazimio ya Baraza la Wawakilishi ya tarehe 04/04/2009.
2. Ni kwa kiasi gani maazimio ya Baraza la Wawakilishi ya tarehe 04/04/2009 yametekelezwa na matokeo ya utekelezaji wake.

Hoja ya ombi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenda kinyume na maazimio ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, maazimio ya Baraza la Wawakilishi ya tarehe 04/04/2009, halitokani na hoja ya SMZ kuhusiana na mapendekezo ya uendeshaji wa kazi za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia Zanzibar, ambayo ilitolewa na Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Mhe. Mansour Yussuf Himid, tarehe 03/04/2009.

Mhe. Spika, taarifa hiyo nayo ililetwa mbele ya Baraza la Wawakilishi kutokana na maelekezo ya Baraza la Mapinduzi ya tarehe 27/03/2009, ambayo yalitolewa baada ya kujadili waraka nambari 225/2009, kuhusiana na ripoti ya mwisho ya mshauri mwelekezi juu ya ugawanaji wa mapato na gharama ya rasilimali ya mafuta na gesi asilia ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, kikao hicho kilipitisha maamuzi ya kukubali mapendekezo matatu, ambayo pia ndiyo yaliyoletwa mbele ya Baraza la Wawakilishi kupitia hoja ya Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi. Mapendekezo hayo ni kama yafuatayo;

1. Ardhi na bahari ya Zanzibar maeneo ambayo kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar, sura ya 1 kifungu cha 2(1) ni miliki ya Zanzibar katika maeneo haya usimamizi udhibiti na uendeshaji wa shughuli zote zinazohusiana na utafiti na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia uwe wa Zanzibar pekee, kama katiba yetu na matakwa ya Wazanzibari yanavyoelekeza.
2. Serikali inashauri nyinyi Waheshimiwa Wajumbe kuwa sasa wakati umefika kwa Zanzibar kuwa na chombo chake cha kusimamia mambo yote yanayohusiana na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.
3. Kwa upande wa bahari kuu serikali inashauri Baraza la Wawakilishi kukubali mashirikiano na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa eneo hili pekee. Hii ni nukuu ya Hansard ya tarehe 03/04/2009 katika ukurasa wa 61 mpaka 62.

Mhe. Spika, baada ya kuwasilisha mapendekezo, Baraza hili tukufu liliridhia mapendekezo mawili kati ya hayo matatu. Kwa upande wa pendekezo la tatu, Baraza halikuafiki na badala yake liliazimia, kuwa hata katika eneo la ukanda maalum wa kiuchumi EEZ. Suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia liwe chini ya mikono ya Zanzibar.

Mhe. Spika, maelezo yaliyotangulia yanadhihirisha mambo yafuatayo;

(a) Vyombo vyote viwili yaani Baraza la Mapinduzi na Baraza la Wawakilishi, havijawahi kujadili hoja ya umiliki au usimamizi wa ukanda wa kiuchumi wa bahari kuu na wala havijawahi kupitisha maamuzi ya Zanzibar kumiliki au kuendesha ukanda huo, kilichojadiliwa na vyombo hivyo viwili na hatimae kutolewa azimio na Baraza hili tukufu, ni matumizi ya ukanda huo kuhusiana na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia kwa upande wa Zanzibar.

(b) Kwa kuzingatia maelezo yaliyotangulia, kwamba kinachodaiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuongeza ukubwa wa mwishio wa ardhi baharini, yaani *Extension of Continental Shelf* na sio ukanda maalum wa kiuchumi yaani EEZ.

(c) Kwa kuzingatia kwamba hata nyongeza hiyo ikipatikana hapo baadae haitoathiri madai wala maslahi ya Zanzibar katika suala la utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia katika ukanda maalum wa kiuchumi na pia katika eneo la ziada.

Mhe. Spika, ni wazi kuwa maombi ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kuongezwa eneo la ziada la uishio wa ardhi ndani ya bahari, hayapingani wala kuathiri azimio lolote la Baraza hili tukufu katika maazimio yaliyopitishwa na Baraza hili tarehe 04/04/2009, kuhusiana na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia.

Baada ya hayo Mhe. Spika, labda tuangalie hoja na maazimio ya utekelezaji wa maazimio ya Baraza la Wawakilishi yaliyotokana na hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba serikali kupitia Baraza la Mapinduzi ilipojadili hoja ya maombi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kuongeza eneo la ziada la uishio wa nchi baharini, ilitafakari pia mambo yote yaliyoelezwa katika hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu, pamoja na maazimio ya Baraza hili tukufu yaliyofuatia hoja hiyo.

Mhe. Spika, ufuatao ni ufafanuzi wa maazimio hayo na maelekezo ya serikali katika utekelezaji wake.

1. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iiandikie rasmi Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuitaka isimamishe taratibu zote za maombi ya kutaka kuongezewa ukanda wa bahari kuu kwa zaidi ya maili za baharini 200 *Exclusive Economic Zone* hadi hapo suala hilo litakapopatiwa ufumbuzi wakati wa mjadala wa katiba mpya.

   Mhe. Spika, katika kutafakari azimio hilo serikali ilizingatia mambo 3 makubwa;

   a) Kama ilivyokwisha tangulia kuelezwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haiombi, bali inadai nyongeza ya mwishio wa ardhi yake baharini kwa maili za baharini 150 na sio maili 200 zilizotajwa kwenye azimio hili.

      Aidha, Tanzania haiombi nyongeza ya EEZ, kwa vile hakuna utaratibu huo katika sheria ya kimataifa, ile inadai kuongezwa mwishio wa ardhi yake baharini kama nilivyotangulia kufafanua.

   b) Tunapaswa tujiulize kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaweza kusitisha mchakato huo.Majibu kama nilivyotangulia kueleza katika maelezo ya utangulizi ni kuwa Jamhuri ya Muungano haiwezi kufanya hivyo, kwa vile mchakato wenyewe unatakiwa ufanyike sio tu katika muda maalum, lakini ndani ya muda mahususi kwa nchi na nchi. Hivyo, iwapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itasitisha mchakato huu, basi itakuwa imeondoa madai yake jambo ambalo litakuwa ni hasara kubwa zaidi kwa Zanzibar ambayo inategemea zaidi bahari kwa uchumi wake wa sasa na baadae.

   c) Ni vyema tujiulize kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itasitisha mchakato huo, Zanzibar itaweza kuja kuomba tena kuongezewa eneo hilo ambalo sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inalidai. Jibu la wazi ni kwamba Zanzibar haitoweza kufanya hivyo, kwa vile;

      1) Haina uwezo huo chini ya sheria za kimataifa.
      2) Itakuwa imepitwa na wakati.
      3) Ni kazi inayohitaji gharama kubwa, na
      4) Ni kazi ambayo inahitaji kushauriana na mataifa mengine ya jirani, jambo ambalo ni dhahiri mataifa hayo jirani hayatokuwa tayari kufanya hivyo.

   Kwa mfano, katika mchakato wa kuandaa ombi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Muungano ilifanya makubaliano na Kenya, Comoro na Msumbuji. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kenya, zilitiliana saini makubaliano hayo mwaka 2009. Aidha, kwa mipaka ya Comoro na Msumbuji, makubaliano hayo yalitiwa saini tarehe 05 Disemba, 2011 na mkataba na nchi ya Shelisheli unatarajiwa kutiwa saini kabla ya Mei, 2012.

   Kwa ujumla ni wazi Waheshimiwa Wajumbe, kuwa haitokuwa kwa maslahi ya Zanzibar kufanya hivyo.

2. Azimio jengine lilikuwa ni, Iwapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitochukua hatua ya kusimamisha mchakato huo, basi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ipeleke ujumbe wake na barua rasmi umoja wa mataifa, kuutaka usimamishe kushughulikia maombi hayo, hadi hapo suala la mchakato wa katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania utakapomalizika na kukubaliana maeneo ya ushirikiano na maeneo ambayo kila upande utayasimamia wenyewe.

   Mhe. Spika, kwanza kama nilivyoeleza hapo awali kuwa mchakato huu ulianza tokea mwaka 2007, ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitakiwa kutangaza rasmi nia yake ya kuomba eneo la

ziada la uishio wa ardhi baharini. Tokea wakati huo hatua kadhaa zilichukuliwa kuendeleza mchakato huu, hatua ambazo sio tu zina gharama kubwa ya fedha, lakini zinahitaji utaalamu wa hali ya juu kama nilivyoeleza hapo awali.

Vile vile mchakato huu tokea ulipoanza mwaka 2007 uliridhiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kwa vile hakuna madhara kwa maslahi ya Zanzibar, katika suala hili hakuna sababu wala haja ya kucheleweshe mchakato huu. Tatu ni dhahiri kuwa kama Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakubaliwa na kutambuliwa kuwa mmiliki wa eneo hilo la ziada, haizuii kujadili matumizi na hata usimamizi wa eneo hilo wakati wa mchakato wa katiba mpya.Kama ilivyotangulia kuelezwa mchakato huo hauwezi kuisubiri nchi itakapokuwa tayari.

3. Azimio jengine lilikuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iitake Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kusitisha shughuli zote ambazo zinahusiana na kutumia rasilimali ziliomo ukanda wa bahari kuu EEZ, hadi hapo suala hili litakapomalizwa baina ya pande mbili.

Mhe. Spika, katika kutafuta kipengele hiki serikali imezingatia mambo yafuatayo;

(a) Tunaposema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania izuie shughuli zote katika eneo hili, tunakusudia hata shughuli za uvuvi na matumizi mengine ya eneo hili. Je, zuio hilo litaihusu Zanzibar pia. Kama hivyo ni sawa basi ni vyema tukatanabahi kwamba eneo hilo linatumika kwa shughuli nyingi ikiwemo uvuvi kwa wananchi, usafiri wa ndani na wa kimataifa, utandazaji wa nyaya za mawasiliano na kadhalika. Baadhi ya shughuli hizo ni haki ya Jumuia ya Kimataifa chini ya sheria ya kimataifa ya bahari. Hata Zanzibar pia inalitumia eneo hilo kwa shughuli mbali mbali, hivyo haitowezekana kuzuia shughuli zote katika eneo hilo kwa sababu ni kinyume na sheria, na pia athari zitakuwa ni kwa pande zote mbili.

(b) Katika shughuli za uvuvi wa bahari kuu, Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zina makubaliano maalum katika eneo hilo. Kwa upande wa mapato mgao ni asilimia 40 kwa Zanzibar na asilimia 60 kwa Tanzania Bara. Aidha, makao makuu ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu yamejengwa na yanaendelea kukamilishwa hapa Zanzibar, tayari leseni kadhaa zimeshatolewa. Kwa hivyo, haitowezekana kusitisha shughuli zote katika eneo hilo.

4. Azimio jengine lilikuwa ni iwapo hatua hazitochukuliwa kuhusiana na mambo hayo, basi Zanzibar haitofungika na chochote kitakacho amuliwa kuhusiana na mambo hayo ambayo hayakushughulikiwa na Zanzibar yenyewe.
Mhe. Spika, kwa vile Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haioni haja ya kuiandikia barua Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama ilivyyopendekezwa katika hoja na azimio hilo msingi wa hoja hii bila shaka nao hautokuwepo.

5. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar isimamie utekelezaji wa maombi, maazimio ya Baraza yaliyopitishwa tarehe 04/04/2009.

Mhe. Spika, kwanza ni wajibu wa serikali kusimamia utekelezaji wa maazimio ya Baraza kwa kuzingatia katiba na sheria nyengine za nchi. Hivyo, katika hili serikali imehimiza taasisi zote husika kuchukua hatua muafaka ili kutekeleza maazimio hayo. Miongoni mwa hatua hizo ni kuitishwa kikao cha pamoja baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uenyekiti wa makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. Katika kikao hicho masuala yaliyojadiliwa ni pamoja na suala la kukamilisha taratibu za kikatiba za kulitoa suala hilo katika Muungano.

Pande hizi mbili zimekubaliana kupeana muda maalum wa kulishughulikia suala hili. Mhe. Spika, baada ya kumaliza hoja hizo tano. Mwisho nimalizie kwa maelezo yaliyotolewa na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe, kwamba Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati wakati huo, alifanya makosa kwa wakati ule kwa azimio hili, yaani Mhe. Ali Juma Shamuhuna. Alifanya makosa kwa kutoliarifu Baraza la Mapinduzi juu ya mchakato wa maombi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuongezewa eneo la ziada la uishio wa nchi baharini.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kueleza kwa urefu hapo awali, kwamba mchakato huu ulianza rasmi mwaka 2007. Katika mwaka huu ndio uamuzi wa kisera ulipotakiwa kufanywa na Serikali ya Muungano wa Tanzania na pia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwani ndipo uamuzi wa kuomba kwa utaratibu gani ulipotakiwa

kufanywa. Serikali imeridhika kwamba kumbukumbu ziliopo zinathibitisha kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliarifiwa na kuafiki juu ya ombi hilo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Spika, hatua zote zilizofuata baada ya hapo zilikuwa ni utekelezaji wa maamuzi hayo ya msingi ya kisera yaliyofanywa mwaka 2007. Hivyo, uwasilishaji wa andiko la maombi hayo ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yalikuwa ni ya utekelezaji na sio ya kisera ambayo yangehitaji maamuzi au maelekezo ya Baraza la Mapinduzi. Hivyo, haikuwa lazima suala hilo kujadiliwa na Baraza la Mapinduzi kabla andiko hilo kuwasilishwa katika Umoja wa Kimataifa.

Hata hivyo, serikali imeagiza kwamba taarifa za mambo kama hayo muhimu ya kitaifa, ziwe zinawasilishwa katika Baraza la Mapinduzi, ili kuwezesha serikali yote nzima kupata taarifa hizo muhimu.

Mhe. Spika, mwisho napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru kwa dhati Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa imani, uzalendo na ari waliyoionesha juu ya kulinda na kutetea maslahi ya nchi yao ya Zanzibar. Ingawa katika kujadili suala hili maneno na kauli zilizotumika zilionekana kali na inawezekana ziliwakwaza baadhi ya wahusika katika kujadili suala hili muhimu. Hata hivyo, naamini yote yalikuwa ni kwa nia ya kujenga. Naamini taarifa hii ambayo imefafanua suala hili kwa kina, itaturejesha katika safu ya pamoja ya kusimamia na kutetea maslahi ya nchi yetu na watu wake. Aidha, bila shaka tutakuwa tumejifunza kwamba linapotokea jambo lenye shaka, kuitaka serikali kulifanyia kazi na kutoa taarifa mbele ya Baraza hili tukufu ni utaratibu wa busara na unaofaa kutumika. Mhe. Spika, baada ya hayo naomba nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Niwashukuru Waheshimiwa Wajumbe kwa kunisikiliza kwa makini na kwa utulivu. Mhe. Spika, baada ya hayo, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe.Mwanasheria Mkuu.Taratibu za kanuni zinatutaka kwamba tumkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ili kutoa maoni ya kamati hiyo. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Ali Abdalla Ali (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, juu ya taarifa ya Serikali ya kuhusu hoja ya maombi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuongeza eneo la uishio wa nchi baharini.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii adhimu kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kunijaalia afya njema na uhai miongoni mwetu na tumeweza kukutana hapa leo hii asubuhi.

Mhe. Spika, napenda pia kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, ili kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, juu ya taarifa ya Serikali kuhusu hoja ya maombi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuongeza eneo la uishio wa nchi baharini.

Mhe. Spika, pia napenda kutumia nafasi hii kumpongeza na kumshukuru Mhe.Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuandaa na hatimae kuwasilisha taarifa ya serikali kuhusu hoja hiyo ya maombi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya kuongeza eneo la uishio wa bahari.

Mhe. Spika, kwa taarifa hii muhimu, hasa kwa kuzingatia kuzungumzia maslahi ya Wazanzibari.Vile vile nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwa umakini wake na ufuatiliaji wa haki za Wazanzibari mpaka akafikia hatua ya kutoa hoja ndani ya Baraza lako tukufu. Alitaka shauri hilo lizungumzwe na Baraza la Wawakilishi vile vile maana ni jambo muhimu sana katika nchi yetu. Mhe. Spika, napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa kamati, kwa kunipa mashirikiano makubwa katika kazi zetu, naomba niwapongeze na niwatakie kila la kheri kwenye jambo hili kubwa liliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, ili kuzipa nguvu shukrani zetu hizo napenda niwatambuwe wajumbe wa kamati hii kama ifuatavyo;

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Mwenyekiti wa Kamati
2. Mhe. Panya Ali Abdalla	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Mjumbe
4. Mhe. Mussa Ali Hassan	Mjumbe
5. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Mjumbe
6. Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Mjumbe
7. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
8. Ndg. Nasra Awadh Salmin	Katibu

9. Ndg. Abubakar Mahmoud Iddi Katibu

Mhe. Spika, baada ya pongezi hizo napenda sasa niende moja kwa moja katika taarifa ya Serikali. Mhe.Spika, katika kikao kilichopita miongoni mwa ahadi zilizotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilikuwa ni hii ya utoaji wa taarifa juu ya hoja ya maombi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuongezewa eneo la uishio wa nchi baharini. Pamoja na kuyazingatia maazimio yaliyotolewa na Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, kwa kuwa nchi zilizoungana mikataba na maridhiano yao ya ndani juu ya mipaka na kila mmoja wao hayabadilishiki na ongezeko la mwisho la ardhi ya baharini. Hivyo, Mhe. Spika, naliomba Baraza lako tukufu liondowe wasi wasi juu ya suala hilo, hasa ukizingatia kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hawaombi ongezeko la EEZ yake, bali inadai kuongeza mwisho wa ardhi yake baharini na sio ukanda maalum wa kiuchumi wa bahari kuu.

Mhe.Spika, naomba ieleweke kuwa eneo lililoombwa kuongezwa sio la nchi yoyote, nchi isipokubaliwa itaendelea kubaki katika mamlaka ya kimataifa.Hata hivyo, kwa kuzingatia muda na madai ya upanuzi wa ukomo, ni vyema tukapata baraka zetu na ndugu zetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kulipata eneo hilo hasa tukizingatia kwa madai yasiyo na maombi.

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa, ipo kwa ajili ya kulinda na kutekeleza maslahi ya Wazanzibari, na mchakato huu wa madai unaoongezwa mwisho wa ardhi ya baharini, tokea ulipoanza mwaka 2007 uliridhiwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, hasa ukizingatia kutokuwa na madhara yoyote kwa maslahi ya Wazanzibari katika suala hili. Pia haizuii kujadili matumizi hata usimamizi wa eneo hilo wakati wa mchakato wa katiba mpya unapoendelea.

Mhe. Spika, pamoja na mambo mengine kamati yetu inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kusimamia na kutekeleza maazimio ya Baraza ikiwa ni pamoja na kuitisha kikao cha pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika maridhiano waliyokubaliana ni pamoja na kulitoa suala hilo katika Muungano.

Mhe. Spika, kwa muhtasari haya ndio maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, pamoja na maoni yangu binafsi.Naomba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii, wanayo fursa ya kutoa maoni mmoja mmoja ambayo mimi sikuyataja.

Mhe.Spika, napenda sasa niwashukuru tena Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa kunisikiliza kwa makini na kwa kuniruhusu wewe kusimama mbele ya Baraza hili tukufu, nikushukuru tena wewe kwa mara ya pili.

Mhe. Spika, mwisho napenda kutamka bayana kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala na kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Mfenesini kwamba naunga mkono hoja ya Taarifa ya Serikali kuhusu hoja ya maombi ya jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuongezewa eneo la uishio wa Nchi Baharini asilimia mia **(100%)** na nawaomba Wajumbe wenzangu wote wa Baraza waichangie na hatimae wairidhie Taarifa hii muhimu kwa maslahi ya Nchi yetu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa wajumbe, hiyo ni taarifa ya kamati ambayo inaiunga mkono taarifa ya serikali.

Kanuni zinatuelekeza kwamba masuali ndio yaaweza kuruhusika ili kuuliza kwa Mwanasheria Mkuu kama kuna jambo bado halijafafanuka vizuri, karibuni Waheshimiwa wajumbe kwa masuali.

UTARATIBU

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nieleze kwamba kifungu cha 151 kanuni kwa kuwa hoja hii wakati wa kikao cha *breffing* tulikubaliana kwamba iletwe katika Baraza lako hili kwa ajili ya kuijadili, kwa kuwa makubaliano yetu katika *breffing* yalielekeza kwamba tuilete katika Baraza ili tuijadili badala ya kuletwa kama ni kauli ya Mawaziri.

Lakini Mhe. Spika, jambo hili ni zito na limegusa maslahi ya Taifa na wananchi wengi wanalisubiri kwa hamu jambo hili, lakini vile vile nakumbuka katika kikao kilichopita serikali ilisema kwamba italeta taarifa kama

ilivyofanya leo, lakini ni wakati huo ambao ndio leo wawakilishi wananchi tutapata muda mzuri wa kujadili suala hili baada ya serikali kuleta kauli.

Mhe. Spika, kwa sababu hizo tatu naomba niitumie kanuni hiyo ya 151 ili Baraza lako liridhie kutengua kanuni ya 43 ili hoja hii tuijadili chini ya kanuni ya 33.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe kuhusu utaratibu wake sisemi kama tumekosea isipokuwa anataka kutoa hoja kwamba tutenge kanuni kando, badala ya kuwa ni taarifa kwa mujibu wa kanuni ya 43 haijadiliwi tuitenge kanuni kando hiyo na sasa iwe ni kujadiliwa. Ndicho anachokisema maelezo yote yaliyokuja ni sahihi Hansard inaeleza hivyo kwamba ilikuwa iletwe taarifa na taarifa imekuja, anachoomba yeye kwa kutumia kifungu hicho ni kwamba taarifa hii badala ya kuwa tuulize maswali kama ilivyo chini ya kanuni ya 43 basi tuijadili, unapojadili jambo basi unataka ufikie pahala kwa maamuzi, ndio maana hizo hoja zinazokuja hizo tunafikia pahala tunaamua juu ya hoja ile.

Hili tunataka tufikie kuamua nini ndio suala baada ya taarifa hii ambayo iko wazi na kamati ya Katiba na Sheria imeunga mkono, wala haiathiri yale maazimio yetu tuliyoyatoa kuhusiana na kutafuta na kuchimba mafuta na gesi asilia.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwanza ningelitoa hoja kwa kanuni ya 151 suala la kuomba kaununi itengwe kando liwe halijadiliwi lakini kutokana n abusara zako kuuliza hilo suala la msingi kama unataka kutoa maamuzi gani.

Mimi naamini kwamba kutokana na maelezo ya taarifa ya serikali humu humu yapo baadhi ya mambo ambayo tungeweza kupata maelekezo ya ziada kwa serikali kuweza kufanyia kazi suala hili, lakini pia katika maelezo yako hapo sasa hivi punde ulipokuwa ukijenga hoja ulisema kwamba serikali imetoa taarifa na kamati imekubaliana nayo. Hili nataka niliweke sawa Mhe. Spika, kwa kutumia kanuni hiyo hiyo ya 43 kwa sababu kanuni ya 43(1) inasema Waziri anaweza kutoa kauli katika Baraza kuhusu jambo lolote ambalo serikali inawajibika, baada ya hapo Mwenyekiti wa Kamati inayohusika anaweza kupewa nafasi ya kutoa maoni ya kamati juu ya kauli hiyo.

Mhe. Mwenyekiti mimi ni mjumbe wa kamati hiyo na nimewauliza wenzangu hapa hakuna katika sisi aliyeitwa katika kamati kukaa kujadili taarifa hii ya serikali, ndio kusema utaratibu kapewa mwenyekiti na mwenyekiti Katoa maoni yake si maoni ya kamati. Na ikiingia katika Hansard Mhe. Spika, kwamba kamati imeunga mkono hoja itafikia pahala hata pa kusema mimi ndio nimeleta hoja hii hapo Mwanza. Mhe. Spika, hili naomba hili liwekwe sawa katika riipoti za Hansard kamati haikukaa kujadili suala hili na yaliyotolewa hapa ni maoni ya Mwenyekiti wa Kamati, lakini nasema nilikuwa nataka kuweka sawa tu.

Mimi zaidi cha kukisaidia kivi chako kwa kusema kwamba tunataka tujadili halafu tupate maamuzi, mimi naamini maamuzi au maelekezo pengine maagizo au maelekezo yanaweza kupatikana kutokana na yale ambayo Serikali imeyagusia katika taarifa yake hii. Mimi naomba sana Mhe. Spika, niungane na Mhe. Omar Ali Shehe kwamba kutokana na uzito wa suala hili na wananchi huko nje wanalisubiri isije ikaonekana kwamba vile baraza letu linajaribu kufunika funika mambo.

Kama alivyosema Mheshimiwa Mjumbe hapa mimi nadhani tukitizama rekodi hazikusema kwamba tutakuja hapa kupewa taarifa tu, naomba ili nilisaidie Baraza lako Mhe. Spika, nirejee kidogo tu siku ilipotolewa hoja ile Mhe. Mwanasheria Mkuu wakati anatoa maoni yake katika mjadala ule katika Hansard Ukurasa wa 64 naomba niseme alisema.

Ukurasa wa 64 unasema "*Mimi nilikuwa napendekeza sana Mhe. Jussa labda stick na haya mapendekezo aliyotoa, serikali iende ikayafanyie kazi haya na baadae tutakapokuja tutakuja kuyajadili".*

Mhe. Spika, naomba sana utuhoji tutengue kanuni kando ili tujadili suala hili kwa maslahi ya Zanzibari. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa nanukuu ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwanza suala la kutenga kando kanuni au kutokutenga kando kanuni ni uamuzi wa baraza, suala tu ni kwamba kama ulivyotuwaidhi kwamba manufaa yake ni yepi na tumetokea kwenye haya maelezo baada ya maadhimio ya baraza, ndio taarifa ya serikali ya utekelezaji wa maazimio ya baraza.

Sasa sijui kama kutakuwa na maamuzi tena juu ya utekelezaji huo lakini cha msingi nirudi kwenye ile hoja ya Mhe. Jussa aliposema kwamba baraza lilisema hivyo, lakini baraza kama kanuni zinavyosema kwamba kinachozingatiwa ni maazimio ya baraza sio majadiliano ya baraza. Kwenye majadiliano mnaweza kujadili mambo mengi lakini situ cha msingi cha kuzingatia ni maazimio baraza liliazimia nini na Kumba Kumba pia katika Hansard ukurasa wa 74 nadhani Mhe. Jussa aliishia 54 hakwenda mpaka mwisho.

Lakini ukurasa wa 74 unasema ifuatavyo:"*Mhe. Spika, ahsante sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa majumuisho haya, waheshimiwa wajumbe sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba masuala haya yakazingatiwe na serikali na baadae kutuletea taarifa kama tulivyokubaliana Mwanza ikichanganya pamoja na lile suala la kuomba serikali isimamie maadhimio yale ambayo yalikuwepo kama ni pendekezo la ziada wanyanyue mkono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda".*

Kwa hivyo azimio la baraza ndio hilo sio lile la ukurasa wa 64 ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Hicho ndicho kilichoamuliwa na baraza hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, na mimi nimshukuru Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kuikariri hiyo hata kama ningekuwa sikufika kama alivyosema yeye huko mbele, yeye katusaidia kufika kwa sababu katika utangulizi wa maelezo yake kaikariri vizuri. Lakini tukiisoma vizuri na mimi pia naomba niisome hii imezungumza.

(Waheshimiwa wajumbe sasa niwahoji waliokubaliana na hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba masuala haya yakazingatiwe na serikali na baadae kutuletea taarifa) kama tulivyokubaliana Mwanza ikichanganya pamoja na lile suala la kuiomba serikali isimamie yale maazimio ambayo yalikuwepo kama ni pendekezo la ziada wanyanyue mikono) Hoja iliamuliwa na kuafikiwa.

Sasa Mhe. Spika, taarifa ina maana nyingi wala hakuna haja ya kusema kwamba taarifa haijadiliwi na hata hiyo kauli iliyotumika ya 43 Mhe. Spika, haizungumzii taarifa ya serikali inazungumzia kauli za mawaziri, ningeliifahamu kama inge-*stick* katika hoja zake ingesema hapa azimio liko wazi kusema kwamba serikali ije itoe kauli ya serikali haikusema hivyo. Kwa sababu Mhe. Spika, nasema jambo lolote linatizamwa katika murtaza wa ilivyoamuliwa, kwa hivyo mimi kunukuu kwamba msemaji pekee wa serikali siku ile alikuwa Mhe. Mwanasheria Mkuu na kama alipokuwa anachangia alikuwa analielekeza baraza hili kwamba serikali italichukua na baadae ilete taafira ili kuja kuyajadili mimi nadhani itakuwa hatufanyi kosa katika kufanya hivyo.

Nilisaidie zaidi baraza lako kwa sababu ni muhimu haya tunayoyasema humu tubaki nayo na tuyaheshimu kinyume na hayo inaweza kuonekana kwamba Baraza hili kama vile tunakuja hapa kuzungumza na kuondoka tu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, naomba nirejee Hansard vile vile ya Tarehe 20 ya kipindi hicho hicho ambacho nilikuwa mfululizo nikisema suala hili na tukipata kauli za serikali. Katika Hansard ya tarehe 20 Mhe. Spika, wakati Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais anatoa maelezo baada ya Mhe. Waziri wa Ardhi wakati ule ilikuwa Ardhi Makaadhi, Maji na Nishati kutoa maelezo yake alitoa maelezo haya.

Ukurasa wa 46 wa Hansard ya tarehe 20 Mhe. Spika, inasema. "*Mhe. Spika, niahidi kwamba tumeyapokea maelekezo hayo na sisi katika kikao kijacho cha Baraza la Mapinduzi tutalizungumza suala hili na baadae tuje tutoe taarifa rasmi katika Baraza lako tukufu, hatuwezi kuwa na taarifa ya haraka haraka hatuwezi kusema situ ambacho hakina kina. Lazima tuwe na kitu ambacho tutakieleza kwa kina hapa ili tuweze kuja kufikiria nini chengine cha kuja kukifanya".*

Mhe. Spika, naomba nirejee maneno haya ya kufungia ya Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais yanasema *(Ili tuweze kuja kufikiria nini chengine cha kuja kukifanya).* Mhe. Mwanasheria Mkuu katika mchango wake wa hoja hasa kama alivyosema kasema ananiomba *ni- stick* serikali ikayafanyie kazi haya na baadae tutakapokuja tutakuja kuyajadili.

Sasa Mhe. Spika, kweli ulipotuhoji umehoji hivyo lakini hukuhoji kwamba tutakuja kuletewa kauli ya waziri umehoji kuja kuletewa taarifa, lakini ukichukua *contect* ya majadiliano yalivyokwenda ilikuwa ni wazi kabisa kwamba baraza hili litapewa fursa, sasa Mhe. Spika, nisene kwamba hili suala kama linagusa maslahi ya watu wengi sana hata siku ile ulipokuwa ukiliongoza hapo ulisema nchi nzima inatizama suala hili tunajadili vipi,

sasa nadhani hakuna mwenye dhamira mbaya na bahati nzuri Mwanasheria Mkuu katika maelezo yake kwa niaba ya serikali kwamba hili suala tunalifanya hivi kwa nia ya kujenga.

Sasa nimuhakikishie yeye na niihakikishie serikali kwamba sote nia yetu ya kujenga nadhani tupate nafasi, kama imekuja chini ya kauli ya mawadhiri tutenge kando kanuni ili tupate nafasi ya kutoa maoni yetu, niseme katika maazimio haya kuna azimio ameongeza Mhe. Ali Mzee wakati ule la kuitaka serikali ikasimamie utekelezaji wa yale maazimio ya 2009 ambayo serikali imetoa majibu. Hata tukitizama uzoefu wa mabunge mengine Mhe. Spika, serikali inapokuja kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa baadhi ya mengine bado bunge au baraza linapata nafasi ya kutoa maoni zaidi juu ya utekelezaji. Kwa hivyo niseme kwamba tutenge kanuni kando tujadili kwa maslahi ya nchi yetu na watu wake. Ahsante sana Mhe. Spika, *(Makofi)*

Mhe. Spika: Sina hakika wala sitaki niseme kama kanuni yetu ina mapungufu lakini kwa kawaida taarifa za serikali nimeangalia chini ya ibara 27 ya kanuni zetu haina pahala ambayo ni *se pret* kwa taarifa za serikali, taarifa zilizopo pale ni mbili tu taarifa ya Rais na taarifa ya Spika. Kwa hivyo taarifa nyengine yoyote ya serikali tunazitoa chini ya kauli za Mawaziri ndio utaratibu ambao tumekuwa tunautumia kwa muda mrefu, sasa unapokuja kwenye kauli za mawaziri chini ya ile ibara ya 43 maelekezo yake ni haya.

Kwamba taarifa itatolewa ingawa sasa imeingia na hoja nyengine kwamba Mwenyekiti katoa maelezo ambayo si ya kamati ni maoni yake, hilo ni suala jengine ambalo kiutaratibu nalo sio jambo jema sana maana angalau ingekuwa kuna utaratibu wa kamati wajumbe wamemuelekeza Mwenyekiti akaandike kitu kwa niaba ya waheshimiwa wajumbe hilo lingekuwa ni suala jengine. Lakini pale ambapo kanuni inaelekeza kuwe na taarifa ya kamati kwa kawaida Mwenyekiti huwa anaongoza kikao hicho na pia huwa anawasilisha ile taarifa sasa hilo ni suala jengine, pengine tu kwa siku za usoni tuone kwamba pale ambapo kanuni inahitaji tupate taarifa ya kamati basi ile kamati ipate muda wa kukaa na kuzingatia hilo jambo na hatimae kutoa taarifa kwa niaba ya kamati.

Pengine taarifa moja ya mjumbe wa kamati bila ya idhini ya kamati yenyewe inawezekana isiwe jambo linaloendana na kanuni, sasa kwa mujibu wa hii kanuni ya 151 ya kutenga kanuni kando kwa kweli hakuna suala la kujadili inavyotakiwa na kanuni, kinachohitajika ni kupiga kura. Kupiga kura inawezekana kufanya hivyo shida yake ni kwamba kila linapokuja jambo mkajaribu kutenga kanuni kando haidhuru jambo linaweza likawa ni muhimu vya kutosha, inaweza kuleta tatizo la mtiririko wa shughuli za baraza.

Kwa sababu shughuli zimepangwa kwa muda ili kujaribu kufikia pahala kwa muda ambao ummeupanga shughuli zile zimalizike na bila ya shaka kwa kuzingatia na bajeti iliyokusudiwa kwa ajili ya shughuli hizo, kikao hichi katika vikao vifupi ni kikao kimojawapo ambacho kimechukua muda mkubwa ratiba yetu inatuelekeza mpaka tarehe 20 ndio inavyotwambia. Hiyo ni baada ya mazingatio ya waheshimiwa wajumbe kwamba ripoti za kamati zipate nafasi ya kutosha.

Mimi nafikiri kwa utaratibu bora za kuendesha shughuli zetu na ili tufikie pahala kumaliza shughuli zetu yatakapoingia mambo mengi tutashindwa kumaliza shughuli hizo kwa mtiririko tunaoukusudia, sasa kama hili lina umuhimu wa kulijadili basi isiwe kwenye kikao hiki, kama tunaona umuhimu wa jambo hili kulijadili basi isiwe katika kikao hichi. Kwa huo huo utaratibu wa kutenga kanuni kando kwa hivyo hata kama nitawauliza waheshimiwa wajumbe je kama tunakubaliana kutenga kanuni kando basi jambo hili lije kwenye vikao vinavyokuja siku za usoni, mtiririko wa shughuli zetu utatuvurugia mpaka bajeti.

Waheshimiwa wajumbe nataka nikumbushe tu kwamba hivi sasa nimewapa kazi makatibu wangu hawa waniambie hivi bajeti yetu ya kuendesha shughuli zetu kwa mwaka huu mpaka kufikia June iko je, mwaka uliopita tulishindwa hata kulipia mshahara vizuri na taka wajumbe hilo mulielewe kwa sababu ya kuendelea sana majembo mengine mengi ambayo yameingilia kati. Sasa hilo nalo lina matatizo yake, katika mkutano huu imenijia hoja Mbali ya shughuli za serikali na zile ripoti za kamati ambazo kwa kawaida huwa tunajadili katika mkutano huu imeingia hoja ya Mhe. Hija Hassan Hija tumeiruhusu pamoja na maombi ya Waheshimiwa wajumbe ambao ni halali kabisa kwamba ripoti za kamati zijadiliwe kwa kupewa nafasi kubwa nalo tumejaribu kuzingatia.

Sasa kati ya ripoti ambazo tumezitaka kwa muda mrefu naelezea zile shughuli zetu ilikuwa na ripoti ya Wiara ya Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuhusu Baraza la Manispaa, ripoti ambayo ninazo Kumbu Kumbu kwamba imedaiwa sana ije hapa nayo ilikuja chini ya kauli za mawaziri. Baada ya mazungumza tuliyozungumza pale juu tukasema kwamba hii kutokana na hoja ambazo zilikuwepo kwa muda mrefu hebu Mhe. Waziri ilete kama ni taarifa ya kujadiliwa ametoa taarifa hapa kwamba hiyo ijadiliwe.

Sasa mimi nadhani naweza nikawauliza waheshimiwa wajumbe ili tutenge kanuni kando hii lakini majadiliano ya jambo hili itabidi tuahirishe tutafute muda huko mbele, kikao chetu hiki tumekisogeza sana mbele na sijapata taarifa ya watendaji wangu lakini bajeti yetu imefikia pahala pabaya kutetereka na bado tuna mkutano wa bajeti haujaanza, ambao sehemu kubwa huwa tunatumia bajeti hii inayoishia tarehe 30 June.

Sasa chini ya utaratibu ulivyokuja moja kwa moja inabidi suala hili lisijadiliwe chini ya utaratibu wa hili kanuni ya 43 tukiisoma tutakuta maelekezo hayo, lakini haja ya umuhimu tunasema hiyo kanuni tuitenge kando nayo ni sehemu ya kanuni zetu inayosema hivyo. Lakini ninachosema ni kwamba hali halisi ya mwelekeo wa shughuli zetu inaweza ikaendelea sana na tukafika pahala tukaja tukakwama na kuendesha shughuli zetu za vikao vinavyokuja huko usoni.

Kwa hivyo nataka tukubaliane kwamba tunapoamua hili basi mjadala wake usiendelee kwenye kikao hichi, hilo tukubaliane kwa sbabu ndio hali halisi ya mambo vyenginevyo itatuharibia mtiririko mzima wa shughuli zetu kwa kikao hiki, lakini pia hata mtiririko wa shughuli zetu za bajeti zetu, kwa hivyo nataka tuline hilo mimi sina atatizo kwa jambo muhimu kujadiliwa na serikali tukaisaidia tukaishauri nini cha kufanya. Lakini ukiangalia taarifa hii maana nayo ni hatari kidogo na nataka niwasihi waheshimiwa wajumbe kama kawaida yetu tunapokuwa tunajadili mambo tujitahidi sana Baraza hili lisiingie katika kuamua jambo ambalo kwa mujibu wa taratibu za katiba na sheria ikawa tumevunja hiyo katiba na sheria, pamoja na uwezo wa chombo hiki kuweza kujadili mambo mengi. Sasa hili ni jambo mojawapo ambalo hatuna maamuzi ya moja kwa moja isipokuwa tunao uwezo wa kuishauri serikali nini cha kufanya, hili ni muhimu kwa sababu chombo hiki kuja kufika pahala siku moja kikapandishwa Mahakamani na kuambiwa kwamba kimeamua sivyo ni aibu kwa chombo chetu kama hichi, tunategemewa tuamue mambo ambayo yanaendana na taratibu zote sio tu za kanuni zetu, yanayokuwa ya kanuni nadhani haijambo kwa sababu kanuni ni document yetu lakini katiba zote mbili ni suala muhimu sana hili tulizingatie.

Kwa hivyo kwanza nilitaka nitoe nasaha hizo kwamba mwelekeo wa bajeti yetu sio mzuri hata kidogo, shughuli katika mkutano huu na mambo mengi ambayo tumeyafanya Mhe. Waziri wa Fedha anaelewa na yote yalikua na maana ya kusaidia chombo hichi na wajumbe wake. Tulifanya safari za nje nyingi. Wengi tumefaidika kati ya Mawaziri na wenyeviti wa Kamati mbali mbali, sasa ile imekula mfuko kwa kiasi kikubwa mno. Mwenginemo mpaka tumeanza kufanya *re-allocation* hichi peleka hapa ili mambo yaende.

Kama ilivyotokea kipindi kilichopita kwamba kulipa mshahara tulitumia vifungu vya Pemba. Nadhani mwenyewe yupo hapa Afisa wetu kutoka Pemba, hii hali ndiyo tuliyonayo katika bajeti hiyo. Kama jambo hili tunataka kulijadili basi tusijadili katika mkutano huu, tutizame nafasi nyengine huko siku za mbele, mtiririko wa shughuli zetu unaweza ukavurugika.

Sasa Waheshimiwa wajumbe hapo sitaki hoja zaidi. (*Makofi*)

Mtakubaliana nami kwamba anaposimama mwenyekiti wa wenyeviti inakua kazi kubwa. Inabidi wakati mwengine kiti sasa kitumie rungu. Kwa hivyo hapa sitaki kuleta majadala, lakini tukubaliane kwamba kama tunatenga kanuni kando basi ni vyema kutafuta muda mwengine siku za usoni. Iwe ni kazi ya kuja kuitizama siku za usoni. Tukubaliane hilo kwanza halafu tena tuone kama tunatenga kanuni kando.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo Wapili wa Rais: Mhe. Spika, kwa kua kanuni zetu zinaturuhusu kutupa nafasi ya kuuliza maswali kutokana na kauli za Mawaziri. Na kwa kua bado fursa hiyo hatujaitumia, ningeliliomba Baraza lako tukufu tukaitumia fursa hiyo na baada ya maswali kama kutaonekana kuna hoja ya kujadili jambo hili, basi mjumbe anaweza kunyanyuka na kuona hivyo na baada ya hapo kama ulivyoelekeza tukaweza kupiga kura na tukaamua hoja hiyo. Naomba kuwasilisha Mhe. Spika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nashukuru mimi ndiye mtoa hoja hii kwamba naomba Baraza lako litenge kanuni kando ili tupate muda zaidi. Nadhani Mhe. Spika, wewe una busara kubwa na za hali ya juu.
Kwa msingi huo huo Mhe. Spika, kwa hekima na busara zako, mimi naona kwa sababu jambo hili linagusa maslahi ya taifa na wananchi ni vyema tupate muda wa kujadili. Kwa msingi huo basi naomba tukishakubali kutenga kanuni kando tutumie kanuni ya 63 ili tuweze kuakhirisha mjadala huu na kwa sababu zake kwamba tuseme, kwamba kwa sababu kanuni inatutaka kifungu cha pili tutoe muda. Mimi nipendekeze kwamba tukijaaliwa Ishaallah Mwenyezi Mungu akitujaali Kikao cha mwezi wa 10 tujadili suala hili Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Hivi ukifanya *lobbing* ni lazima mtu umsifu kwanza. Waheshimiwa Wajumbe mimi nadhani tufikie pahala tuamue hili jambo na tuone vipi tutakwenda nalo. Kwa kifupi mjadala wa kikao hichi au mkutano huu haupo. Tunaweza tukaangalia uwezekano wa kutafuta muda huko mbele. Niwahoji basi wale wanaokubali

kutenga kanuni kando ili jambo hili kutafuta muda wa baadae kulijadili jambo hili wanyanyue mikono na wanaosema tusitenge kanuni kando taarifa hii itosheleze na wao wanyanyue mikono. Wanaotaka tujadili jambo hili wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Kwa sasa tupokee taarifa hii, suala la kujadili tuliangalie katika vikao vyetu, mikutano yetu ya usoni. Nashukuru na kwa maana hiyo ile nafasi ya kuuliza maswali sasa inaondoka. Ahsante sana tunaendelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kuhusu jambo jengine lakini linahusiana na hizi hizi kauli za serikali. Nataka twende vizuri katika Baraza. Katika maelezo yako ulivyokua ukilitolea ufafanuzi swali lililopita ulitu-*refer* katika kanuni ya 27 ambayo ilikua inataja kwamba hakuna taarifa ya serikali, zilizotajwa pale ni taarifa ya Rais halafu kuna na kauli za mawaziri. Sasa lilikua nataka kidogo utuwekee sawa vizuri si kwa hili, hili limeshamalizika lakini hata kwa mengine ili tupate muongozo wa kiti vizuri sana.

Mhe. Spika, ukiangalia katika orodha ya utaratibu wa shughuli za Baraza katika Kanuni ya 27(1) pametajwa mambo yameanzia (a) mpaka (m), katika hayo (b) pamezungumzwa "Hati za Kuwasilisha Mezani". Kwa mtiririko huu ilivyokaa ni kama vile "Hati za kuwasilisha Mezani" ni kitu kinachojitegemea na hakijumuishi haya maneno mengine yaliyotajwa hapa. Ukisoma kanuni ya 32 inafafanua kwa urefu "Hati za kuwasilishwa Mezani" Hata hivi leo tukisoma *Order paper* ingelikua ile hoja inasimama utakuta taarifa ya Mwanasheria Mkuu imeorodheshwa katika "Hati za Kuwasilishwa Mezani" na hivyo hivyo taarifa ya Mikopo ya Bodi ya Elimu ya Juu. Kwa hivyo ikaambiwa itumike ile Kanuni ya 43 kwamba hizi kauli za Mawaziri tusijadili.
Lakini hapo hapo hoja ya serikali juu ya ripoti ya Baraza la Manispaa ya Mji wa Zanzibar ni sehemu ya "Hati za kuwasilishwa Mezani" lakini imekuja kama hoja ya serikali. Haidhuru katika mririko wa shughuli hapa kuanzia (a) – (m) hakuna hoja ya serikali. Ndio maana nilikua nasema ni vizuri ikae vizuri ukitoa muongozo wa jumla. Na kama kanuni zetu zina matatizo kwa sababu tunapita Kanuni nafikiri kesho tulione hili tunalirekebisha vipi.

Ukisoma hiyo "Hati za kuwasilishwa Mezani" halafu ukenda katika kanuni ya 33(1) inasema "Wakati wowote baada ya hati yoyote kuwasilishwa kwa mujibu wa kanuni 32.

(1) Waziri au mjumbe aliyewasilisha hati hiyo au mjumbe mwengine yeyote anaweza kuomba kutoa hoja kwamba Baraza lijadili hati hiyo,

(2) Mjadala unaweza kugusia kila jambo liliomo katika hati.

(3) Waziri au mjumbe yeyote ambaye anaruhusika kulihutubia Baraza kwa mujibu wa kanuni hizi ikiwa hakuiwasilisha hati yake kabla basi Spika, atamzuia waziri au mjumbe huyo asisome hati yake hiyo.

Mhe. Spika, nilikua nataka utuwekee sawa kwamba ukiitizama Kanuni ya 27 hati ya kuwasilishwa mezani zimeandikwa kama ni kitu kinachojitegemea. Haidhuru ukiisoma tafsiri yake katika Kanuni ya 32, Kanuni ndogo ya 5 inasema "kwa mujibu wa Kanuni hii neno hati linajumuisha "Hati" rasmi zote zinazotakiwa na Katiba, sheria au kanuni hizi kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi ikiwa pamoja na maelezo yoyote ambayo yapo katika maandishi yanakusudiwa kuwasilishwa Barazani na Waziri au na mjumbe mwengine yoyote.

Sasa ukiisoma na 33 inasema "Hati zote hizi zinapaswa kujadiliwa ikiwa mjumbe katoa hoja kwamba zijadiliwe". Nilikua naomba Mhe. Spika, muongozo wako kwa hili ili kama kuna matatizo katika kanuni tutakapokaa kupitia na Kamati yetu inayohusika na marekebisho ya kanuni tulione hili ili tufafanue hasa "Hati za Kuwasilisha Mezani zipi na zinachukua tafsiri ipi na je, unaitafsiri vipi hasa ukiizingatia hiyo *Order paper* ya leo ilivyokua imekaa. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Unajua suala hili lina historia yake kidogo juu ya "Hati za Kuwasilishwa Mezani". Hapo kabla hati ambazo zilizokua zikiwasilishwa Mezani ni magazeti rasmi ya serikali ambayo yalikua yanachapishwa katika kipindi cha kutoka mkutano uliopita hadi mkutano huu hapa kati kati, ndio kwa mazoea yetu ilikua zinawasilishwa. Lakini tukafika pahala tukaona kwamba mbona kuna hati nyingi na hizi pale ambapo Waziri anawasilisha haya magazeti rasmi ambayo anasema nawasilisha nakala zote za gazeti kutoka, hua anaeendesha hapa ana tizama je, kuna mtu mwenye swali kutaka kuhoji juu ya hati hizi ndio maana ya ile kusita kidogo.

Bahati nzuri kumbukumbu yangu ni mara moja tu ambapo Mhe. Mkema wa jimbo la Koani ambalo jimbo hili sasa hivi limechukuliwa na Mhe. Mussa Ali Hassan, aliwahi kuuliza nataka kuziona hizo hati. Maana kulikua na wasi wasi kwamba wakati mwengine tunasema kama kwa mazoea, nawasilisha hati zote lakini kumbe mezani hazipo. Mhe. Mkema wakati ule akauliza nataka kuziona hizo hati. Kwa bahati kumbe lile faili lilikuwepo zimewekwa mle, kwa hivyo ikawa kumbe hati zimewasilishwa. Lakini ni kweli kabisa baadhi ya wakati ilikua inatokezea ni kama utaratibu tu wa mazoea kwamba bila shaka kuna magazeti lakini hatukuchukua juhudi ya kuzileta hati zile mezani za kuonesha kwamba kumbe serikali ilichapisha mambo haya katika gazeti rasmi la serikali.
Baadaye tukaona ni vizuri mambo yote ambayo ndio tafsiri hiyo imekuja ndani ya kanuni.

Mambo yale ambayo sasa tunataka yawasilishwe rasmi katika maandishi itolewe taarifa kama nawasilisha mezani, ndio yakaja haya maoni ya kamati mbali mbali. Niliposimama mwanzo nilisema *order paper* yetu hii inamakosa, imeacha utaratibu wa kumuomba mwenyekiti hapa na yeye awasilishe hati. Lakini kurekebisha jambo lile kwa kuakhirisha kikao tukatengeneza *order paper* mpya niliona hiyo itatuvurugia mpangilio mzuri wa shughuli zetu.

Pili nikasema kwamba ili kwa uendeshaji bora hebu tuimalize hoja ya Mheshimiwa ndipo sasa tuje na hizi kauli. Hii waliifanya hivi kwa sababu ilifuata hii inavyosema, kwa sababu “Kauli za Mawaziri” hua zinakuja mapema. Kwa uendeshaji bora nikasema hapana tumalize Mswada halafu twende. Hata wakati fulani ulipoleta hoja yako juu ya jambo hili, kanuni inasema kwamba jambo la dharura la aina ile basi itasitishwa shughuli nyengine. Lakini nikasema kwa mpangilio bora wa uendeshaji wa shughuli zetu kulikua na jambo lilikua limebakia kidogo tulimalize halafu tena tuende na lile.

Kimsingi hoja ya leo imeacha baadhi ya mambo ya hati ambazo zimesomwa hapa hazikuwasilishwa mapema pale asubuhi. Lakini kiutaratibu ilikua ziwasilishwe, kauli za mawaziri inahitaji hati ile au maelezo yale ya Kamati inayohusika itoe ili iwe imepata ruhusa rasmi vyenginevyo kama ulivyosema kwamba sasa ilikua asiitoe kwa sababu hakusema mapema kwamba atawasilisha ile hati. Niiruhusu kwa sababu ni utaratibu wa kawaida wa kanuni kwamba baada ya maelezo ya taarifa basi mwenyekiti atoe maelezo ya Kamati. Ambayo kwa bahati mbaya sana nayo yamekua yana matatizo.
Kwa hivyo nadhani kanuni yetu ipo vizuri hadi sasa, kama kutakua na jambo la kuweza kuliangalia ipo *role* ya kuweza kusema kwamba turekebishe nini. Lakini *order paper* ya leo ilikua kidogo imesahau baadhi ya mambo ndio nikasema kwamba ipo haja ya marekebisho pamoja na mpangilio mwema wa uendeshaji wa shughuli zetu, tukamaliza hoja ile halafu ndio yakaja masuala tuliyoyawasilisha pamoja taarifa ile.

Kimsingi hapa sina jambo jegine zaidi kwamba hii *order paper* iliacha baadhi ya mambo yawasilishwe kama hati pale mwanzoni kabla ya kuja kusomwa moja kwa moja na mwenyekiti, labda niseme hivyo. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba nitoe ufafanuzi kidogo. Kwa kua Baraza lako tukufu linaendesha shughuli zake kwa kufuata kanuni. Serikali inaleta ima taarifa ima hoja katika Baraza lako tukufu kwa kufuata kanuni zetu tulizojiewekea katika Baraza hili. Kwa mujibu wa *order paper* ya leo tuliweza serikali kuleta taarifa kupitia kauli za mawaziri kutokana na ile kanuni uliyoieleza ya 43(1). Vile vile tumeweza kuleta hoja ya serikali kutokana na kanuni ya 27(10) (k) ili tuweze kujadili ripoti ya Baraza la Manispaa ya Mji wa Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda niseme kwamba serikali haikua na nia ya kufunika funika wala haikua na nia yoyote nyengine zaidi ya kusikiliza maelekezo ya Baraza lako tukufu. Napenda kutoa ufafanuzi huo Mhe. Spika. Ahsante sana.

TAARIFA YA MIKOPO YA BODI YA ELIMU YA JUU.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu taarifa juu ya hatua mbali mbali iliyochukuliwa na Wizara yangu kufatia hoja binafsi ya Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura iliyowasilishwa katika Baraza lako tukufu siku ya tarehe 26 mwezi wa Oktoba mwaka 2011, kuhusu upatikanaji wa fedha za kutosha kwa ajili ya kuengeza uwezo wa bodi ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaopata nafasi za kujiunga na taasisi za elimu ya juu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2011 bodi ya Mikopo Zanzibar ilipata maombi 1,850 kutoka kwa vijana mbali mbali kwa ajili ya kujiunga na taasisi za elimu ya juu. Maombi hayo yalihitaji jumla shilingi bilioni 15 kuwawezesha kugharamia vijana wote katika vyuo vya nje na ndani.

Maombi 250 yalikua ni kwa ajili ya vyuo 22 vya nje ya nchi na maombi 1,596 ni kwa ajili ya vyuo 41 vya ndani ya nchi.

Kuhusu Bajet
Mhe. Spika, bajeti iliyoidhinishiwa kwa mikopo hiyo ilikua ni shilingi bilioni 4. Lakini mahitaji halisi kwa wanafunzi waliokuwepo vyuoni kabla ya kupeleka vijana wetu yalikua ni bilioni 4.8. Bodi ilifanya uteuzi wa wanafunzi wapya 209 kwa mwaka wa 2011, 2012. Wanafunzi hao wapya walihitaji shilingi milioni 411 na kwa hivyo kufanya gharama zifikie shilingi bilioni 5.2.

Kwa ujumla upungufu wa bajeti kwa mwaka 2011/2012 ilikua shilingi bilioni 1.2 hadi hivi sasa bodi ya mikopo ya elimu ya juu imeshaingiziwa jumla ya shilingi bilioni 3. maombi yalikua shilingi bilioni 4, kwa hivyo kilichoingizwa ni sawa na asilimia 75 ya maombi yote ya bajeti hiyo. Hata kama fedha zilizobakia zitaingizwa serikalini na kuifanya bajeti ya mikopo ni asilimia 100 bado kutakua na upungufu wa fedha za bajeti ya mikopo. Upungufu wa shilingi bilioni 1.2 ndio utakaolazimika kupelekwa katika bajeti ya mwakani. Wanafunzi 1,641 hawakuweza kupatiwa mikopo kwa masomo ya elimu ya juu kutokana na upungufu wa bajet.

Hatua zilizochukuliwa
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inafahamu tatizo hili kubwa la kitaifa la kukosa mikopo ya wanafunzi mbali mbali kwa kuwapeleka au kwa kuwahudumia kwa masomo yao ya juu. Serikali imechukua hatua zifuatazo:

1) Serikali inajaribu kukusanya madeni ya wanafunzi ambao wamemaliza masomo yao, wamepasi, wamepata ajira na hawajalipa hata senti moja. Waliokopa walikua 1,280 ambao hao ndio waliomaliza masomo na wamepata ajira, kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka 2011. Katika juhudi hizi sasa tumeweza kuwapata wanafunzi 200 ambao tunajua wanapofanyakazi, mishahara wanayolipwa na wamemaliza masomo. Utaratibu huu tumeuanzisha hivi karibuni na unaanza kuleta tija. Kwa sababu tumewaandikia waliowaajiri na serikali au *private segment* au zote mbili kwa pamoja walipe au wawakate waajiriwa wao asilimia 10 kukidhi haja ya mkopo waliochukua.

   Hatua hiyo imeanza kuchukuliwa tokea mwezi wa Februari mwaka 2012 hadi hivi sasa jumla ya shilingi milioni 4 tumeshazikusanya. Zoezi hilo bado linaendelea na tunao wanafunzi kama 300 ambao idara zao zinatafutwa kwa kutumia vitambulisho na hawa baadaye watalazimika kulipa fedha zao.

2) Makisio ya bajeti kwa mwaka 2012/2013 zaidi ya njia hii tuliyoizungumza mwanzo njia yetu ya pili au jitihada yetu ya pili ni kuomba ongezeko la bajeti kwa asilimia 50 ili tuweze kukidhi ongezeko la vijana wetu wanaohitaji mikopo kwa ajili ya masomo yao ya juu.

3) Serikali au Wizara inatafuta marafiki, washiriki ili watusaidie kutupatia *scholarship*. Tumeanza kuwasiliana na benki ya kiislamu (*IDB*) na wamekubali kuongeza nafasi za ufadhili wa elimu. Benki hii imekubali kuanza kusomesha wanafunzi wetu katika vyuo vya ndani badala ya vyuo vya nje. Pia serikali inafanya mazungumzo na nchi nyengine rafiki kama vile Misri, China, Oman na Qatar, ili wao waweze kutusaidia kutupa msaada wa *scholarship* ili tuweze kuwapeleka wanafunzi wetu masomoni.

   Jengine tumezungumza kwa pamoja Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuhakikisha kwamba mtu hachukui mikopo miwili ya huku na huku. Hiyo itasaidia kumjua aliyekopa kakopa kwa Zanzibar au kakopa kwa Tanzania Bara na kwa hivyo itakua ni rahisi kumfatilia kupata fedha zetu.

4) Ni mazungumzo na *ZSSF* watusaidie kutupatia mikopo ya kuwasaidia wanafunzi wetu. Mazungumzo hayo yalizaa matunda na *ZSSF* wakakubali kusomesha wanafunzi ndani ya nchi na sio nje ya nchi. Kwa hivyo mikopo ambayo wanafunzi wetu wataipata kutoka *ZSSF* ni ya kusomesha ndani ya nchi na sio nje ya nchi. Lakini kwa bahati mbaya ingawa mazungumzo bado tunaendelea lakini *ZSSF* watadai fedha zao pamoja na riba. Huenda tukafanikiwa tukaifuta riba baadaye.

Mhe. Spika, maombi ya mikopo kwa mwaka 2012/2013 Bodi imeshafanya mazungumzo ya kutafuta mikopo ya kipindi hichi cha mwaka 2012/2013. Bodi imeshazungumza na skuli 26 za *Secondry* ya juu yaani *form five* mpaka *form six* kuhusu utaratibu wa mikopo utakaotumika, fedha zitakazopatikana na pengine kuandika mikataba kwa wale watakaopata fedha ili kuhakikisha baada ya kumaliza skuli au masomo hatimaye kupata kazi waanze kukatwa asilimia 10 kama Kanuni inavyozungumza.

Bodi imeshafanya mazungumzo na kupokea maombi ya wanafunzi mbali mbali hivi sasa, kati ya maandalizi hayo bodi ilitembelea skuli 26 za Skuli za Sekondari ya kutoa taaluma mbali mbali kuhusu namna ya ukopeshaji utakavyotumika.

Halikadhalika imetoa taaluma ya wanafunzi hao kuhusiana na namna ya vipau mbele vitakavyotumika kwa wale watakaochukua fani mbali mbali. Mkazo utawekwa kwa wanafunzi watakaochukua fani zifuatazo. Kwa mfano walimu wa sayansi, fani mbali mbali za udaktari na ufamasia, *business administration, hotel management, tourism management, tourism relation, mining, developing planning, environmental studies* na kadhalika. Utaratibu huu utakua ukibadilika mara kwa mara au mwaka hadi mwaka kutokana na hali ya madadiliko ya soko letu.

(a) Tayari serikali kupitia Wizara husika inaendelea na utafiti wa mahitaji ya wataalamu na baadaye kutayarisha mpango madhubuti wa kuwa-*identify* hao wataalamu Vis-*à-vis* masoko ya ulimwengu yanavyokwenda.

(b) Kupeleka wanafunzi kulingana na uwezo wetu. Kwa sababu tunachelea kupeleka wanafunzi wengi, uwezo wetu mdogo, hatimaye wanafunzi wetu wanapata matatizo ya kuzuiliwa masomo yao. Kwa hivyo tutakua makini sana katika uteuzi na kuwapeleka wanafunzi kwa kuwapa mikopo kutokana na uwezo wetu. Uwezo wetu katika mwaka ujao kama tukifanikiwa kuipata nyongeza yetu tunayoiomba hali itakua nzuri.

(c) Kuzuia kwa muda kupeleka wanafunzi nchi za nje ambao skuli hizo zinahitaji malipo makubwa. Tutatumia zaidi skuli zetu za ndani ili kupunguza matumizi ya kusomesha watoto wetu.

(d) Mkazo zaidi utawekwa kwa wale wanafunzi wa shahada ya mwanzo na hatimaye tutazingatia wale wengine wa shahada ya Pili na Shahada ya Tatu.

Mhe. Spika, kazi ya kuwapatia wanafunzi mahitaji yao ya masomo ni kubwa. Idadi za wanafunzi zinaongezeka kila uchao na hii ni manufaa na faida kwa nchi yetu. Lakini hali yetu ya kiunchumi inalingana sana na wenzetu majirani ambao utaratibu huu wameshaufuta. Zanzibar haikusudii kuufuta utaratibu huu, tutaendelea nao, tutatafuta wahisani mbali mbali watusaidie. Lakini pia tunatoa wito kwa wenzetu wa nchini nao vile vile wasaidie kuwekeza katika elimu ya juu kwa watoto wao kwa wale wanaojiweza ili na sisi tupate nafasi ya kuwashughulikia wale ambao ni masikini.

Mhe. Spika, naomba wasilisha.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri tunakushukuru kwa taarifa hiyo, muda umekwisha taarifa ya kamati itatolewa jioni. Waheshimiwa wajumbe kuna matangazo matatu.

1) Tunachukua nafasi hii kuwashukuru madaktari waliokuja kutusaidia kupima afya na wametuomba kama kuna wajumbe wowote ambao hawajapima afya basi wafanye hivyo. Lakini inavyoonekana kwa muda huu pengine hata ule utaratibu wa watu waliojizuia kula utakua umeshavurugika. Kama wapo waheshimiwa wajumbe ambao bado hawajapima afya tutawaomba tu madaktari labda warudie tena kesho kwa utaratibu ule ule kwamba ikifika kwenye saa 6:00 za usiku tujuzuie kula chakula na kunywa maji. Nimeletewa taarifa nyengine sasa kwa wale wajumbe ambao hawajapima afya kesho kumbe madaktari wana ratiba nyengine. Kama bado hawajafungua wakapime leo wapo bado pale wanasubiri kwa wale ambao hawajapima afya.

2) Nimeombwa nitoe taarifa kwa Kamati ya Habari, Mifugo na Uwezeshaji kwamba mara baada ya kuakhirisha shughuli zetu basi wajumbe wa Kamati hiyo wakutane kwenye chumba Nam. 3 cha Kamati kuna mambo wayazungumze huko.

3) Waheshimiwa Wajumbe wafuatao wanaombwa waende katika Ofisi ya Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kuchukua mambo fulani kwa ajili ya jimbo. Wajumbe wenyewe ni kama hawa wafuatao:

    1) Mhe. Issa Haji Ussi.

    2) Mhe. Abubakar Khamis Bakary

    3) Mhe. Haji Faki Shaali

    4) Mhe. Thuwaibah Eddington Kisasi

5) Mhe. Makame Mshimba Mbarouk

6) Mhe. Nassor Salim Ali

7) Mhe. Rufai Said Rufai

8) Mhe. Abdalla Juma Abdalla

9) Mhe. Said Ali Mbarouk

10) Mhe. Salim Abdalla Hamad

11) Mhe. Haji Omar Kheir

12) Mhe. Ali Abdalla Ali

13) Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa

Wengine waendelee kufanya subra kwa siku za usoni. Waende chumba cha Ofisi ya Katibu wa Baraza wataonana na Maofisa kutoka Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Baada ya hayo naakhirisha kikao hichi hadi saa 11: jioni leo.

(Saa 7:00 Mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wanawake na Ustawi wa Jamii: Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na afya leo hii na kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu ili kutoa maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mikopo ya Bodi ya Elimu ya Juu.

Mhe. Spika, aidha ningependa uwatambue wajumbe wa kamati husika kabla ya kuwasilisha maoni ambao wajumbe wenyewe ni:-

1.	Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Mwenyekiti
2.	Mhe. Hija Hassan Hija	-	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Asha Abdu Haji	-	Mjumbe
4.	Mhe. Ashura Sharif Ali	-	Mjumbe
5.	Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Mjumbe
6.	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Mjumbe
7.	Mhe. Nassor Salim Ali	-	Mjumbe
8.	Mhe. Saleh Nassor Juma	-	Mjumbe
9.	Ndg. Talib Enzi Talib	-	Katibu
10.	Ndg. Asha Said Mohammed	-	Katibu

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 43 (2) ya kanuni za Baraza la Wawakilishi, kamati yetu imepewa nafasi ya kutoa maoni juu ya taarifa ya serikali kuhusu hatua mbali mbali zilizochukuliwa kufuatia hoja binafsi iliyowasilishwa katika Baraza la Wawakilishi tarehe 26 Oktoba, 2011 na Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura (Mhe. Hamza Hassan Juma), kuhusu kupatikana fedha za kutosha ili kuongeza uwezo wa bodi wa kutoa mikopo kwa wanafunzi wanaopata nafasi ya kujiunga na taasisi za elimu ya juu. Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inaikumbusha serikali kwamba kuendelea kuwa na bajeti ndogo kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kutaathiri maendeleo ya baadae ya elimu hiyo nchini. Kwa hivyo, kuna haja kwa serikali kujipanga katika kuweka bajeti itakayolingana na mahitaji iliyopo ili kukabiliana na ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaofaulu na kuhitaji mikopo ya elimu ya juu mwaka hadi mwaka.

Aidha, kamati imeona kuwa kiwango cha wanafunzi waliopatiwa udhamini wa mikopo kwa ajili ya masomo nje ya nchi bado ni kikubwa na huhitaji gharama kubwa. Kamati yetu inaipongeza serikali katika maandalizi

yakupokea maombi mapya ya mikopo kwa mwaka 2012-2013, kuzuia kwa muda na kupeleka wanafunzi kwa masomo katika vyuo vya nje.

Mhe. Spika, kamati yetu inatahadharisha serikali kuwa huko nyuma hakukuwa na umakini wakati wa utoaji wa mikopo husika, hali ambayo imepelekea hivi sasa kuwepo kwa usumbufu wa kuwatafuta wahitimu waliokopeshwa na kuajiriwa ili waanze kulipa madeni yao. Wizara kupitia Bodi yake ya Mikopo lazima ihakikishe kuwa suala la kuwatambua wakopaji ni la mwanzo ili kuondosha usumbufu kama huo.

Mhe. Spika, tumeelezwa kuwa kuna taarifa za wahitimu 300 zilizowasilishwa katika Idara ya Vitambulisho vya Ukaazi Zanzibar, na Wizara ya Utumishi ili kuweza kuwatambua sehemu wanazofanyia kazi. Hili linatia shaka kwamba je, walipewa mikopo hiyo kweli ni Wazanzibari? Kama ni hivyo iweje taarifa zao zipelekwe kwa ajili ya kutafutwa katika idara hiyo. Mhe. Spika, hilo ni tatizo.

Mhe. Spika, Kamati ya Wanawake na Ustawi wa Jamii inapongeza wizara kwa hatua ya kuendelea kutafuta wahisani wakusaidia kutupatia nafasi za masomo na kuongeza nafasi za ufadhili zaidi wa elimu katika vyuo vyetu vya ndani badala ya kuwapeleka vijana nje ya nchi.

Mhe. Spika, kuhusu suala la mgao wa fungu la fedha za elimu ya juu kwa Zanzibar kamati yetu inaona halihitaji tena mazungumzo marefu ambayo hupelekea kuendelea kuwepo kwa urasimu ni suala la utekelezaji, ili Zanzibar nayo iweze kuondokana na tatizo la uhaba wa kibajeti katika upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu.

Mhe. Spika, kamati inaipongeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuanzisha utaratibu mzuri wa maombi ya mikopo kwa mwaka 2012-2013. Utaratibu huo ni pamoja na kuwaelimisha vijana wetu juu ya vipaumbele mbali mbali vilivyoweka katika utoaji wa mikopo hiyo. Hatua hiyo itawezesha vijana wetu kuelewa mapema sifa za msingi zinazotakiwa kwa waombaji wa mikopo hiyo. Hata hivyo, hizo ziende sambamba na kulipa kwa madeni yaliyopo vyuoni ili kuwapa utulivu wanafunzi wetu.

Mhe. Spika, mwisho kamati inapendekeza licha ya kuwepo kwa matarajio ya kuongezeka kwa makisio ya fedha za bajeti kwa mwaka 2012-2013 kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa zaidi ya asilimia 50. Kuna haja ya kuwepo kwa utaratibu maalum wa mapitio ya kibajeti ya kila mwaka ya mikopo hiyo ili kwenda sambamba na mahitaji yaliyopo ya bajeti ya mikopo ya elimu ya juu. Mhe. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ahsante sana naomba kwanza nichukue fursa hii kuipongeza na kuishukuru serikali kwa taarifa hii iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, naomba pia nichukue fursa hii kumpongeza yeye Mhe. Ali Juma Shamuhuna kwa uteuzi alioupata kwa kuiongoza wizara hii. Lakini ili nisiendelee kuja kuonekana navunja kanuni yake niende moja kwa moja kwenye maswali.

Mhe. Spika, naomba kutoka kwa Mhe. Waziri anipatie ufafanuzi kuhusu maswali haya machache.

Mhe. Spika, la kwanza katika ukurasa wa pili wa taarifa hii kumezungumzwa kumekuwa kukichukuliwa hatua za kukusanya madeni kutoka kwa wanafunzi au wahitimu ambao walishapewa mikopo huko nyuma ambao jumla yao ni 1280 waliomaliza masomo kati ya 2006-2011. Kwa hivyo, wamesema hatua hiyo imeanza kuchukuliwa katika mwezi wa Februari, 2012 na hadi hivi sasa zimepatikana shilingi 4,000,000/=. Mhe. Spika, nilikuwa naomba kujua jumla zinazodaiwa ni kiasi gani na anategemea ndani ya muda gani wanaweza kuzikamilisha kuzikusanya, hilo la kwanza Mhe. Spika.

Mhe. Spika, suala langu la pili linakuja katika maelezo ambayo yako katika ukurasa wa pili mwishoni yanaendelea mpaka ukurasa wa tatu kuhusu jitihada za serikali kuomba nafasi kutoka katika nchi marafiki kwa ajili ya kupata *scholarship.* Juzi tu Mhe. Spika, katika kujibu baadhi yaliyotokea katika Baraza lako Naibu Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Abdalla Juma alisema kwamba Zanzibar imepatiwa nafasi 10 za kupeleka wanafunzi katika Chuo cha Utalii Mombasa ambazo zilikuwa zimetolewa kama *scholarship,* lakini Serikali ya Zanzibar imeshindwa hadi leo kuzitumia nafasi hizo kwa kuwapeleka wanafunzi. Mhe. Spika, katika moja ya maeneo ambayo yametajwa katika vipaumbele vya kozi zilizotajwa, moja ni kozi zinazohusiana na utalii, sijui kwa nini Serikali ya Zanzibar mpaka leo haijazitumia nafasi hizi 10. Nilikuwa naomba ufafanuzi.

Mhe. Spika, la tatu hapo hapo ukurasa wa 3 pametajwa kwamba kuna mazungumzo yanaendelea kati ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Zanzibar na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Jamhuri ya Muungano juu ya mgao wa fedha za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Zanzibar. Mhe. Spika, taarifa

tulizonazo ni kwamba bajeti iliyotengwa kwa Bodi ya Mikopo ya Elimu kwa upande wa Jamhuri ya Muungano kwa jumla ni shilingi bilioni 317. Kwa hivyo, nilikuwa najiuliza kwa nini Serikali ya Zanzibar katika kuepusha hata ile ambayo imetajwa katika ripoti hii kwamba kuna watu wanaomba sehemu zote mbili isitake tu ipewe mgao wake kutokana katika bodi hii ambao mgao huo uingie katika Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar na badala yake wanafunzi wa Zanzibar wote waombe kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nimefanya hesabu ya haraka haraka kwamba ikiwa tutapewa hata ile asilimia 4.5 ambayo mara nyingi wenzetu wanaipenda kuitumia ya mgao, basi katika bilioni 317 Zanzibar itapata bilioni 14.15 ambayo itakuwa imemaliza kabisa yale mahitaji ya Zanzibar aliyoyataja Mhe. Waziri katika ripoti hii. Kwa hivyo, kwa nini waziri asichukue pendekezo hili la kuitaka Serikali ya Muungano katika mgao ule itupe asilimie 4.5 ili wanafunzi wa Zanzibar wote waombe kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, jengine ambalo ni la mwisho linatokana na maelezo yaliyokuwepo katika ukurasa wa 4. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 4 pametajwa orodha ya fani ambazo zinapewa kipaumbele kwa mwaka 2012-2013. Halafu baada ya pale kuna maelezo yamesema kwamba tayari serikali kupitia wizara husika inaendelea na utafiti wa mahitaji ya wataalamu na baadae kutayarisha mpango wa mafunzo ya kitaifa *National Training Program.* Mhe. Spika, nilitaka nisaidiwe jibu la swali langu kwamba je, juzi tu hapa tumepitisha sheria ya kuunda upya tume ya mipango, na moja katika kazi yake ni kuweka vipaumbele vya taifa katika masuala mazima ya mpango wa kiuchumi. Mhe. Spika, ni kiasi gani mpango huu wa *National Training Program* utakuwa umezingatia kufanya uratibu katika serikali kwa ujumla wake ili yale yaliyoamuliwa kwamba ndio mambo yanayohitaji kupewa kipaumbele yawe yametokana na mpango huo.

Mhe. Spika, nauliza hilo kwa sababu katika orodha niliyokuwa nimeiona hapa nimeona mambo mengi, lakini liko iko hii fani ya uchimbaji wa maadini, lakini sikuona chochote katika vipengele hivi fani inayohusika na mafuta na gesi ambayo Zanzibar tunategemea huko mbele tutahitaji wataalamu wengi katika hilo na pia katika masula ya *geology*. Kwa hivyo, nilikuwa naomba Mhe. Spika, suala hilo Mhe. Waziri anisaidie kwa nini katika orodha hii hatuna fani ya *oil, gas* na *geology* kwa jumla. Vile vile atahakikishaje kwamba mahitaji yetu haya yatakuwa yamezingatia vile vipaumbele vya taifa kama vilivyo katika Tume ya Mipango. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikapata ufafanuzi wa masuala mawili matatu kwa Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Spika, kabla ya kuanza kuuliza masuala yangu kwanza nataka nitoe pongezi na shukurani zangu za dhati kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwanza kwa kuipokea ile hoja yangu, lakini vile vile serikali kwa kutekeleza ile ahadi yake walivyosema kwamba watakwenda watakao wataiangalia na wataifanyia kazi. Mhe. Spika, kwa kweli naishukuru sana serikali na kama tutaendelea na moyo huo huo basi naamini mambo mengi ambayo tunayazungumza hapa Barazani serikali ikiyafanyia kazi tutaweza kupata ufumbuzi wa kudumu kwa matatizo yetu hasa kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo sasa nataka nije moja kwa moja katika *paper* hii ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali. Mhe. Spika, katika ripoti hii ya Mhe. Waziri ameelezea kwamba katika wakopaji 1280 ambao waliomaliza mwaka 2006-2011 kwa hivi sasa ni wanafunzi 200 tu ndio waliotambuliwa katika hao waliopewa mikopo hiyo. Mhe. Spika, suala langu liko hapa, je, katika hao wanafunzi 1280 waliopewa mikop na mpaka hivi sasa waliogunduliwa 200. Je, hawa wanafunzi 1080 wako wapi?

Mhe. Spika, kwa kuwa Zanzibar tuko kidogo na tuko wachache sana, bila shaka mikopo hii ilivyokuwa inatoka kulikuwa kuna utaratibu maalum uliokuwa umewekwa. Je, Mhe. Spika, huoni kwamba wizara leo inatwambia katika wanafunzi 1280 ambao wametambuliwa mpaka sasa hivi ni 200 tu. Je, hatuoni kwamba hawa wanafunzi wengine kwa lugha ya kisasa ni wanafunzi hewa.

Mhe. Spika, je, kama wizara haijatuthibitishia wanafunzi hawa sio hewa, je, wako tayari kuikabidhi kamati aidha ya PAC au kamati inayoshughulikia wizara hii kwenda kuchunguza fedha hizi namna zilivyokwenda. Mhe. Spika, inavyokuwa utaratibu wa fedha za serikali ambao ni fedha za umma karibu bilioni 8 zilizotoka tumeambiwa fedha zilizorudishwa ni milioni 4. Je, Mhe. Spika, hatuoni kwamba fedha za umma zinapotea bila ya utaratibu na serikali haijui fedha hizi zilikopita.

Mhe. Spika, katika wanafunzi hawa ambao waliopewa mikopo nadhani kuna sababu ambayo iliyosababisha wanafunzi hawa mpaka leo hawajuulikani, lakini kwa kawaida mimi najua wanafunzi hawa wanajuulikana. Mhe. Spika, suala langu jengine liko hapa ni kwamba tuna taarifa ambazo ndio maana nikasema kamati ipewe kazi ikachunguze kwamba miongoni mwa wanafuzi hawa waliopewa mikopo wengi wao walikuwa hawana hizo

sifa. Mhe. Spika, je, kama tunasema wanafunzi hawa 1080 hatuwajui walipo, je, hatuwajui wanafunzi wetu waliomba nafasi za masomo nje ya nchi kuanzia mwaka 2006-2011. Mhe. Spika, baada ya masuala yangu haya naamini Mhe. Waziri ataweza kuja na jawabu ambayo itakayoweza kunitosheleza, lakini kama mimi ndiye niliyekuwa mtoa hoja kama nitakuwa sijatoshelezwa na jawabu hizi basi nitakuomba uniruhusu Mhe. Spika, Kamati yako ya Baraza ikamsaidie Mhe. Waziri kuzitafuta fedha hizi zilikopotea, lakini na hao wanafunzi ambao wizara haiwajui nakuaminisha Mhe. Spika, Baraza lako tuko watu makini tutakuletea fedha hizi zilizopotoa na hao wanafunzi hewa ambao tuna wasi wasi waliopatiwa hizi fedha tutakuletea orodha yake, kwa kumsaidia Mhe. Waziri. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kumuuliza Mhe. Waziri baadhi ya maswali. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri na serikali kwa ujumla kuweza ku-*respond* hoja za wajumbe na kuweza kutoa taarifa inapohitajika.

Mhe. Spika, suala langu la mwanzo liko kwenye ukurasa wa 1, Mhe. Waziri ametaja hapa idadi ya wanafunzi na vyuo walivyoomba idadi yake vikiwa vya ndani na vya nje. Mimi suala langu ni je, kuna sera yoyote inayoongoza nchi kuhusiana na maombi ya wanafunzi kwenda kusoma nje? Kwa sababu Mhe. Spika, nchi nyingi zinatumia hasa nchi ambazo fedha zake ni kidogo kwamba *degree* ya mwanzo ilivyokuwa inapatikana ndani ya nchi hawatoi nafasi kwa wanafunzi kwenda nje ya nchi kufanya *degree* ya mwanzo. Lakini *paper* hii haielezi sera ya wanafunzi gani wanaopewa nafasi kwenda kusoma nje. Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri katika kutoa hii mikopo ambayo wanaokwenda kusoma nje wanachukua sehemu kubwa ya mikopo kuna sera yoyote inayoongoza kwamba mwenye kusoma *degree* ya kwanza au ya pili ndio mwenye fursa ya kusoma nje au mpaka *degree* ya pili ndio aweze kwenda kusoma nje. Hilo suala la kwanza.

Mhe. Spika, la pili mimi kidogo niko nje ya takwimu kwa hivyo naomba nimuulize Mhe. Waziri ikiwa hapa vilivyotajwa vyuo ni 41 ndani ya nchi. Je, mikopo hii inatolewa chini ya *degree* moja wanatoa mikopo kwa wanaosoma diploma kwa sababu sina hakika kama Tanzania tunatimiza vyuo vikuu 41 na mikopo hii inatarajiwa iweze kutolewa kwa elimu ya juu, lakini vilivyotajwa hapa ni 41 hizi ni vyuo vikuu au ni vyuo vyengine vidogo vidogo kwa hivyo mikopo inatolewa kwa wale wanaosoma diploma.

Mhe. Spika, suala langu la 3 liko utaratibu wa mikopo, hoja iliyotolewa na Mhe. Hamza ilikuwa inataja utaratibu wa kutolewa mikopo. Lakini *paper* hii haikusema marekebisho yoyote yatakayofanywa katika kutoa mikopo katika kipindi kijacho. Je, Mhe. Waziri kuna maandalizi yoyote ya mabadiliko ya utoaji mikopo hususan wakati wa kupokea maombi na wakati wa majibu. Kwani Mhe. Spika, wale wanaopeleka maombi hawapewi jibu la moja kwa moja kwa vile wameomba mwanzo, wanaekwa sana na matokeo yake wanaingia tamaa na baadae wanapewa majibu kwa umoja.

Mhe. Spika, wenzetu wanatumia *short listing* ikifika tu unajua kwamba wewe hu-*qualify* unaambiwa pale pale, lakini utaalamu huo haujatumika. Je, wizara imejipanga kutumia utaalamu huo ili wale ambao hawakustahiki tokea mwanzo wakapata jibu mapema mno kuliko kungojea mpaka wakaingia tamaa halafu wakaja wakapewa majibu pengine baada ya miezi mitatu kwamba hawakufanikiwa.

Mhe. Spika, suala la mwisho liko kwenye *list* ya hizi fani ambazo zimepewa kipaumbele. Kidogo nina masikitiko na namuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa tumezungukwa na bahari, kwa kuwa nchi yetu inahitaji kuwa na mafundi wengi hakuna fani ya *marine* ya aina yoyote iliyotajwa hapa wala ufundi uliotajwa hapa. Je, hizi si fani ambazo zinazopewa kipaumbele hapa ni kwa nini hazikutajwa katika *list*? Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipa nafasi niulize kidogo katika hoja hii. Mimi nina maswali mawili la kwanza katika ukurasa wa 3 imeelezwa hapa kwamba Benki ya ADB imekubali kufadhili wanafunzi humu nchini. Mimi nilikuwa nataka kujua tu je, ni wanafunzi wa fani gani ambao wamekubaliana nao, na kiasi gani cha wanafuzi ambao watafaidika na mkopo huo kwa mwaka ujao?

Mhe. Spika, jengine katika ukurasa huu huu wa 3 kuna maelezo hapa ya Mhe. Waziri yanasema kuna kikao ambacho kitafanyika baina ya mawaziri wa pande hizi mbili kujadiliana kuhusu masuala ya bodi ya mikopo kinatarajiwa kufanyika hapa Zanzibar tarehe 4 na tarehe 5 April nilikuwa nataka kujua kwamba kile kikao kimefanyika na kama kimefanyika kuna makubaliano yepi baina ya pande hizi mbili. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa na mimi niulize maswali yangu. Mhe. Spika, ninavyoelewa mimi elimu ya juu ni sehemu au ni suala la Muungano kwa maana hiyo napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa sababu suala hili ni suala la Muungano. Je, kuna uwiano gani unaotumika kwa ajili ya kupata uwiano baina ya wanafunzi kutoka Zanzibar na wale wa Tanzania Bara. Kwa sababu kama hakuna

uwiano wa aina yoyote je, serikali imejipanga vipi kujua kama wanafunzi kutoka Zanzibar wanapata kiwango fulani na wanafunzi kutoka Bara wanapata kiwango fulani.

Mhe. Spika, suala la pili napenda kumuuliza Mhe. Waziri kama maana ya kuwekwa bodi ya mikopo ni kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wale ambao hawana uwezo ili waweze kujifaidia na kusoma na kujiendeleza, nafikiri sana kama hiyo ndio adhma ya serikali kuwasaidia wananchi awke. Napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwa kuwa mikopo inapotolewa wananchi huomba wanafunzi na wakishaomba wakawa wanaingia tamaa kama wavyozungumza wenzangu, lakini inakuwa na ucheleweshaji mkubwa wa kupata majibu mtu akajua kama mimi nimebahatika au sikubahatika. Je, kwa sababu kipindi kilichopita kuna baadhi ya wanafunzi waliomba mikopo na wakatoa fedha zao mkononi kwa ajili ya kujisajili kwa kujiendeleza na masomo, lakini mwisho wake mikopo ile hawakuipata.

Je, Mhe. Waziri kutokana ma matatizo yaliyojitokeza kipindi hicho je, kwa kipindi hiki Mhe. Waziri umejiandaa vipi ili wanafunzi wapate kujua mapema kama mimi nimepata mkopo au sikupata mkopo?

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi kidogo yakuweza kuuliza swali moja. Katika *paper* hii ya Mhe. Waziri imezungumza kwamba serikali inafanya mazungmzo na nchi nyengine rafiki kama vile Misri, China, Oman na Qatar na dhamira ya kufanya hivyo nikuwapatia nafasi za masomo bila ya malipo ili wanafunzi wengi zaidi waweze kupatiwa nafasi za masomo ya elimu ya juu.

Mhe. Spika, napenda nimuulize Mhe. Waziri katika mazungumzo hayo baina ya Serikali ya Zanzibar na hao marafiki mazungumzo haya wameyakubali? Na kama wameyakubali je, ni mwaka gani ambayo nafasi hii ya nchi za nje tutaipata kama mwaka huu au mwaka ujao au miaka ijayo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, ahsante kwa ruhusa yako na mimi naomba niulize swali moja. Mhe. Spika, nilipokuwa naupitia waraka huu nimesikitishwa kwamba Wizara ya Elimu haikuwa imepanga mpango madhubuti wa kuhakikisha kama ile mikopo inayotolewa hatimae inarudi na kuwafaa vijana wetu wengine. Na kadri nilivyosoma mikakati ya sasa hivi pia sikuona suala hilo, nimeona namna ya kutafuta fedha zaidi kwa ajili ya kuwafanya vijana waendelee kusoma.

Je, Mhe. Waziri amejipanga vipi ili kuonekana kama pesa zinazopatolewa kwa mikopo zinarudi baadae kwenye bodi halafu zikawasaidia wanafunzi wengine ili ziwe endelevu kuliko kuzitoa zikapotea.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, naomba na mimi nimuulize Mhe. Waziri masuala yafuatayo. Mhe. Spika, katika ukurasa wa 2 Mhe. Waziri amesema kwamba wanafunzi 1280 ndio waliokopa na tayari wamemaliza masomo yao. Na hapo hapo amesema kwamba kuna wanafunzi zaidi ya 300 ameomba msaada wa vitambulisho vya Mzanzibari na Ofisi ya Utumishi wa Umma. Je, Mhe. Waziri anakusudia kuniambia kwamba tangu mwanzo hawajui aliowakopesha anajua *figure* tu. Lakini pili, haoni kwamba hao ambao wamepewa mkopo huu na leo anaomba msaada wa vitambulisho ama hawa si Wazanzibari au walipewa vitambulisho juu ya utaratibu wa serikali.

Mwisho tulipokwenda Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania, wenzetu walitwambia wazi kwamba mwaka huu unaomalizika walitengewa zaidi ya shilingi bilioni 300 kwa ajili ya elimu ya juu. Na tulipohoji kwa nini Zanzibar hatupati fursa hiyo ya kuwasomesha wanafunzi wetu kwa kiwango hicho ilionekana kwamba wizara yenyewe imeridhika na Bodi ya Mikopo iliyopo Zanzibar, na leo mnatwambia kwamba mnafanya mazungumzo. Hebu turidhishe vipi tujipange, tuamini vipi kwamba fedha hizi za elimu ya juu ya Tanzania ambayo ni haki yetu Wazanzibari wataipata.

Mhe. Spika: Nawashukuru Waheshimiwa Wajumbe, sijui sasa mmejipangaje.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kujibu maswali ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu waliyoyatoa kwa kuhoji taarifa ambayo niliitoa hivi leo mchana. Kwanza nawashukuru wajumbe wote waliotoa maswali haya muhimu sana, mengi, nataka niseme kwa mimi ni magumu kwa ugeni wangu, lakini nitajaribu kuyajibu kadiri nitakavyoweza na yale ambayo nitashindwa kuyajibu ama nitakuwa nakubaliana nayo au vyenginevyo Mhe. Spika, uniruhusu niombe msaada kwa waziri aliyenitangulia katika wizara hii. Naona umetikisa kichwa kwa hivyo umekubali, na waziri aliyenitangulia amekiri kwamba atasaidia, hivyo mimi kwanza naanza kujibu mwenyewe kitachonishinda nitampasia mwenzangu.

Mhe. Spika: Sijui wewe umalizie aanze yeye? Bora aanze yeye wewe umalizie.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kwanza kutoa majibu juu ya masuala haya. Lakini nasikitika kwamba niliyoyawahi mimi ni machache yameanza kwa Mhe. Rashid Seif kuendea chini, yale yaliyoko juu sikuyapata.Kwa hivyo, haya niliyoyapata nitajaribu kuyajibu.

Kwanza Mhe. Rashid Seif amezungumzia juu ya suala zima la kuchelewa kutolewa majibu kwa wanafunzi wanaoomba mkopo katika Bodi ya Elimu ya Juu. Mhe. Spika, nataka kumfahamisha Mhe. Rashid Seif ni kwamba, kupokea maombi ya mikopo yanaanza mwezi wa Machi na majibu yanatolewa kwenye Julai baada ya kupata mwelekeo wa bajeti, kwa hivyo hawachelewi kujibiwa, lakini ni utaratibu kuwa hawawezi kutoa majibu mpaka kwanza wapate muelekeo wa bajeti, halafu hapo tena ndio unatoa majibu kujua kwamba wataweza kuwahudumia wangapi.

Hivi sasa tayari watu wameshaanza kuomba utaratibu unaendelea kule wanakusanya maombi, lakini maombi hayo uhakikishe majibu yake watayapata Julai baada ya muelekeo wa hii bajeti na kawaida *semester* mara nyingi huwa zinaanza kwenye mwezi wa Septemba tunazotumia sisi hatutumii hizi za Febuari/Machi tunatumia za Septemba. Kwa hivyo, sio kwamba wanachelewa, ni kwamba utaratibu uko hivyo, lazima tupate mwelekeo wa bajeti baada ya kupitisha hapa kwenye Juni kuingia kwenye Julai. Hilo ni moja.

La pili kuna suala la fani ambazo anaweza akaziona kwamba hazikuwekwa katika hii orodha iliyotolewa. Kwa sababu katika utaratibu wetu mpya wa kutoa mikopo kinachotizamwa mahitaji gani kwa sasa hivi yanatakiwa na katika Bodi ya Mikopo tuna mtu kutoka Wizara ya Fedha, tuna mtu kutoka Tume ya Mipango, na tunao wengine wanaosaidia katika haya masuala, sasa hao wanajua kwamba mahitaji kwa kipindi hiki ni fani ipi na ipi na ipi.

Kwa hivyo, kwa mwaka huu ndio hizi fani ambazo zimeorodheshwa ambazo kutokana na bajeti yetu itakavyoturuhusu, hawa ndio wanaoweza kupewa mikopo na ndio maana katika hii taarifa ikaeleza kwamba Bodi imezitembelea skuli 26 ambazo watu wanamaliza kusoma *Form VI*, kuwaeleza kwamba safari hii mkitaka kuomba basi muombe kwenye fani hizi. Kwa hivyo unapofanya kazi na kusema wale wenye mitihani ujue kwamba wewe utabidi uje u- *qualify* kwa mwaka huu kwenye fani hizi ndio maana tukaona baadhi ya fani mle hazimo.Zote ni muhimu lakini kwa mwaka huu zitachukuliwa zipi na kwa mwaka ujao zitachukuliwa zipi, huo ndio utaratibu ambao unaendelea.

Halafu kuna suala la benki *IDB*, *Islamic Development Bank* inasaidia zamani tu kuwachukua wanafunzi kuwapeleka kusoma nje katika fani tunayoitaka sisi hapa nchini, sisi tunataka watu wa fani gani, sasa wao wakishajua sisi tunataka fani gani, wanachotaka ni sifa zao tu, sifa hizo zikipatikana wale wanafunzi wanachukuliwa na *IDB*. Lakini tulipozungumza nao kwa mara ya mwisho kwamba, kuna wanafunzi wengi wana-*qualify* na wanahitaji kupata hii elimu wakatwambia basi ili tuwasomeshe wengi, ni bora tuwasomeshe hapa hapa nchini Tanzania na sisi tutahudumia, badala ya kuwa tunakupeni watu sita sasa hivi nafikiri kwa utaratibu huu tunaweza tukafikia watu 12 mpaka 15 tukakusaidieni. Kwa hivyo, utaratibu huu ndio utaanza mwaka huu wa kuwasaidia wale watakao-*qualify* katika zile fani ambazo zimetajwa katika uamuzi wa bodi.Hiyo ndiyo itakayotokezea.

Mhe. Mtando ameuliza juu ya suala la kikao kuwa kilifanyika, na makubaliano yepi yalikwishafikiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Kwa bahati kikao kimefanyika tarehe 4 kama ilivyoandikwa hapa na Waziri wa Elimu alikuja hapa na tukaeleza matatizo yetu kuhusu mambo haya ya mikopo, na yeye kwa sababu tulimpelekea kabla alichoahidi kwamba mwaka huu ataongeza idadi ya mikopo.Lakini hata hivyo, tukazungumzia suala ambalo Mhe. Subeit Khamis Faki ameliuliza kwamba ni vizuri tuwe tuna *quarter* kwa Zanzibar ni wanafunzi wangapi kwa mwaka huu. Hilo hatujalimaliza bado mazungumzo baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hivyo hili linajibika suala la uwiano vile vile, kwamba uwiano watakapofika kukubaliana baina ya Wizara ya Elimu ya Zanzibar na ya Tanzania Bara hapo tutakuwa tuna uwiano. Hivi sasa pana *technical points* ambazo zinazungumzwa namna zinavyopatikana hizi *scholarship* ambapo hatujamaliza, tarehe 4 wameanza tu na Mhe. Waziri amemuahidi kwamba tutaendelea kulizungumza suala hili, na kwa hivyo wataendelea kulizungumza suala hili.

Halafu kuna suala la ucheleweshaji mkubwa wa watu kwenda kujisajili, hili ndilo tatizo ambalo linatokea. Mhe. Spika, kwa sababu tuna wanafuzi wengi wanao-*qualify*, hii inatupa mwanya kuchukua *point* za juu katika mikopo, kwa sababu uwezo wetu si wa kuwasomesha wote. Kwa hivyo, tunachukua *point* za juu katika mikopo, sasa utamkuta mtu yuko chini lakini yuko katika *agree* ile ya *regional qualification* lakini tunaowapa umuhimu ni wale waliofanya vizuri zaidi na wale wengine wanabakia. Lakini kinachotokea ni kwamba mtu anachukua

kama kwamba keshapata *guarantee* kuwa mkopo ataupata, kwa hivyo anakwenda kujisajili mwenyewe na anasema *semester* ya kwanza atajilipia yeye mwenyewe.

Sasa unamhadharisha usifanye hivyo, kwa sababu hatujaona ile orodha ya wote walioomba na zile *passing* zao zilivyo, ukifanya hivyo utaingia kwenye matatizo, matokeo yake kuna wanafunzi wamefanya hivyo na sasa hivi ndio matokeo tuna matatizo ambayo Wizara ya Elimu inakwenda nayo, kwamba kuna mtu keshasoma *semester* moja, keshalipia kwa kutegemea *semester* ya pili atapata mkopo lakini *point* zake hazim-*qualify* katika wale waliochaguliwa kuingia katika mkopo. Sasa hayo ni baadhi ya matatizo ambayo tumekuwa nayo.

Mhe. Spika, hayo ndio masuala ambayo nimeyapata mimi mwisho na majibu yake ndio hayo. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kwa kumruhusu aliyenitangulia kusaidia kujibu hoja, pamoja na kumshukuru yeye mwenyewe kwa kujibu hoja vizuri na amenisaidia sana namshukuru.

Mhe. Spika, sasa naanza kwa Mwenyekiti. Mwenyekiti alipongeza, alitushukuru, lakini pia alituasa kwamba pengine tuwe makini sana wakati wa bajeti namna ya kukisia bajeti zetu za Mafunzo ya Juu, pamoja na kuomba pesa za kutosha, ili wanafunzi wetu waweze kufaidika.Nakubaliana na wazo hilo na hiyo ndiyo dhamira yetu na nilipokuwa nawasilisha hii taarifa nilisema mwaka 2013/2014 bajeti ya Mafunzo ya Elimu ya Juu yataongezeka kwa asilimia 50. Kwa maana nyengine tunakusudia kuomba shilingi bilioni saba badala ya shilingi bilioni nne tulizoomba mwaka jana na tukapata bilioni tatu, tunakusudia kuomba shilingi bilioni saba ili angalau kukidhi mahitaji ya bajeti yetu. Kwa hivyo, hilo tunalo tumelizingatia na namshukuru sana kwa hoja yake.

Nije kwa Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Mheshimiwa amestaajabu kwamba deni hili la shilingi 1,200,080 bado ni kubwa halijalipwa bado, na akatuomba tuwe makini katika kuzitafuta na kuzifuatilia. Alipozungumzia suala la bajeti ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alisisitiza kwa nini tusizigawe kila mmoja akachukua fungu lake, na hapo ndipo tutapokuwa na uwezo mzuri wa kupanga bajeti yetu na kuzitumia vizuri fedha hizi kuliko huu utaratibu unaotumika hivi sasa.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe.Jussa kwa asilimia mia moja kwa utaratibu huo aliouzungumza, na ndio utaratibu uliotawala mazungumzo yetu kwa sababu na mimi nilialikwa katika mazungumzo hayo.Kulitawala mazungumzo tarehe 4 katika suala la sasa tuhangaike lakini tukipate chetu, tukasimiwe madaraka yetu ya kutumia pesa zile ambazo zitatuhusu ili kuweza kuwa na wanafunzi wengi zaidi, na ndio maana tukaweka mkazo kwamba tutazitumia zaidi kwa wanafunzi watakaopata nafasi Vyuo Vikuu vya Tanzania *including* Zanzibar kuliko kwenda nje ya Tanzania, kwa sababu huko ni ghali na inawezekana hata hizo zisitoshe kwa kuzitumia huko.

Mhe. Hamza Hassan Juma nimemfahamu kwamba anataka majibu ya kina kwa sababu yeye ndiye mtoa hoja aridhike na hoja aliyoitoa. Mimi nimefahamu matatizo yake na akaomba basi kama inayumkinika nikubali Kamati ya *PAC* au kamati nyengine yoyote tuiombe itusaidie kuwatafuta hawa waliochukua pesa zetu kwa mkopo, baadae wakatoweka hawakurudi kutulipa.

Mhe. Spika, hilo sina haja ya kulijadili alikubali moja kwa moja. Kwa sababu tunao utaratibu tumeuanzisha pale wizarani wa kutumia *identity cards* kuwatafuta waajiri, kuwatafuta waajiriwa na kwa miezi ya mwanzo michache tumeweza kukusanya shilingi bilioni nne bila ya matatizo. Lakini matatizo yaliyopo ni matatizo ambayo wenzetu Waganda wameyaona ni matatizo yaliyokuwa si ya lazima, na kwa hivyo wakaufuta kabisa huu utaratibu wa mikopo.

Mimi nilipokuwa natoa taarifa yangu nilisema sisi hatufuati utaratibu wa kufuta kabisa, lakini utaratibu wa kujiandaa vizuri, wa kujiandaa kabla ya mikopo, wa kujiandaa kutia mikataba, saini, na wale wakopaji pamoja na wale wanaochukua dhamana halikadhalika, sasa kuangalia zile *identity card* ili tujue hawa waliokopa ni hewa au si hewa kama alivyoonesha *concern* Mhe. Hamza. Kwa hiyo namuomba Mhe. Hamza alichukulie jibu hili litoshe, na pale ambapo pana ulazima wa kuiagiza Kamati ya *PAC* itusaidie kuwatafuta hawa jamaa kama ni hewa au si hewa, wapo au hawapo, mimi nalikubali sana kwa asilimia mia moja kwa sababu watatusaidia kuzipata pesa za serikali.

Mhe. Rashid Seif Suleiman ni pale alipoanzia Mhe. Waziri kupajibu namshukuru sana.

Mhe. Hija Hassan Hija alitaka kujua hawa tuliozungumza nao, na kuwaomba nafasi watusaidie wame-*respond* vipi, wametupa hizo nafasi, wametusaidia, na kadhalika. Mhe. Spika, nilipokuwa natoa taarifa nilisema kwamba kwa mfano hawa *ZSSF* walitukubalia kuwasomesha watoto wetu sisi ndio tutakaochagua, lakini wao wakataka malipo haya tuwalipe kwa riba, yaani tulipe kwa *interest rate*. Kwa kuanzia tumekubali, lakini bado tunaendelea na mazungumzo, *ZSSF* ni taasisi ya Zanzibar, watoto wanaolipiwa ni Wazanzibari, masomo haya ni kwa manufaa ya Wazanzibari. Kwa hivyo, sisi tutaendelea kuzungumza nao, na hatujakata tamaa kwamba watatukubalia.

Lakini wenzetu wa Oman na Waturuki. Watu wa Oman tayari wameshatupa nafasi sita tumeweza kupeleka watu wanne sasa hivi na siku chache zijazo tutawapeleka wale waliobakia. Halikadhalika na Uturuki hatujapata bado *response* nzuri ya Misri na kwengineko, lakini tuna tamaa kubwa sana, mawili katika moja tutapata. Dalili zinaonesha ama watatupa *scholarship* tuwapeleke wanafunzi wetu wakasome bila ya malipo kwa huko, au watawachukua wanafunzi wetu na kuwalipia hapa Zanzibar kwa gharama za hapa Zanzibar, na hilo kwetu sisi tunaliona ni nafuu zaidi kwa sababu tutapata kufundisha wanafunzi wengi zaidi kuliko wakienda kwa *scholarship* katika nchi hizo. Kwa hivyo, mipango hii iko mbioni, mazungumzo yanaendelea na tuna tamaa kubwa sana Mwenyezi Mungu akipenda tutafanikiwa. Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri sasa baada ya majibu hayo kilichobaki ni kuona kama taarifa hii inapokelewa, basi moja kwa moja niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wale wanaopokea taarifa hii ya serikali wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

HOJA ZA SERIKALI

Hoja ya Serikali juu ya Ripoti ya Baraza la Manispaa ya Mji wa Zanzibar

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kuangalia Utendaji wa Baraza la Manispaa, na kupendekeza hatua za kuchukuliwa za kuimarisha utendaji wa Baraza hilo, ripoti hii kama ilivyotayarishwa na kamati iliyoteuliwa na serikali.

Mhe. Spika, ripoti yenyewe *original* ni kubwa kwa kweli ina kurasa zipatazo 89, ni *big document* Mhe. Spika. Sasa hii tumefanya *summary* yake ambayo ndio tunaisambaza na ndio nitayoi-*present.*

Mhe. Spika, kama wizara humu hamna chetu, hii ni ripoti kamili ya kamati kwa hivyo mimi ni mjumbe wa kamati naiwasilisha ripoti hii kama walivyoiwasilisha katika document yao. Labda kama nilivyosema Mhe. Spika, tulichofanya ni kuifupisha tu kwa sababu ya wakati.

Mhe. Spika, ripoti yenyewe kwa muhutasari huu ina kurasa 28, na ina viambatanisho vitatu. Kiambatanisho cha kwanza kiko ukurasa wa 14 ambacho kinaonesha majina ya wajumbe wa kamati pamoja na sekretarieti. Halafu ukurasa wa 15 mpaka 17, inaonesha zile hadidu rejea za kamati walizopewa na serikali, na mwisho kabisa kiambatanisho cha tatu Mhe. Spika, kinaonesha Bango Kitita ya eneo, hoja na maelezo ya kamati pamoja na maoni ya ofisi yaani wizara sasa nini mtazamo wetu, ndio tumetoa maoni yetu. Sasa kwa ruhusa yako Mhe. Spika, naomba moja kwa moja niwasilishe ripoti hii.

Chimbuko la Kazi:

Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba imedhamiria kuimarisha utendaji kazi wa taasisi mbali mbali za serikali kwa lengo la kuongeza kasi ya maendeleo na kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi. Kutokana na malalamiko ya wananchi na wadau mbali mbali wa Baraza la Manispaa la Zanzibar juu ya hali ya utendaji wa Baraza hilo, serikali iliamua kuunda kamati ya wataalamu kutoka sekta mbali mbali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa ajili ya kuangalia kwa kina utendaji na changamoto zinazoikabili Baraza hilo.

Aidha, kamati ilipewa jukumu la kutoa mapendekezo kwa serikali, juu ya hatua muafaka za kuchukuliwa, ili kuweza kuimarisha utendaji wa Baraza la Manispaa na kuliwezesha kutoa huduma kwa jamii kwa ufanisi zaidi.

Kuundwa kwa Kamati na Majukumu yake (hadidu rejea):

Kamati ya Wataalamu yenye wajumbe 10 kutoka kwenye taasisi mbali mbali za serikali iliundwa kwenye tarehe 24 Mei, 2011, na kuanza kutekeleza majukumu yake tarehe 3 Juni, 2011, baada ya kukutana katika kikao cha kwanza ambapo walikubaliana kuwepo na wajumbe watatu wa sekretarieti kutoka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. *List* ya wajumbe wa kamati imeoneshwa katika kiambatanisho cha kwanza. Kwa kuipa uzito kamati yenyewe naomba Mhe. Spika, niitaje.

Wajumbe wa Kamati ni kama wafuatao:

1. Dr. Khalid S. Mohammed - Katibu Mkuu Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais
2. Ndugu Asha Ali Abdalla - Katibu Mkuu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika.
3. Ndugu Mwalimu Ali Mwalimu– Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati.
4. Ndugu Abdi Khamis Faki - Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.
5. Ndugu Mwinyiusi A. Hassan- Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ.
6. Ndugu Said Hassan Said - Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali.
7. Ndugu Omar Hassan Omar- Mhasibu Mkuu wa Serikali
8. Ndugu Naim Ramadhan Pandu- Mkurugenzi Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.
9. Ndugu Kai Bashir Mbarouk Mkurugenzi wa Utumishi, Uendeshaji Wizara ya Katiba na Sheria.

10 Ndugu Abdulrahman Mnoga - Afisa Mwandamizi Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mhe. Spika, Wajumbe wa Sekretarieti ni watatu. Kwanza Ndugu Issa Ibrahim Mahmoud yeye ni Mkurugenzi Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa Ofisi ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais. Wa pili Ndugu Amina Talib Ali Mwanasheria Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Wa tatu Ndugu Asya Yahya Hussein Afisa Uratibu Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Mhe. Spika, hiyo ndio orodha kamili ya Kamati iliyofanya kazi. Ripoti hii iliwasilishwa rasmi serikalini mwezi Agosti , 2011.

Njia zilizotumika katika kukusanya taarifa

Mhe. Spika, katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya kamati njia mbali mbali zilitumika katika kukusanya taarifa. Njia hizo ni kupitia nyaraka mbali mbali, kufanya majadiliano ya ana kwa ana na wadau mbali mbali na kutembelea sehemu mbali mbali za Baraza la Manispaa.

Muundo wa Taarifa Kamili ya Kamati

Kamati imeweza kuyaangalia maeneo 13 ya kiutendaji ndani ya Baraza na kutoa mapendekezo yake. Sehemu ya tatu inaelezea Muundo na Majukumu ya Baraza la Manispaa. Sehemu ya nne inaelezea Sheria ya Baraza la Manispaa Nam. 3 ya mwaka 1995. Mipango na Bajeti inaelezwa katika sehemu ya tano na sehemu ya sita inaelezea juu ya Mfumo wa Usimamizi wa Fedha. Sehemu ya saba inaelezea nguvu kazi katika Baraza la Manispaa na sehemu ya nane inaelezea juu ya Mazingira ya Kazi ya Baraza la Manispaa. Miundombinu ya Baraza la Manispaa imeelezewa katika sehemu ya tisa.

Mhe. Spika, sehemu ya kumi inaeleza juu ya uzoefu wa Baraza la Manispaa katika kutayarisha, kutekeleza na kusimamia miradi mbali mbali. Aidha, sehemu ya kumi na moja imegusia mambo mengineyo kuhusu Baraza la Manispaa na sehemu ya kumi na mbili inatoa mapendekezo ya kamati juu ya hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto zilizopo katika Baraza la Manispaa. Sehemu ya kumi na tatu na ya mwisho inatoa hitimisho la taarifa hiyo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba hadudi rejea za kamati zimeoneshwa katika kiambatanisho cha pili ukurasa wa 15. Wajumbe wanaweza kuziangalia hapo sina haja ya kuzisoma ziko hadudi rejea 13 kwenye ukurasa wa 15 mpaka 17. Hayo ndio majukumu ya kamati waliyopewa.

MAELEZO YA JUMLA KUHUSU BARAZA LA MANISPAA

Eneo la Baraza

Mhe. Spika, Baraza la Manispaa la Zanzibar lina jumla ya wadi 20 na shehia 45. Kutokana na Sensa ya Idadi ya Watu na Makaazi iliyofanyika mwaka 2002 idadi ya watu wanaoishi katika eneo la Manispaa ya Zanzibar ni 205,810, wanaume 99,248 na wanawake 106,622. Ongezeko la idadi ya watu linakadiriwa kufikia asilimia 3 kwa mwaka. Idadi ya watu kwa eneo nayo inakadiriwa kuwa watu 350 katika eneo la kilomita moja ya mraba. Kwa wastani watu 7 wanaishi katika familia moja katika Manispaa ya Zanzibar. Makadirio rasmi ya idadi ya watu katika Manispaa ya Zanzibar hivi sasa ni watu 250,000. Idadi hii inatarajiwa kuongezeka mara mbili kufikia watu 470,000 ifikapo mwaka 2015. Baraza la Manispaa lina jumla ya wadi 20 na shehia 45. Jadweli namba moja inaonesha wadi na shehia katika Manispaa ya Zanzibar kama zilivyooneshwa wadi hizo hapo na shehia hizo hapo.

Muundo

Baraza la Manispaa la Zanzibar kwa mujibu wa sheria lina madiwani wa wadi 20 wa kuchaguliwa, sita wa viti maalum na watatu wa kuteuliwa na Waziri anayehusika. Vile vile Baraza linaongozwa na Mstahiki Meya na Naibu Meya, Meya ndie Mwenyekiti wa Baraza na Mkurugenzi wa Manispaa ni Katibu wa Baraza ambaye pia ni Mtendaji Mkuu akisaidiwa na Wakuu wa Idara 5. Idara hizo ni kama ifuatavyo:

(a) Idara ya Fedha na Uchumi
(b) Idara ya Mipango Miji
(c) Idara ya Sheria na Utawala
(d) Idara ya Huduma za Jamii
(e) Idara ya Kazi, Ujenzi na Mazingira

Vile vile kuna Kamati za Kudumu 5 za Baraza la Manispaa ambazo ni kama ifuatavyo:

1. Kamati ya Uchumi na Fedha
2. Kamati ya Sheria na Utawala
3. Kamati ya Mipango Miji
4. Kamati ya Huduma za Jamii
5. Kamati ya Kazi na Ujenzi wa Mazingira

Majukumu ya Msingi

Kwa mujibu wa Sheria ya Baraza la Manispaa Nam. 3 ya mwaka 1995 Manispaa ina majukumu manne ya msingi kama ifuatavyo:

1. Kushughulikia na kusimamia usafi wa mji. Mfano, ukusanyaji na uondoaji taka, ujenzi na usafishaji wa michirizi, makaro, vyoo na kadhalika.
2. Kusimamia maeneo ya wazi na bustani *(open spaces)*, barabara, taa za barabarani na uimarishaji wa maegesho.
3. Upandaji na ukataji miti pembezoni mwa barabara.
4. Usimamiaji wa Mipango Miji.

CHANGAMOTO ZINAZOLIKABILI BARAZA LA MANISPAA NA MAPENDEKEZO YA KUKABILIANA NAZO

Baada ya kukusanya taarifa za uendeshaji wa Baraza la Manispaa na kupata maoni kutoka kwa wadau mbali mbali juu ya changamoto zinazolikabili Baraza hilo, Kamati inatoa mapendekezo yenye lengo la kuimarisha utendaji wa Baraza la Manispaa na kuliwezesha kutoa huduma bora, endelevu na zenye unafuu kwa wananchi. Mapendekezo hayo ni kama ifuatavyo:

Kutayarisha Sera ya Serikali za Mitaa

Baraza la Manispaa kwa sasa linatekeleza majukumu yake bila ya kuwepo kwa Sera ya Serikali za Mitaa. Kukosekana kwa Sera ya Serikali za Mitaa kunalifanya Baraza kutokuwa na miongozo katika kuandaa mipango na programu za maendeleo. Kutokana na hali hii, Kamati inapendekeza kutayarishwa Sera ya Serikali za Mitaa

ili kuwa na muongozo na usimamizi mzuri wa utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Manispaa na Halmashauri nyengine zilizopo Zanzibar.

Kufanyiwa Mapitio Sheria ya Baraza la Manispaa Nam. 3 ya mwaka 1995 na kuandaa Sheria ya Serikali za Mitaa

Kutokana na mgongano mkubwa wa kisheria baina ya Sheria ya Baraza la Manispaa Nam. 3 ya mwaka 1995 na sheria nyengine za kisekta ziliopo katika ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa rasilimali katika Mji wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na Sheria ya Mji Mkongwe. Kamati inapendekeza kufanyiwa mapitio sheria hiyo na kuainisha *(harmonization)* na sheria nyengine ili kulifanya Baraza la Manispaa liweze kuendesha kazi zake kwa ufanisi na bila ya migongano na taasisi nyengine.

Sambamba na hilo, Kamati inapendekeza iandaliwe Sheria ya Serikali za Mitaa. Sheria hii itaweka miongozo ya kisheria kwa masuala ya kiutendaji ambayo utekelezaji wake utaondoa au kupunguza matatizo ya ajira, manunuzi, ukusanyaji wa mapato, matumizi na pia itaweka bayana majukumu ya wahusika mbali mbali na kuainisha kwa uwazi sifa zinazohitajika za Mkurugenzi na Maafisa wengine wa Serikali za Mitaa.

Kuweka Mipaka Mipya ya Eneo la Baraza la Manispaa

Mhe. Spika, imebainika kwamba Mji wa Zanzibar umeongezeka kwa kiasi kikubwa hivi sasa na mipaka ya eneo la Baraza haieleweki rasmi kisheria hivyo kusababisha muingiliano na migongano katika majukumu baina ya Baraza la Manispaa na Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi. Kutokana na hali hii, Kamati inapendekeza Serikali kufikiria mipaka mipya ya eneo la Baraza la Manispaa na kuiweka kwenye sheria husika na kuitangaza kwenye Gazeti Rasmi la Serikali ili ieleweke na kuondoa migongano na kuimarisha utendaji wa Baraza la Manispaa katika kutoa huduma na ukusanyaji wa mapato kama inavyostahiki.

Kufanyiwa Mapitio Muundo wa Baraza la Manispaa

Mhe. Spika, Kamati imebaini kwamba muundo wa sasa wa Baraza la Manispaa una upungufu mkubwa na unahitaji kufanyiwa mapitio. Muundo uliopo hauzingatii majukumu muhimu ya Baraza na unachanganya majukumu katika kitengo kimoja. Aidha, muundo huo hauoneshi vitengo muhimu kama vile Kitengo cha Mipango, Uchumi na Utafiti, Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini, Kitengo cha Manunuzi, Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Kitengo cha Huduma kwa Wateja. Kwa ujumla hali hii inapelekea kuwa na mrundikano wa majukumu na kupunguza ufanisi.

Katika kulitafutia ufumbuzi tatizo hili Kamati inapendekeza kufanyiwa mapitio muundo wa Baraza na kuunda muundo mpya utakaoendana na majukumu muhimu *(core functions)* ya Baraza. Kuondoa migongano ya majukumu baina ya Baraza la Manispaa na Taasisi nyengine.

Mhe. Spika, kumekuwepo na migongano katika utekelezaji wa majukumu baina ya Baraza la Manispaa na Taasisi nyengine za Serikali. Baadhi ya Taasisi hizo ni Bodi ya Mapato ya Zanzibar *(ZRB)*, Mamlaka ya Uhifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, Wizara ya Kilimo na Maliasili, Wizara ya Mifugo na Uvuvi na hata Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pamoja na Kamisheni ya Utalii.

Mhe. Spika, migongano iliyopo inatokana na baadhi ya vifungu vya sheria mbali mbali. Hali hii imebainika kwamba inazorotesha uwajibikaji katika ukusanyaji wa mapato, utoaji huduma na uwekezaji katika Mji wa Zanzibar. Katika kulikabili tatizo hili Kamati inapendekeza kuainisha sheria ziliopo ili kuondoa mgongano na kuimarisha utendaji wa Baraza la Manispaa. Aidha, Kamati inasisitiza haja ya kutekelezwa kwa haraka mageuzi ya Serikali za Mitaa *(Local Government Reforms).*

Kuimarisha Kazi za Ukusanyaji wa Mapato

Mhe. Spika, miongoni mwa changamoto kubwa za Baraza la Manispaa ni wigo mdogo wa ukusanyaji wa mapato, mgongano wa Taasisi mbali mbali katika ukusanyaji wa mapato na kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa ukusanyaji wa mapato hayo. Kutokuwa na mfumo mzuri wa ukusanyaji wa mapato kunatoa mwanya wa upotevu wa mapato na kupelekea Baraza kuendelea kuwa tegemezi kwa ruzuku kutoka Serikalini.

Katika kulitafutia ufumbuzi suala hili Kamati inapendekeza ufanywe utafiti utakaopelekea kujua vyanzo mbali mbali vya mapato kwa Baraza la Manispaa. Uwezo wa vyanzo hivyo katika kuzalisha mapato na kuandaa

mfumo mzuri wa kisasa wa ukusanyaji wa mapato na usimamizi wake ambao unatambua vyanzo vya walipa kodi au ada kwa wote *(data base system)* ili kuongeza ukusanyaji wa mapato na kuimarisha uwekezaji wenye tija katika Baraza. Vile vile Kamati Mhe. Spika, inapendekeza Baraza kuwa na mpango endelevu wa kutoa elimu kwa walipa kodi au ada ili kuongeza uwajibikaji na walipa kodi/ada *(compliance).*

Kuwepo mfumo mzuri kwa kuandaa mipango na kuwa na usimamizi mzuri wa fedha za Baraza

Mhe. Spika, hali ya sasa ya Baraza ni kwamba Baraza halina mfumo mzuri wa kuandaa mipango ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Aidha, Baraza halina Mpango Mkakati madhubuti *(strategic plan)* na hakuna Kitengo cha Mipango. Vile vile Baraza halina Maofisa wa Mipango wenye sifa za kielimu katika masuala ya mipango. Hii inapelekea kuwa na Bajeti zisizoendana na majukumu ya Baraza *(core functions)* na kuwa na matumizi makubwa kwa masuala ya uendeshaji wa Baraza badala ya uwekezaji.

Katika kulitafutia ufumbuzi suala hili Kamati inapendekeza kuanzishwa kwa Kitengo cha Mipango na Uendeshaji na kukiimarisha Kitengo cha Mkaguzi wa Ndani wa Hesabu na Sehemu ya Hesabu kwa kuwaajiri Wahasibu wenye sifa kwenye dhamana hizo.

Kamati pia inapendekeza kuajiri kwa Maafisa wa Mipango wenye sifa nzuri za elimu na kuandaliwa kwa Mpango Mkakati wa Baraza la Manispaa. Kamati pia inapendekeza kuandaliwa kwa utaratibu mzuri wa matumizi ya fedha za Baraza na utoaji wa taarifa za mapato na matumizi ili kuwezesha ufungaji wa hesabu za kila mwaka.

Kuimarisha Mahusiano katika Utekelezaji wa Majukumu ya Baraza la Manispaa

Mhe. Spika, mahusiano yaliyopo katika utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Manispaa yana upungufu mkubwa na yanaathiri utekelezaji wa majukumu ya Baraza ya kila siku. Kumejitokeza migongano ya kiutendaji baina ya Uongozi, Watendaji na Waheshimiwa Madiwani. Hapana utaratibu mzuri wa mawasiliano baina ya watendaji wa Baraza. Aidha, hakuna utaratibu mzuri wa kuweka kumbukumbu za vikao vya Wajumbe wa Baraza la Manispaa na watendaji. Suala hili limebainika kwamba linakwamisha utendaji wa Baraza kwa kiasi kikubwa. Kamati inapendekeza kuwekwa wazi kwa mipaka ya kazi na majukumu baina ya viongozi wa Baraza na watendaji na zaidi inasisitizwa kufuatwa kwa sheria na taratibu ziliopo katika uendeshaji wa Baraza na kutekeleza majukumu ya Baraza.

Vile vile inashauriwa kuwekwa wazi kwa majukumu ya Wizara inayohusika na Serikali za Mitaa, Baraza na watendaji wa Baraza na kuanzisha utaratibu wa ushirikishwaji wa viongozi na watendaji wa Baraza pamoja na wadau wengine kutoa maoni, ushauri na katika mambo yanayolihusu Baraza ikiwemo masuala ya mipango na uwekezaji.

Kuimarisha Utunzaji na Usimamizi kwa Maeneo ya Bustani na Maeneo ya Wazi

Mhe. Spika, Kamati imebaini kwamba kuna tatizo la umiliki, utunzaji na uendeshaji wa maeneo ya bustani, maeneo ya michezo na maeneo mengine ya wazi unaotokana na kutotii sheria ziliopo ambayo hupelekea matumizi mabaya na uvamizi kwa baadhi ya maeneo. Hii inatokana na kukosekana kwa usimamizi mzuri wa sheria, hatimiliki na huduma muhimu. Katika kulipatia ufumbuzi suala hili Kamati inapendekeza kupimwa kwa maeneo yote ya wazi na kutolewa kwa hatimiliki kwa taasisi inayostahiki kwa ajili ya kuwa na mipango mizuri ya kuyaendeleza maeneo haya, ikiwemo uwekezaji katika miundombinu, ustawishaji wa mazingira na haiba ya Mji wa Zanzibar.

Kuweka Utaratibu Mzuri wa Uajiri, Mafunzo na Maslahi kwa Wafanyakazi

Mhe. Spika, Kamati imegundua kwamba hadi sasa Baraza la Manispaa halina utaratibu mzuri wa uajiri, mafunzo na maslahi kwa wafanyakazi. Hali hii imepelekea kuwa na ajira za kiholela na kulifanya Baraza kuwa na watumishi wengi wasiokuwa na tija. Aidha, Baraza halina mpango wa mafunzo kwa wafanyakazi wake na hakuna Muundo wa Utumishi wa Baraza *(Scheme of Service).* Hali hii inaondosha ari kwa wafanyakazi kujituma na kutoa huduma bora kama inavyohitajika.

Aidha, Kamati inapendekeza kuandaliwa kwa Sheria ya Serikali za Mitaa na katika utekelezaji wa sheria hiyo Baraza liwe na muundo wake wa utumishi. Baraza liajiri wafanyakazi kwa mujibu wa mahitaji yake na kwa taratibu zinazokubalika katika mamlaka ya Serikali za Mitaa. Baraza lifanye tathmini na kutambua mahitaji ya mafunzo kwa wafanyakazi wake *(training needs assessment)* na kutokana na matokeo ya tathmini hiyo

kuandaliwe mpango wa Baraza wa mafunzo kwa watendaji na viongozi yaani mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Baraza pia liajiri wataalam katika fani za Uhandisi, Uhasibu, Uchumi, Sheria, Mipango, Miradi, Mipango Miji, Ununuzi, Ufuatiliaji na Tathmini na fani nyengine muhimu. Wafanyakazi wa Baraza waliofikia umri wa kustaafu kisheria wastaafishwe kwa mujibu wa sheria ziliopo na kuajiriwa wafanyakazi wapya kwa mujibu wa mahitaji ya uwezo wa Baraza.

Kuimarisha Upatikanaji wa Vitendea Kazi

Mhe. Spika, tatizo la uhaba wa vitendea kazi katika Baraza la Manispaa ni kubwa jambo ambalo limebainika kwamba linakwamisha kazi za uendeshaji wa Baraza na utoaji wa huduma kwa jamii. Vitendea kazi hivyo ni pamoja na majengo ya ofisi, vifaa vya ofisi na samani na vyombo vya moto na vifaa vinavyotumika kwa ajili ya kutoa huduma za usafi. Ili kulipatia ufumbuzi tatizo hili Kamati inapendekeza Baraza liongeze juhudi zaidi katika uwekezaji na ukusanyaji wa mapato na hivyo kuongeza uwezo wake wa kufanyia ukarabati majengo yake na kununua vifaa vya ofisini na vya kufanyia kazi za usafi wa mji. Kamati inashauri Baraza kuanza kuandaa mpango wa muda mrefu wa kuwa na majengo yake mapya yenye hadhi kuendana na wakati wa sasa wa ongezeko la matumizi ya sayansi na teknolojia kama matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano *(ICT).*

Kuimarisha Miundombinu ya Baraza la Manispaa

Mhe. Spika, suala la miundombinu hasa ya michirizi ya maji machafu na ya mvua, bustani, maegesho, taa za barabarani vyoo vya umma haiko katika hali ya kuridhisha na hivyo kuwa ni changamoto katika kuimarisha utendaji wa Baraza la Manispaa. Katika kulitafutia ufumbuzi suala hili Kamati inapendekeza Baraza kuweka utaratibu mzuri wa kuimarisha na kujenga miundombinu mipya kwa kushirikisha sekta binafsi na mashirika ya maendeleo.

Vile vile Kamati inapendekeza kuwa Baraza kuanza kufikiria kushirikisha watu wengine kufanya kazi za Baraza kama Jumuiya za Kiraia *(CBOs* na *NGOs)* na hata sekta binafsi, hasa katika masuala ya ujenzi na uendeshaji wa masoko, miundombinu ya usafi na utoaji wa huduma mbali mbali kama maegesho ya magari na usafi.

Aidha, Kamati inapendekeza kwamba Baraza liwe na usimamizi mzuri wa miundombinu yake ikiwemo kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kuifanyia matengenezo miundombinu hiyo kila inapohitajika.

Kuweka Utaratibu Mzuri wa Ununuzi na Ufungaji wa Mikataba

Mhe. Spika, Kamati imebaini kwamba uwazi katika kufanya ununuzi na ufungaji wa mikataba ni mambo muhimu katika Taasisi yoyote ili kuondoa utata unaoweza kujitokeza wa kuwa na matumizi mabaya ya fedha. Katika Baraza la Manispaa suala hili ni changamoto kubwa kutokana na ukweli kwamba hadi sasa hakuna Kitengo cha Manunuzi na hakuna Bodi ya Manunuzi ambapo ni kinyume na matakwa ya Sheria ya Manunuzi na uondoshaji wa mali za Serikali ya mwaka 2005. Aidha, Kamati imegundua kuwepo kwa utata mkubwa katika ufungaji wa mikataba kwa kukosekana uwazi wa kuwapata wakodishwaji wa mali za Baraza na kutofuatwa kwa taratibu za kisheria.

Katika kulitafutia ufumbuzi suala hili Kamati inapendekeza Baraza la Manispaa lianze kutumia kikamilifu Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali ya mwaka 2005 na kuwa na wataalam wenye sifa katika fani hiyo. Vile vile Kamati inapendekeza Baraza limuajiri Mwanasheria mwenye sifa kuweza kusaidia katika utayarishaji na uingizaji wa mikataba na makampuni binafsi. Aidha, ni vyema Baraza la Manispaa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kuandaa mikataba kabla ya kuwekwa saini ili kusaidia ushauri katika kusaidia Baraza kutopoteza haki zake kutokana na mikataba mibovu.

Kujenga Uwezo kwa Baraza katika Utayarishaji, Uendeshaji na Usimamiaji wa Miradi ya Maendeleo

Mhe. Spika, suala la utayarishaji, uendeshaji na usimamizi wa miradi ya maendeleo katika Baraza la Manispaa ni changamoto kubwa. Hii inatokana na uhaba wa wataalam na kukosekana kwa mifumo bora ya utayarishaji wa mipango, usimamizi wa fedha, mfumo wa manunuzi, uwekaji wa kumbukumbu, ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa taarifa za utekelezaji. Katika kufuatilia ufumbuzi wa suala hili Kamati inapendekeza Baraza liwe na wataalam wenye sifa za elimu na uzoefu katika fani ya mipango, fedha, ununuzi, ufuatiliaji na tathmini. Kamati pia inashauri kuanzisha mifumo bora ya kusimamia utekelezaji wa miradi mikubwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano *(ICT).*

Kuanzisha Programu za Kutoa Elimu kwa Umma

Mhe. Spika, kutokana na taarifa ambazo Kamati imezipata inaonesha kwamba bado jamii kubwa ya Wazanzibari haina uelewa juu ya umuhimu wa Baraza la Manispaa na haja kwa jamii kutoa ushirikiano na Baraza hilo katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, jamii haijahamasika ipasavyo katika kuimarisha na kutunza Mji wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na kudumisha usafi, kuacha kutupa taka ovyo, utunzaji wa bustani na kufuata taratibu katika kuegesha magari. Vile vile wananchi hawajakuwa na uelewa wa kutosha juu ya dhana na umuhimu wa kuchangia kwa huduma mbali mbali zinazotolewa na Baraza. Pia wapo wananchi wanaokwepa kulipa ada na kodi za Baraza.

Mhe. Spika, kutokana na hali hii Kamati inapendekeza Baraza la Manispaa lichukue jitihada maalum ya kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuimarisha na kutunza mji wetu. Baraza pia liandae mpango wa kuhamasisha jamii katika utunzaji wa mazingira, bustani na maeneo ya wazi pamoja na miundombinu ya usafi na masoko na kuonesha umuhimu kwa jamii kushirikiana na Baraza kwa kutoa michango yao. Sambamba na hilo ipo haja ya kusimamia utekelezaji kikamilifu wa sheria ambayo itawabana wale wote wanaokwenda kinyume na taratibu na sheria ziliopo katika utupaji taka ovyo, kuegesha magari pahala pasipostahiki na kukwepa kulipa kodi na kutodhibiti wanyama wanaozurura ovyo katika eneo la manispaa.

Kuimarisha Uwekaji wa Taarifa Muhimu

Mhe. Spika, Kamati vile vile imebaini kuwepo kwa udhaifu mkubwa wa udhibiti na uwekaji wa taarifa muhimu katika Baraza la Manispaa. Taarifa nyingi hazionekani na baadhi ya kumbukumbu za vikao pia hazionekani, uwekaji wa majalada katika ofisi zilizotembelewa pia hauridhishi. Kamati inapendekeza kuimarishwa uwekaji wa taarifa pamoja na kuwapatia mafunzo wafanyakazi husika juu ya uwekaji wa kumbukumbu.

HITIMISHO

Mhe. Spika, kwa kuhitimisha Kamati imefanya kazi ya kuangalia utendaji wa Baraza la Manispaa, kuainisha upungufu uliopo katika utendaji na kutoa mapendekezo ya kuimarisha utendaji wa Baraza hilo. Matokeo ya kazi hii yameonesha kuwepo kwa upungufu katika maeneo mengi ya Baraza la Manispaa ikiwemo masuala ya sera na sheria, uendeshaji, nguvu kazi, uwekezaji, mapato na matumizi.

Katika kukabiliana na upungufu uliopo Kamati imetoa mapendekezo ya kina ikiwemo haja ya kuwa na Sera ya Sheria ya Serikali za Mitaa, kujenga uwezo wa kitaasisi *(Institutional Strengthening)* ili kuliwezesha Baraza la Manispaa kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Mhe. Spika, mapendekezo haya ni mengi na si rahisi yote kuweza kutekelezwa kwa wakati mmoja. Hivyo ni vyema ukaandaliwa Mpango wa Utekelezaji *(Action Plan)* mpango ambao utaonesha mapendekezo yanayohitajika kutekelezwa kwa haraka *(Shortcoming Interventions)* na yale yanayohitaji muda wa kuweza kutekelezwa *(Medium and Long Term Interventions).* Vile vile mpango huo ni muhimu kuonesha wahusika katika utekelezaji na kuwa na viashiria *(indicators)* vya kupima mafanikio katika utekelezaji wa mpango huo.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 19 kama nilivyosema naonesha Bango Kitita kwanza inaonesha eneo la kufanyiwa kazi mfano kufanyiwa mapitio muundo wa Baraza la Manispaa, hoja yenyewe, maelezo ya Kamati na maoni ya ofisi. Yote tumekwenda nayo kwanza Kufanyiwa Mapitio Muundo wa Baraza la Manispaa, Upungufu katika Mfumo wa Kisheria Uliopo Unaokwamisha Utekelezaji wa Baraza la Manispaa. Tatu Mipango ya Bajeti. Halafu ukurasa wa 21 Kuweka Mipaka Mipya ya Eneo la Baraza la Manispaa, Migongano na Majukumu Baina ya Baraza la Manispaa na Taasisi Nyengine za Serikali, pia Kuimarisha Kazi za Ukusanyaji wa Mapato.

Ukurasa wa 22 Kuimarisha Mahusiano katika Utekelezaji wa Majukumu ya Baraza la Manispaa. Ukurasa wa 23 Utunzaji na Usimamizi kwa Maeneo ya Bustani na Maeneo ya Wazi. Ukurasa wa 24 Kuweka Utaratibu Mzuri wa Uajiri, Mafunzo na Maslahi kwa Wafanyakazi. Ukurasa wa 25 Kuimarisha Upatikanaji wa Vitendea Kazi, pia Kuimarisha Miundombinu ya Baraza la Manispaa. Ukurasa wa 26 Utaratibu Mzuri wa Ununuzi na Ufungaji wa Mikataba, pia Kujenga Uwezo kwa Baraza katika Utayarishaji, Uendeshaji na Usimamiaji wa Miradi ya Maendeleo. Ukurasa wa 27 pia Elimu kwa Umma, pia Kuimarisha Uwekaji wa Taarifa Muhimu.

Kwa hivyo, hizi kurasa nilizozizungumza zinaonesha eneo na hoja yenyewe, maelezo ya Kamati na mapendekezo yao na maoni ya ofisi.

Mhe. Spika, kwa muhtsari huu ndio ripoti ya Kamati ya kuangalia utendaji wa Baraza la Manispaa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, makofi yalikuwa mengi, hoja imetolewa na sijui kama imeungwa mkono. (Vicheko/Makofi)

Kama hoja imeungwa mkono, basi tuijadili.Sasa labda mjadala huu utupeleke kwenye ripoti hii. Hii ni ripoti ya hiyo tume ambayo iliundwa, ni ripoti ya Serikali. Kwa hivyo, kila kwenye hoja fulani kuna mapendekezo, nafikiri Waheshimiwa Wajumbe tunachoweza kufanya hapa ni kuona je, mapendekezo haya yanatosha au kuna nyongeza ambayo nyinyi mnayo huko, ili sasa tumpe Mhe.Waziri hapa kwa ajili ya kuifanyia kazi pamoja na haya yaliyoripotiwa kwetu.

Basi mchangiaji wa kwanza atakuwa ni Mhe. Omar Ali Shehe na baadae Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza kuhusiana na ripoti hii inayohusiana na Baraza la Manispaa.Mhe. Spika, msingi wa hoja hii tutaona kwamba ilikuwa ni ripoti ya Waheshimiwa Madiwani, waliyoitoa katika kikao chao cha manispaa.

Naomba nitumie fursa hii Mhe.Spika, niwapongeze sana madiwani wale, kwa kuwa makini na wenye uchungu wa maendeleo ya manispaa yao hii ya Zanzibar.Mhe. Spika, katiba yetu ya Zanzibar kifungu cha 5, kinaelezea mgawanyiko wa madaraka baina ya mihimili mitatu. Serikali kazi yake kubwa ni jukumu la utekelezaji, Baraza letu lina jukumu la kutunga sheria pamoja na kuisimamia serikali shughuli zake na Mahakama ina jukumu la kutafsiri sheria zinazotungwa na chombo hiki.

Mhe.Spika, kama hivyo ndivyo, basi Baraza la Wawakilishi kwa sababu kitendo kile kimefanywa na serikali, bado narudia hoja yangu kwamba Baraza hili ndilo lililokuwa na wajibu wa kusimamia shughuli za serikali na kwa msingi huo, Baraza ndilo lililokuwa lina wajibu wa kuunda tume ili ichunguze matendo ya serikali.

Mhe. Spika, kwa wakati ule Baraza lilitoa hoja, lakini serikali iliingilia kati, ikasema wao tayari wameshaunda tume.Wameharibu wao na wao waunde tume wajichunguze wao. Kitu ambacho leo kimedhihirika kwamba serikali haikuwa na uwezo huo wa kuharibu na kujichunguza wenyewe.Ripoti iliyowasilishwa na Mhe. Waziri imeonesha hivyo, kwamba serikali inapoharibu, basi haina uwezo wa kujisimamia na kujichunguza.

Mhe. Spika, mimi ninayo ripoti ya Waheshimiwa Madiwani, naomba niisome ripoti ya madiwani ambayo imesema, mapendekezo kwa serikali, katika 31.

> "Kufuatia kamati kubaini kuwa Baraza la Manispaa lina maovu mengi kuliko mafanikio, yaliyosababishwa na mtu mmoja kwa kupindisha sheria na kanuni kwa makusudi.Kamati inashauri kufanya mabadiliko katika nafasi ya Mkurugenzi".

Mhe. Spika, hilo ni moja kati ya mengi ya mapendekezo yaliyotolewa na kamati iliyoundwa na manispaa yenyewe.

Sasa Mhe. Spika, kwa kweli katika Baraza la Manispaa, kama ilivyoeleza katika ripoti hii na kama sisi wawakilishi wa wananchi tunaopita mitaani tunaosikia na kuona, kwa kweli Baraza la Manispaa lina *chaos* kubwa sana. Lina matatizo makubwa ya kiutendaji, kwa sababu wafanyakazi wenyewe wanatueleza hivyo, kuwa Baraza la Manispaa lina matatizo makubwa ya ubadhirifu wa fedha, na Baraza la Manispaa lina matatizo makubwa ya upindishaji wa sheria zilizowekwa.

Mhe. Spika, tulitegemea leo serikali itakuja na jawabu juu ya uchunguzi walioufanya, lakini inasikitisha na ndio ile hoja yangu kwamba serikali haikuwa na uwezo wa kuharibu na baadae kujiundia tume kujichunguza wenyewe.Tulitegemea tupate ripoti, lakini Mhe. Spika, ripoti hatukupata, tumepata maelezo tu ambayo kwa kweli hayana mbele wala hayana nyuma. Tulitegemea tupate ripoti kamili, hii ripoti ya madiwani kwa kweli pamoja na kwamba ni wanasiasa wenzetu ambao kidogo kiwango chetu tunalingana, lakini ina *content* nzuri sana, imekwenda mbali mno kuweza kujua tatizo, kiini na namna ambavyo Baraza la Manispaa linaweza kurekebishwa kutokana na ripoti hii ya manispaa.

Mhe. Spika, bado ninasikitika kwamba serikali haikuleta jawabu juu ya tuliyoyataka, kwa kweli imetupotezea muda, kwa sababu tuliliomba Baraza hili liunde kamati teule kuchunguza, serikali ikaliingilia kati. Kwa maana

hiyo Mhe. Spika, mimi nataka nitoe hoja, kwamba ripoti hii tunaikataa kwa sababu haikufanya chochote. *(Makofi).*

Mhe. Spika, zile ni fedha za wananchi walipa kodi wa manispaa hii ya Zanzibar, kwa msingi huo kufanya mambo ya mchezo na fedha za walipa kodi ni kitu ambacho hakikubaliki. Kwa msingi huo basi sisi tunakubaliana na madiwani, kama walivyoagiza na kwa msingi huo Mhe. Spika, chombo chako hiki naomba sasa tuirudishe ripoti hii tusiipokee na badala yake Baraza la Wawakilishi liunde kamati teule kwa ajili ya kuchunguza manispaa. Mhe Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naomba nitoe mchango wangu kwa ufupi juu ya maelezo ya taarifa fupi ya kamati ya kuangalia utendaji. Hii Mhe. Spika, haikuwa kamati ya kuchunguza, ilikuwa ni kamati ya kuangalia utendaji wa manispaa.

Mhe. Spika, mara kadhaa Baraza hili, Mhe. Waziri amekuwa na kauli ya kutuambia kwamba tumuamini, kila akizungumza anasema niaminini. Kwa hivyo, baadhi ya wajumbe wamekuwa na hofu kwamba tukuamini wewe kila mara kwa nini. Bahati nzuri leo Mhe. Spika, imedhihirika kwamba Mhe. Waziri mimi binafsi ananishawishi kuwa nisimuamini.

Mhe. Spika, kwa kweli muda wetu umepotea. Tulisema kuwa nyinyi kama serikali hamuwezi kujichunguza, akatuambia niaminini. Leo anatuletea hadithi badala ya ripoti. Sisi hatukumwambia atuletee utendaji kazi wa karo na bustani. Aliagizwa aangalie upotevu wa fedha na uvunjaji wa sheria, yote hakuyazungumza.

Mhe. Spika, nadhani hii kamati kwanza iliyoundwa, wao wenyewe kwanza wachunguzwe ni wazima. Hii kamati iliyoundwa kuchunguza, nadhani na wao wanahitaji kuchunguzwa. Hatuwezi kuwa na watu tuliowaamini au tuliowapa madaraka kisha wakatuletea mchezo huu. Kama sio dhambi basi ningechana hapa hapa.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri hakutuletea ripoti kama tulivyomuagiza, kumbe muda wote ule ambao alikuwa akichelewa alikuwa anachakachua. Mhe. Spika, sisi ni wawakilishi, kweli hatuna elimu lakini tunajifunza. Sidhani kama wawakilishi hawa ni wapumbavu kiasi hicho. Tunawaongoza watu wakubwa sana, wana elimu kubwa, wana maarifa mengi na ndio sisi wanatuelekeza. Leo mwakilishi atoke hapa na ripoti hii akawaambie wananchi wake kuwa hii ndio ripoti ya serikali, ni aibu Mhe. Spika.

Mhe. Spika, katika sheria yenyewe ya fedha hapa Mhe. Waziri amezungumza, katika ukurasa wa 11. Mhe. Waziri amekiri kwamba sheria ya fedha ya mwaka 2005 imevunjwa. Lakini anasema kuwa kuanzia sasa Baraza wazingatie sheria hiyo, ni aibu na kama huu ndio utendaji wa serikali hii, *Wallahi* ni mtihani mkubwa, kwamba sheria inavunjwa lakini anaambiwa hapana, huko nyuma kote kuachie kuanzia leo uanze utaratibu.Kama haya ndiyo mafunzo ya China, basi tusiende tena. Sheria ikivunjwa kuna adhabu zake zimetiwa ndani ya sheria. Mhe. Waziri atuambie kuanzia leo hapa paachwe tuanze ukurasa mpya.

Mhe. Spika, mimi nawashauri wawakilishi wenzangu, kila anayekiri kwamba amechaguliwa na wanyonge kuja hapa, basi ripoti hii tuikatae katakata.Lakini anayesubiri uwaziri basi aunge mkono ripoti. Mimi sihitaji uwaziri, mimi fahari yangu ni kuwaona wanyonge wa nchi hii tunawalinda na kuwatetea. Anayesubiri uwaziri, mwengine aanguke apewe yeye na asubiri.

Mhe. Spika, kwa msingi huo naunga mkono iundwe kamati teule, ili serikali tuichunguze. Kwa hivyo, ripoti hii siiungi mkono na siikubali, ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi jioni hii ya leo, kuweza kuchangia ripoti hii iliyoletwa na Mhe. Waziri, iliyosheheni mambo chungu nzima.

Mhe. Spika, samahani sana sauti yangu leo kidogo imeliwa na hasa imeliwa kutokana na hii ripoti yenyewe ilivyonifanya nipate maradhi ya sauti yangu. Mhe. Spika, sijui sheria, lakini nitajaribu kufafanua sheria.Sisi hatukutaka hapa sera, tulichotaka ni maharibiko yaliyotendeka na mwenyewe kaonesha katika kifungu cha 8 kwenye ukurasa wa 11.

Mhe. Spika, siku moja nilisema hapa kuwa tutumieni kanuni ya ukurasa wa 88, kifungu cha 117, nilikisema hapa kwa vizuri tu. Leo ataona dhahiri Mhe Rais kama hatuna watendaji, tuseme ukweli. Siku zote mimi nasema, jamani tunamdanganya Mhe. Rais na hili nitalisema siku zote. Sasa kweli leo Mhe. Rais aangalie ripoti hii na aangalie ripoti ya madiwani ipi ya kweli. Madiwani hatukuwaambia sisi undeni tume, lakini waliona

kuwa hapana, kuna tatizo hebu tuundeni tume kwa nia nzuri tu, kwa sababu wana kanuni zao zinaelekeza jinsi gani ya utendaji wa kazi, lakini haufuatwi ndio wakaona waunde tume ili wafuatilie yale masuala yaliyokuwepo.

Mhe. Spika, Baraza lako linatiwa aibu sana. Mhe. Spika, mimi nina wasi wasi hii sio kweli, sio watendaji hasa, mimi nakataa kabisa wala siwatii makosani. Hii imefanywa vyengine. Ma-*professor* wale walioundwa kwenye hii tume ya serikali sio mchezo wamesoma, kwa kweli wametuletea ripoti hii na wameichakachua hali hii, mimi sikubaliani nalo, *never* sikubaliani nao Mhe. Spika. Sio kitu rahisi hawawezi kufanya utumbo huu hata siku moja. Lakini inawezekana ripoti hii baada ya kupeleka na kusema ukweli wale watu, ikafanyiwa kwa njia nyengine ndio tukaletewa hii leo. Jamani tunawatukanisha wenzetu tuliounda tume.

Mhe. Makamo wa Pili wa Rais nakuomba sana ulinde watu wako. Mhe. Spika, tuna ushahidi tosha na mikataba ambayo tukikuonesha hapa ya milioni 170 na mingineyo. Lakini Mhe. Spika, tunaonesha kwa nia nzuri tu, halafu itakuwaje ni sawa sawa na sisi tuko katika Baraza la Wawakilishi, iwe mfano katibu wetu hatuelewani naye si itakuwa ni vichekesho na wao madiwani wameona itakuwaje mkurugenzi wao wasisikilizane naye. Mhe. Spika, kamati teule iundwe, kwa mujibu wa kanuni zako mwenyewe Mhe. Spika. Sasa Mhe. Spika, wewe umesoma, hivyo sidhani kama utaikataa hii hata siku moja, lazima utatuunga mkono kamati teule iundwe Mhe. Spika, ripoti hatuikubali hii.

Mhe. Spika, wananchi wa Jimbo la Kitope hawakubali hata siku moja ukiwaambia suala kama hili, kwa sababu watu wamesoma siku hizi hawaikubali hata siku moja ripoti hii. Kwa hivyo, tunaikubali ripoti ya madiwani ndio sahihi. Tuwapongeze sana madiwani wamepata tabu sana. Walinyimwa ofisi, walinyimwa fedha na kila kitu. Lakini Mhe. Mkuu wa Mkoa akajitolea kifua mbele akatoa ofisi. Sio vibaya kumtaja na Mhe. Makamo wa Pili na yeye akatoa akasaidia ili mambo yaende vizuri. Leo inaletwa hapa ripoti haijulikani ina kichwa wala miguu. Mhe. Spika, tunasema Baraza lako tulilinde, *red carpet* yako ilindwe na tunasema iundwe kamati teule ili tuendelee na mchakato wetu. Mhe. Spika, mimi siungi mkono hata asilimia 2, ahsante sana Mhe. Spika. Nimemaliza heee!

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru sana Mhe. Spika, na mimi kupata nafasi hii. Awali ya yote niseme kwamba na mimi naungana na wenzangu kuikataa ripoti hii iliyoletwa na serikali.

Mhe. Spika, kama walivyoeleza wajumbe waliotangulia, kuwa msingi wa hoja hii ni hoja ambayo ilitokana na Wajumbe wa Baraza hili tukufu kutoridhishwa na uendeshwaji wa mambo katika Baraza hili, na hasa katika suala la upotevu wa fedha na ukiukwaji wa sheria na taratibu zote zinazohusu manunuzi katika Baraza hili.

Mhe. Spika, Baraza lilidai iundwe kamati teule kwenda kuchunguza uoza uliokuwepo Baraza la Manispaa, kama ilivyosemwa kuwa serikali ikaomba kwamba tusiunde kamati teule kwani yenyewe ilishaunda kamati na inapitia maeneo hayo hayo ambayo wawakilishi wanalalamikia, kwa hivyo ripoti ile ikikamilika italetwa katika Baraza. Sisi kwa nia safi kabisa tukaiamini serikali, lakini kinyume chake leo Mhe. Spika, tunaletewa hata sijui niziiteje zilizokuwemo ndani. Sina hata jina la kuziita nikaambiwa ninakiuka kanuni, lakini sijui kilicho humu ndani ni nini.

Mhe. Spika, ukiangalia Hansard ya toka Baraza la Wawakilishi la Mkutano wa Nane, tarehe 29 Juni, 2011 mwaka jana, wakati wa kujadili bajeti. Ukiangalia mjadala wa wawakilishi, ninayo hapa Mhe. Spika, lakini kwa kuokoa muda sitaki kuisoma. Lakini ukiangalia michango ya wawakilishi mbali mbali, takriban wote waliochangia walipochangia Wizara hii ya Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, basi waliligusa Baraza la Manispaa na wakataka hatua zichukuliwe. Lakini halikufanyika na tukaambiwa serikali inaunda kamati.

Leo Mhe. Spika, inatuletea mambo ya kiutawala, mambo ya kupendekeza taratibu za mageuzi katika serikali za mitaa. Haya siyo tuliyoyataka Mhe. Spika. Tunayataka, lakini sio katika muktadha wa hili, haya tuliyatolea maoni na tunaamini katika bajeti ikija basi wizara itakuja kutujibu kuhusu haya. Lakini haya siyo tuliyoyataka, tuliyoyataka sisi yalikuwa yanahusu ukiukwaji wa taratibu na matumizi mabaya ya fedha.

Mhe. Spika, ili kunusuru muda Mhe. Omar Ali Shehe, mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chake Chake, ameitaja hapa ripoti ya kamati ya kazi maalum iliyofanywa na Baraza la Manispaa. Inasikitisha Mhe. Spika, nimeipitia haraka ndio kwanza nimeiazima sasa hivi tu, nimeipitia haraka tu kwamba madiwani walikuwa na uwezo wa kufichua uchafu na uoza kiasi hichi uliokuwemo kwenye ripoti hii.Lakini haya yamefunikwa hayakuguswa kabisa katika ripoti hii. Sasa Mhe. Spika, tumeambiwa kuwa ripoti ilikuwa kubwa, kama ilikuwa na haya halafu hatukuletewa sisi, maana yake ni kulificha Baraza lako taarifa muhimu kabisa Mhe. Spika, ambayo ilitaka kuzifanyia uchunguzi yenyewe.

Mhe. Spika, Mhe. Omar Ali Shehe kanukuu katika majumuisho. Mimi naomba univumilie kidogo, nisome kurasa kama tatu tu kabla sijamaliza ripoti hii. Katika ukurasa wa 10 wa ripoti hii ya madiwani. Ripoti hii naisoma kama ilivyo Mhe. Spika, imeelekezwa kwa Mstahiki Meya, mbaye bahati nzuri tunaye juu pale katika ukumbi wako Mhe. Spika wa wageni wako. Ripoti inasema,

"Mstahiki Meya, uwezo wa Baraza la Manispaa kifedha unatokana na vyanzo vyake vya kukusanya mapato. Kamati imegundua vyanzo vilivyokuwepo hivi sasa vya mapato vya Baraza, havina usimamizi mzuri na wakitaalamu, na mtandao uliopo wa mapato ya Baraza haufanyi kazi kwa nidhamu na taratibu zinazokubalika katika kada ya fedha. Aidha, mtandao huo upo kienyeji sana.Moja katika mihimili mikuu ya taratibu za fedha katika kusimamia mapato na matumizi popote ni kuwepo kwa mkaguzi wa ndani, yaani *internal auditor*, Baraza halina Ofisa huyo kwa muda mrefu sasa.

Mstahiki Meya, chanzo kikubwa cha mapato ya Baraza la Manispaa ni masoko, leseni za biashara na *parking*, imebainika kwamba vyanzo vyote hivyo vinasimamiwa na watu wasio na ujuzi wowote wa shughuli za fedha na matokeo yake ni kuwa hakuna udhibiti unaokubalika katika mapato yanayokusanywa. Ushahidi wa hayo ni mkanganyiko wa taarifa zinazotolewa na watendaji wa sehemu hizo katika makusanyo ya mwezi kwani kila mtendaji alitoa takwimu zake. Imebainika hali ya usimamizi wa mapato inafanywa ibaki hivyo na kulindwa kwa nguvu zote, ili wahusika wa shughuli za fedha, wapate kuvuruga mapato ya Baraza kama wanavyoweza.Imebainika kuwa hakuna utaratibu maalum unaojulikana kwa kutumia vigezo au mazingatio ya uwezo wa utendaji kazi kwa watendaji wanaopangwa kukusanya mapato, hali ambayo inasababisha uvujaji mkubwa wa mapato.

Kamati imegundua kuwa hakuna mafunzo yanayotolewa kwa wakuu wa masoko kwa kazi waifanyayo, na ndio maana maofisa hao hufanya kazi kwa kubahatisha na kukubali kila watakaloshushiwa na bosi wao hata ikiwa ni kinyume cha maadili ya majukumu yao. Katika soko la Mwanakwerekwe, Mkuu wa Soko amechukua jukumu la kupandisha kodi kwa wafanyabiashara kutoka Shs. 500/- hadi Shs. 1,000/- bila hata ushauri ama ridhaa ya Baraza kama utaratibu wa kisheria ulivyo.

Kisheria kitendo ambacho kimewahi kutokea eneo hilo hilo na Baraza lilifanya maamuzi kwa njia ya kura katika kupandisha kodi kutoka Shs. 300/- hadi Shs. 500/- hapo awali. Aidha, kitendo cha uteuzi wa mtu mmoja kuwa ndio mkuu wa masoko mawili, soko la Saateni na Mwanakwerekwe, kamati haikuona kigezo kilichotumika".

Kuhusu kuchukuliwa mapato ya leseni. Naomba suala hili nilikwepe Mhe. Spika, na nimalizie hapo kwa kunukuu.

Katika ukurasa wa 12 "Mstahiki Meya, kamati inamwambia, imebainika kuwa Baraza halina utaratibu unaoeleweka wa kulipa watu wanaoingia na wasioingia nao mikataba, sambamba na matumizi makubwa yasiyozingatia bajeti, kama ambavyo ilivyo kisheria. Mfano ununuzi wa basi milioni 40, jenereta milioni 16 na malipo ya milioni 20 kwa ujenzi wa jengo liliomo katika ofisi za Baraza.

Vile vile Baraza halina utaratibu unaoeleweka wa manunuzi na mtu dhamana wa kufanya manunuzi hayo anayejulikana kwa jina la *Purchasing Officer*. Hivyo, hupelekea kuwepo kwa kinyang'anyiro cha kufanya manunuzi na hasa inapotokea manunuzi nje ya Zanzibar".

Mhe. Spika, kama nilivyosema nikiamua kulisoma hili basi nitachelewa mno, lakini nataka kusema kwamba ukiendelea hapo kuna majenzi mbali mbali na mikataba, ripoti hii inaonesha jinsi taratibu zilivyokiukwa na wakubwa. Inataja wazi wazi kwamba mkurugenzi na watendaji wake wawili au watatu aliowaweka karibu, ndio wanaosimamia mambo haya na wale wenye dhamana zao ambazo wametajwa kwa mujibu wa sheria za wafanyakazi wa Baraza, wote wamewekwa upande.

Mhe. Spika, ukiisoma ripoti hii kuanzia ukurasa wa 14 inazungumzia kwa urefu kabisa, kadhia ya soko la Saateni mpaka kwenye ukurasa wa 18, hapo inazungumzia soko la Darajani, ujenzi unaofanyika pale, jinsi watu walivyokiuka taratibu, fedha zinavyoliwa, watu walipopewa milango kinyume na taratibu. Ukurasa wa 20 unazungumzia soko la Mwanakwerekwe, ukurasa wa 22 unazungumzia ujenzi wa jengo ndani ya Ofisi ya Baraza, halafu ukurasa huo unazungumzia bustani ya Jamhuri, ukurasa wa 23 unazungumzia bustani ya Darajani Makontena na mengineyo.Lakini zaidi Mhe. Spika, inazungumzia kwa urefu sakata la mabango katika ukurasa wa 24 hadi ukurasa wa 30.

Mhe. Spika, suala hili la mabango ya matangazo ndio ambalo liliibuliwa mara ya kwanza humu ndani ya Baraza na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na akaonesha taratibu zilizokiukwa.

Mhe. Spika, ili kuepusha kuchukua muda, ili na wenzangu wapate nafasi ya kuchangia nimalizie kidogo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba ripoti hii tuikatae ila tuombe wajumbe wote tugaiwe ripoti hii ya Baraza la Madiwani.

Vile vile Mhe. Spika, naomba kwa hatua hii Baraza hili lipitishe azimio la kumtaka Rais amstaafishe kwa manufaa ya umma Mkurugenzi wa Manispaa kwa kushindwa kazi. Baadae mapendekezo haya ambayo yametolewa na Baraza la Madiwani ambalo lina mamlaka kisheria, yapate nguvu ya chombo hiki yasimamiwe na yatekelezwe na haya mengine yanayohusu jumla shughuli za utawala Mhe. Spika, yatakuja kutekelezwa na serikali kupitia katika utaratibu wa kawaida.Lakini kwa sasa yale ambayo yametajwa humu yafanyiwe kazi.

Mhe. Spika, nimalizie kusema ninaunga mkono hoja ya wenzangu kwamba kwa uoza uliokuwemo humu ndani ya ripoti ya Baraza la Madiwani, ni wazi kwamba kunahitajika hatua za haraka zichukuliwe ama tui-*adopt* ripoti hii au Baraza la Wawakilishi liunde kamati teule ikafanye uchunguzi wa kina zaidi katika hili au tuiagize PAC, lakini kusema kweli haya hayakubaliki.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, namalizia kusema tumuombe Mhe. Rais amstaafishe Mkurugenzi wa Baraza la Manispaa kwa manufaa ya umma, lakini vile vile Baraza liunde kamati teule kuchunguza haya kwa kina au tui-*adopt* ripoti hii na tuifanyie kazi ripoti hiyo, ahsante sana Mhe. Spika. *(Makofi).*

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii nichangie kidogo, maana naona mjadala huu wenzangu wameshauchangia sana na yale ambayo wameyatanguliza basi wamenifilisi mengi ambayo na mimi ningeweza kuyasema.

Kwa kweli Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha sana kabisa, kwa sababu hoja ambayo ilikuwepo katika kitabu hiki mimi sikuiona, ile ambayo tuliizungumzia. Sisi tulizungumzia kuhusu ubadhirifu wa fedha na mali za serikali pale, kuna ubadhirifu, kuna mikataba.Kitu kimoja Mhe.Spika, kinafungwa mkataba mara mbili, hiyo ndiyo ilikuwa hoja ya Mhe. Mshimba.

Sasa Mhe. Spika, unapotuletea hii sera, hii ni sera.Sera hii inahusu vipi Baraza la Manispaa litahuika na vipi litafanya kazi. Hiki ni kitu kizuri sana, hawa jamaa walioteuliwa ni watu wazuri sana, wameweza kufanya kazi moja nzuri sana ambayo wameagizwa. Mimi nawasifu sana hawa wajumbe wa kamati hii, ni wajumbe wazuri sana na ni waelewa kabisa katika mambo. Maana yake ukiangalia mchanganuo ambao wameuchanganua kwa kweli mimi nawapa hongera sana. Lakini hii ndio kazi ambayo wamepewa Mhe. Spika. Lakini hii sio kazi ambayo sisi tulitaka ifanywe. Sisi tulitaka uchunguzi wa fedha, ubadhirifu wa fedha, mali za serikali na mikataba, hiyo ndiyo ilikuwa hoja yetu kubwa. Lakini inaonekana Mhe. Waziri alipokwenda huko akabadilisha hoja yetu ile, akenda na hoja ya kwake, kwa hivyo hawa mimi siwatii lawamani wamefanya kazi moja nzuri sana wametoa maelezo vizuri sana, ukiangalia hii wakati wa bajeti akituletea kitu kama hichi tutafurahi kweli kweli maana tunaiona hasa kwamba Manispaa inabadilika, hapa picha ya jengo hili inapendeza kweli kweli ukiangali mimi nilichokiona ni jengo tu. Jengo zuri inaonekana limepigwa picha wakati ute wa sherehe za Mapinduzi kwa sababu limepigwa rangi hili safi kabisa.

Lakini humu ndani hamna kitu kwa hivyo Mhe. Spika, mimi naungana na wenzangu kwamba ripoti hii hamna kitu hatuwezi kuipokea tumuwachie Mhe. Waziri arudi nayo hii, naunga mkono hoja wenzangu waliotangulia kwamba tuchukue ripoti ile ya waheshimiwa madiwani ndio ripoti nzuri ambayo tunaweza kuifanyia kazi.

Lakini vile vile naunga mkono hoja ya Mhe. Omar Ali Shehe kwamba tuunde kamati teule kwa ajili ya kwenda kuchunguza ubadhirifu, mikataba hewa na mikataba mchanganyiko, nisichukuke muda mwingi sana maudhui yangu nafikiri itakuwa imeeleweka. Labda Mhe. Waziri anaweza kutwambia kwamba ripoti hii ni (a) labda iko na (b) inakuja, kama ni hivyo mimi ningeshauri tuisubiri hiyo (b) tuione nayo labda itakuwa na hayo maudhui tuliyoyakusudia, lakini hii hamna kitu.

Kwa hivyo mimi ripoti hii siikubali wala siiungi mkono Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono wenzangu waliotangulia lakini ripoti hii mimi ninaiwacha. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia machache kuhusiana na yaliyowasilishwa leo, maana atukisema ripoti tutakosea kwa hivyo bora tuite yaliyowasilishwa leo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nitoe historia fupi ya chanzo ya hicho kilichowasilishwa leo tulipokuwa katika kazi za kamati ya Mawasiliano na Ujenzi nikiwa mimi ni Makamo Mwenyekiti wa kamati hiyo, tuligundua tatizo la kiutendaji baina ya Shirika la Simu la Zantel wakitumia mawakala wao na Baraza hili la Manispaa kuhusiana na upachikaji wa mabango ya Zantel katika njia za Mji wa Zanzibar. Kwa sababu Zantel ni shirika ambalo serikali ina hisa ndani yake isiyopungua asilimia 21 sisi tukaona ni wajibu wetu kufuatilia maslahi ya serikali kwa sababu shirika lile Serikali ina hisa tuone ni kwa nini Manispaa wanakwamisha shughuli za upachikaji wa mabango ya Matangazo ya Zantel.

Mhe. Spika, mimi ndani ya droo yangu ninayo mikataba miwili iliyotiwa na mtu huyo huyo wa shirika la Zantel akatia tena mkataba kwa Shirika la simu la Tigo na waliotupa hatukwenda kufungua faili sisi, siku hiyo hiyo ya mkutano wetu wale wawakilishi waliokuja wa Manispaa walituletea mikataba hiyo. Sasa kwa bahati Mwenyekiti wangu akaja akawawasilisha katika michango yake wakati wa bajeti au wakati wa kamati.

Kwa hivyo chanzo kikubwa ni mikataba iliyokuwa inafungwa na Manispaa ya Zanzibar hilo la mwanzo Mhe. Spika, sasa baada ya kukataliwa kuundwa kwa kamati ya baraza tukapata faraja kwamba hawa madiwani wameona tatizo ndani ya hiamaya yao, kwa hivyo ikaundwa kamati na kamati ikatoa ripoti.

Mhe. Spika, sasa mimi leo nimeona kanuni imevunja kwa sababu asubuhi iliandikwa hapa alihudhurisha mezani hoja ya serikali juu ya ripoti ya Baraza la Manispaa ya Mji wa Zanzibar, sasa ulisema wewe katika ufafanuzi wako Mhe. Spika, kwamba zile hati zinazowasilishwa mezani zinatakiwa ziwepo, sasa kilicholetwa asubuhi sio ripoti ya Manispaa lakini ni hoja ya serikali, kwa hivyo ile ripoti ya Manispaa haikuletwa kabisa aliyoleta Mhe. Waziri ni hoja ya serikali sasa sisi hatukataka kupokea hoja ya serikali tumetaka kupokea hoja ya serikali juu ya ripoti ya Manispaa.

Kwa hivyo ilikuwa tuwe na mambo mawili kwanza tuwe nayo hiyo ripoti ya Manispaa kama walivyopata wenzangu huko, halafu serikali ndio itueleze kutokana na ripoti ile imeazimia kufanya jambo kadhaa au imeshatekeleza jambo kadhaa na kadha kama ambavyo imeonekana katika ripoti ya Spice Ilenders. Kabla haijatufika hatua zimeshachukuliwa, lakini Mhe. Waziri kachemsha leo akubali tu. *(Makofi)*

Sasa hii si hali nzuri ya kuendesha shughuli za kibaraza mimi naipongeza sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hali iliyokuwepo leo asubuhi hapo kama hatukuendelea kidemokrasi wale wasingerudi majumbani kwao leo, lakini waheshimiwa Mawaziri kama hawa ndio wanaovunja moyo watu *(Makofi)* Kwa sababu serikali inaendeleza demokrasi wao wanaitia kamba. Kwa hivyo ilikuwa aeleze wazi wazi mwenye kosa ajulikane na aliyekuwa hana kosa ajulikane, aliyekosa awekwe kando tuendelee mbele, lakini inawezekana ile aliyoikataa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais asubuhi ya leo Mhe. Waziri kaichukua yeye kafunika funika. *(Makofi)*

Hii ambayo ilikataliwa huku yeye kaona aa huku ilikokataliwa hakustahiki bora nipasiwe mie, kwa hivyo Mhe. Waziri ukweli kafunika funika mambo na mambo yote yako wazi sasa utayafunika vipi, hata ukijaribu kuyafunika yameshafunuliwa. Kwa hivyo baada ya maelezo haya Mhe. Spika, naomba niseme kwamba mimi kwa kadri ya uwezo Mwenyezi Mungu alionipa sikuona kama Mhe. Waziri katuletea ripoti iliyotakiwa kwa hivyo yale maelezo yaliyoelezwa yote namuomba ayabakishe mpaka siku ya bajeti aje ayatoe na hii ripoti hii naikataa, na haya mambo ambayo ya marekebisho siku ya bajeti aje atueleze kaweka marekebisho gani. Lakini ripoti yetu atuletee ile ile *original* halafu tuje tuijadili. Mhe. Spika, naomba nimalizie hapa ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, kwanza nichukue nafasi hii nikushukuru kwa kunipatina nafasi hii na mimi kuchangia, wala hata sijui nichangie nini, maana yake humu hamna cha kuchangia kwa kweli lazima tukubali, lakini niseme tu kwamba naionea huruma sana serikali ya awamu ya saba. *(Makofi)*

Mhe. Spika, dhamira ya wajumbe wako ambao wanachangia na wanaonekana kama wana chuki na mtu au wanajejea walahi sio dhamira hiyo, wajumbe wako ambao wanachangia katika shughuli mbali mbali za serikali wallahi wana nia nzuri sana za kuisaidia serikali hii ya awamu ya saba. Lakini niseme Mwenyezi Mungu amemuamrisha rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuteua viongozi mbali mbali katika awamu yake ya saba, ni Mwenyezi Mungu kamwambia mteue fulani na fulani na dhamira kubwa ya rais ni mategemeo makubwa sana katika viongozi wake ambao amewateua kwamba watamsaidia. Lakini nasikitika Mhe. Spika, na nasema wazi kabisa miongoni mwa baadhi yao hawamsaidii. *(Makofi)*

Mimi niseme hii niungane na wezangu kama wamesema sera au mambo ya kwenda kutumika yapelekwa ofisini kule ifanyiwe kazi, lakini kwa kweli dhamira na makusudi ya wajumbe wa baraza lako tukufu walipochangia suala la manispaa walichangia kwa moyo mkunjufu kabisa kuhakikisha kwamba Manispaa itafanya kazi zake kwa mujibu wa taratibu na sheria. Nimpongeze sana Mstahiki Meya wa Mji wa Zanzibar na chimbuko Mhe. Spika, mimi ni miongoni mwa kamati iliiyotembelea na nadhani aliposikia vita kuu katika afisi ya baraza la wawakilishi Mstahiki Meya akaunda kamati, kwa sababu yalimuelemea yeye mwenyewe.

Lakini leo Mhe. Spika, tukizungumzia ukweli wa hali halisi katika baraza la wawakilishi tunatafsirika vibaya, tunatafsirika labda hatuipendi serikali hii, labda tunamlenga mtu, labda tuna kitu. Mimi namshukuru Mwenyezi Mungu nimeshawahi kuwa Naibu Waziri, nikapata step by step mpaka nikawa Waziri , lakuni kama tunakwenda namna hii Mhe. Spika, naionea huruma awamu ya saba kwa baadhi sisemi wote, hebu tumsaidieni rais jamani tunakaa tunajadili mambo Mhe. Spika, kwenye baraza lako tukufu tukisha kujadili tukitoa maelekezo yanachukuliwa yanafinyangwa finyangwa yanatiwa kwenye meza *finish* au yamekwisha. *(Makofi)*

Tatizo sio wabunifu, tatizo sio watendaji ukamilifu, tatizo tunajitafutia mambo wenyewe kwa manufaa ya mtu binafsi naweza kusema hivyo, tulikuwa tunaingojea kwa hamu sana ripoti ya Manispaa na imezubaa zubaa tukasema labda tutaletewa kitu kizuri ambacho tutaridhika, matokeo yake tumeletewa sera na bango kitita . Maana yake picha hii sijui inamaanisha nini sijui nani aliyekuwa halijui jengo la Baraza la Manispaa.*(Makofi)*

Mhe. Spika, lakini mimi nasema hebu tuwa wakweli sisi sote humu ndani ni watu wazima tunalijua jema lipi na baya lipi, tunajua nini tunalifanya na tunajua nini namna ya kuisaida serikali hii ndio maana kukawa na Mawaziri, Manaibu Mawaziri, kuna na *back bencher* . kazi yetu sisi ni kuisimamia serikali na hatutokuwa tayari kwa sababu tumepewa dhima na wananchi katika nchi hii, sisi ndio wasemaji wa kuu wa wananchi katika nchi hiikuwatetea maslahi yao, kuwatetea kile ambacho tunahisi kwa mujibu wa taratibu na sheria ni haki yao. Naiomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tusaidie sasa hivi siasa tulicheza zamani, narudia kusema tena Mhe. Spika, siasa tumemaliza kilichobakia sasa ni kuijenga nchi hii kwa maslahi ya wenyewe wenye nchi wenyewe wako nje wanatusikiliza hao ndio wenye nchi Mhe. Spika, tujaribu kumsaidia rais na viongozi wake wawili, tusijaribu kuficha mambo ambayo yako hadharani haya. Kwani jamani tukisema hapa tumekosea kuna lipi jengine tunaficha donda ndugu jamani maradhi ya donga ndugu hayaponi, donda ndugu hata uchukue dawa gani haliponi hiyo ndio tabia yake, hata ukilitia moto ndio unalizidisha. *(Makofi)*

Kwa hivyo Mhe. Spika, mimi nimesema hatuna dhamira mbaya dhamira yetu ni nzuri sana, naomba sana kama walivyosema wenzangu tujaribu kuwa wakweli, waungwana nimpongeze tena Mstahiki Meya, lakini pia niwapongeze sana wenzetu madiwani na haya wameyafanya kwa kuona uchungu kwa mambo ambayo kuna watu wachache hivi wanataka utajiri wa haraka haraka, usile na kipofu mpaka akakukamata mikono. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nilisema nizungumze haya mimi kama kawaida yangu niungane na wenzangu yale yote kwamba hii ikawekwe Manispaa ifanyiwe kazi, ripoti hii ndio iwe ripoti kama ni kuundwa kamati teule iundwe naunga mkono na katika mmoja atakayekataa ni miye, kwa sababu nilichangia na miongoni niliyotoa uoza wa Manispaa mwengine ni mimi. Kwa hivyo sitokuwa kigeu geu nitakuwa mkweli kilicho na manufaa ya wananchi nitatetea kwa nguvu zangu zote, kilichokuwa hakina manufaa nitawapinga wale wenzangu ambao wanaambiwa wananiburura mimi sibururwi. Mimi hakuna mtu wa kuniburura Mhe. Spika, natumia demokrasi yangu na ninavyoona hivi ndivyo ambayo yataleta manufaa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba sana tumsaidie rais kwa umoja wetu tukijenga hoja ya kuleta faida kwa nchi basi tuwe pamoja, baada ya kusema hayo naungana na wenzangu katika yale mambo yote matatu na haya niliyoyazungumza mwenyewe, nikasema ni mmoja ambae suingi mkono na kama ni kamati teule ikiamulika iundwe ili twende sambamba kwa mujibu wa taratibu zetu na sisi ndio watunga sheria, sheria ichukue mkondo wake. Ahsante sana Mhe, Spika, *(Makofi)*

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema na uwezo nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii angalau na mimi kusema machache sana juu ya taarifa ya kamati ambayo sio tuliyohitaji sisi, kwa sababu sio tuliyoihitaji ndio iliyonifanya nisimame na mimi niseme.

Mhe. Spika, kwa namna tunavyokuamini na tuna kila sababu ya kukuamini na kukuheshimu lakini sio tu tunakuheshimu kwa sababu tuna kila sababu ya kufanya hivyo, pamoja na Makamo wa Pili wa Rais aliyemo humu ndani kwa shughuli za serikali.

Mhe. Spika, nadhani leo ni uthibitisho dhahiri kwamba tulichokidai siku ile wajumbe wa baraza lako hili tukufu kupata kamati teule ilikuwa ni haki yetu, ni haki yetu na haki ya Wazanzibari wa majimbo hamsini ya Zanzibar

yamo humu ndani. Mimi nataka niwaombe sana waheshimiwa wajumbe wenzangu haya yanayoendelea kufanywa haya na wenzetu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa upande ule pale simsikii vizuri mjumbe wangu.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Nasema yale yanayoendelea kufanywa na wenzetu na sisi tunaposimama hapa kuyakemea kwamba ni maovu na yanaharibu sana sifa ya serikali yetu inayoongozwa na rais wetu Mhe. Ali Moh'd Shein.

Mhe. Spika, nimesema sana na leo nitasema kwamba ni Mzanzibari wa mwanzo aliyebahatika kuiongoza serikali ya umoja wa kitaifa ni Dk. Ali Mohammed Shein kuna *challenge* nyingi ambazo dunia ilifikiria kwamba tungeshindwa kufikia hatua hii, mifano ipo mingi kwa wenzetu. Kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kwa nia safi ya Wazanzibari na nia safi aliyonayo Mhe. Rais tumepiga hatua ya kuigwa, tunawashangaza walimwengu mataifa makubwa yanajiuliza. Lakini kumbe tuna wachache wenzetu tunakwenda mbele wanatuvuta nyuma tena kwa makusudi, *(Makofi)*

Mhe. Rais analitambua Baraza hili na wajumbe wake na naamini anatuamini na wajumbe wote wanajua hivyo ushahidi upo, tukisema anasikia na anatusikiliza lakini kumbe kuna wenzetu wanatukebehi na kutubenza. Mhe. Spika, tutaendelea kulinda katiba tuliyokula kiapo na tutaendelea kuwalinda Wazanzibari na Watanzania kwa namna yoyote itakavyokuwa na wale watakaoamua kufanya vyenginevyo hatukubali kutoa nafasi, kama wameamua mapambano na waamue na ishara zipo kwamba wameamua mapambano kwa nini hatuelewani tukakubaliana.

Mhe. Spika, tulichodai Baraza la Manispaa Zanzibar kuna uwoza, sisi tunalipwa hapa kufanya kazi ya wananchi fedha ile ni ya umma, tunakwenda mimi nimo kwenye kamati zako mbali mbali za kudumu na wenzangu. Tumekwenda kule ndio tunayakuta hayo. Tunaposema uwoza sio ule wa mapapai na ndizi zinazoharibika sokoni, hapana.

Mhe. Spika, kuna uwoza unaofanywa na watendaji wizi kuna wizi kule. Kuna vitabu vya risiti kila mtu chake. Tutasema, kuna watu wamewekwa kukusanya mapato ya Baraza, watu hawana uwezo huo lakini wanaishi kwa maslahi ya watu na mengi mengine yanayofanana na hayo ndio tukasema ni uwoza kwa serikali kama hii ya Mapinduzi. Ule ni uwoza uundiwe kamati teule yakachunguzwe yajulikane, tusawazishe twende mbele na tusirudi nyuma. Hichi ndicho tunachokidai. Taarifa hii ya Dokta wangu hii wenzangu wameshasema itatufaa kwenye bajeti sio leo.

Mhe. Spika, nilitarajia swahiba wangu, ndugu yangu, mwenzangu wa tangu, Dokta Mwinyi haya mambo yatamchafua. Yeye ni Dokta inamtambua dunia kule anakuja kutosome hii, hii kweli inatoka serikalini, huu ni mtihani waheshimiwa.

Mhe. Spika, hapa juu hii Kamati kuna Dokta mwengine ndiye aliyeiongoza kua Mwenyekiti, ukija ukitizama maudhui ni utumbo mtupu humu. Tunasema kulia, mwenzetu anatwambia kushoto, maana yake nini? Hivi wajumbe wote hawa hawajui kulia ni wapi. Sasa tukijiuliza maswali haya tutafika kugumu sana lakini tunachosema kwa ufupi sana Mhe. Spika, nadhani leo huna sababu ya kutuomba tena.

Mzee wetu Makamo wa Pili alilitia kifua tukaheshimu sana alikua hajayajua na leo keshajua yaliyokuwepo serikalini kwake. Tegemeo letu leo mtatupa nafasi yetu na sisi. Kamati teule ya Baraza lako tukufu wananchi wasikie leo utaje na wao wabaki na imani ya Baraza na Serikali yao, inayoongozwa na Dokta Shein.
Mhe. Spika, zile kura za Wazanzibari sio mchezo hazijapatikana hapo mahali. Hii serikali watu wana imani nayo kubwa. Tusikubali kutoa nafasi wenzetu kutuvuruga kiasi hichi, hata kidogo.

Mhe. Spika, yote tunayoyadai yakachunguzwe. Mhe. Waziri, Serikali kwa ujumla ikajipiga kifua, wameyatupa kule baidi, wanakuja na yao kutupa namna gani Baraza litakwenda, sera zipangweje. Haijapangwa sera mpaka leo, hiyo ni juu yao wenyewe sisi hatujadai sera. Sisi tumedai tunachokidai na ndicho tunachokitaka na kama hawajaweza kukileta tunaomba sana tukubalieni Mhe. Spika, na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais, ndiye yumo humu ndani ndiye aliyesema tukubali nasi tukakubali.

Mhe. Spika, bila ya kupoteza muda maudhui yetu umeyaelewa, tunakuomba sana kwa jinsi tulivyo na wananchi wanavyofuatilia Baraza lako hili hakuna sababu tena ya kulitia madoa. Hebu toa nafasi, hii ni haki yetu na kwa kukukumbusha Dokta wangu nakuomba kwa ruhusa yako ninukuu kidogo usia wa pili wa Katiba ya Zanzibar,

Kifungu cha 9 (1) “Zanzibar itakua ni nchi ya kidemokrasia na haki za kijamii”
Kifungu cha 9(2) Kwa hiyo hapa inaeleza rasmi kwamba:

(a) Mamlaka ya uendeshaji nchi ni ya wananchi wenyewe ambapo nguvu na uwezo wote wa Serikali. Hiyo serikali nguvu zake zote hufuatana na katiba hii utatoka kwa wananchi wenyewe”

Wenye mamlaka na madaraka ni sisi kwa niaba ya wananchi na si serikali, serikali kusimama ikasema tukaridhia ni ridhaa yetu. Leo tunataka nafasi yetu. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo machache sana nakuomba wajumbe wako leu utukubalie kamati teule tunaihitaji kwa kweli kufanya kazi ya wananchi waliotutuma. Nakushukuru sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru kunipa nafasi hii nikazungumza kwa muda mchache sana katika historia tokea niingie katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, mimi kwanza nasikitika sana kua rafiki yangu, swahibu wangu, waziri wangu nikiwa mimi ndiye mwenyekiti wa Kamati ya kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa kitaifa ambaye Mhe. Waziri anatakiwa awe mimi ndiye swahibu wangu mkubwa.

Mhe. Spika, nasikitika sana kwamba ripoti hii angalau basi angelinichungulisha nikaiona, Mheshimiwa kauli za wajumbe zisingekua kama hivi unavyozisikia. Najua ripoti imekuja kama hoja ya serikali kama Kamati hatukupata nafasi ya kuweza kuipitia na kutoa maoni. Nakuthibitishia Mhe. Spika, ripoti hii laiti kama ingelikuja kwenye Kamati ripoti hii tungelimwambia Mhe. Waziri asubiri katika kitabu chake cha bajeti aje atueleze.

Mhe. Spika, wenzangu wamezungumza mengi lakini mimi nataka nizungumze kwamba wenzetu waliokuwepo mstari wa mbele tuisaidie sana serikali. Mheshimiwa kwa utaratibu huu bado hatujadhamiria kuisaidia serikali. Wananchi wetu wanajiuliza kuna nini Barazani mbona kila siku hoja za serikali zinapokwenda zinakua ngumu kupita. Tatizo linajitokeza hapa tunapojadili Miswada yetu hapa au hoja zetu mbali mbali wenzetu wakishakuondoka hawarudi kwenye hansard wakaangalia nini tulichokizungumza.

Mhe. Spika, sisi kazi yetu kuisimamia serikali kama Katiba ya Zanzibar inavyoeleza kifungu cha 5. Masuala ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Waziri hajaleta jawabu yake. Na mimi naomba sana Mhe. Spika, ripoti hizi tulizogaiwa kwa ridhaa yako uturuhusu tuzikusanye tuzilete ofisini kwako uzihifadhi usubiri ripoti tutakayokuletea sisi baada ya kuunda hicho chombo ambacho wajumbe wanachokihitaji.

Mhe. Spika, serikali kuchunguzwa wala sio aibu ndio utaratibu wa mabunge yote duniani, pengine tunachokisema sisi ni dhana tutakapokwenda Mhe. Spika, tutathibitisha yale yaliyokua yanazungumzwa. Lakini ukenda katika Hansard humu hupati hata moja tuliyoyadai sisi. Mheshimiwa mimi naomba sana wala tusiwalaumu hawa walioandika hii ripoti. Hii ripoti ya maboresho ya Baraza la Manispaa kwa hivyo hii itatusaidia sana. Mimi ni mwenyekiti wa Kamati nimejaribu kuangalia nikaona kama hii tutaifata basi mambo yatakuja kua mazuri sana. Lakini kama ingekua kuna wale rafiki zangu wale wamakonde wenzangu ningeliwaambia “nilikua chipo”

Mhe. Spika, nataka niseme kwamba Mhe. Waziri kama nilivyosema mimi swahibu wangu na kama alivyotuomba swahibu wangu zaidi Mhe. Makamo wa Pili wa Rais (Balozi Seif Iddi) kwamba tuiwachie serikali. Serikali tumeiwachia na mara nyingi rafiki yangu, swahibuu wangu Mhe. Waziri Dokta Mwinyi Haji Makame anasema tuaminini, Waheshimiwa tuaminini. Sasa Mheshimiwa tunakuamini sana na hii ripoti kama tulivyosema sio zitupwe, tusikusanye, serikali tunaiamini kwamba Baraza la Manispaa kwa ripoti hii itakuja kwenda vizuri huko mbele.

Baada ya hayo machache na mimi nataka niseme kwamba Mhe. Waziri inaonesha ripoti labda zilikua mbili. Aliyokusudia kuileta ilikua siyo, sasa aturuhusu tulete kile kitu ambacho Mhe. Spika, serikali itaridhika kwa kuisaidia serikali. Baada ya hayo machache Mhe. Spika, nakushukuru sana naomba ripoti tuzikushanye. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni kwa kuendelea na mchango wa shughuli hii bado tunao wachangiaji wawili watatu tutawasikiliza kesho baada ya kipindi cha Maswali penye majaalia. Ripoti hizi wacha tubaki nazo kama kumbukumbu tusizikusanye. Nafikiri itakua haitudhuru kubakia nazo, kwa hivyo angalau tubaki nazo kama kumbukumbu ili tuendelee mjadala tuone tunafika wapi hiyo kesho.

Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe sasa naakhirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 12/4/2012, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:38 usiku Baraza liliakhirishwa
hadi saa 3:00 asubuhi tarehe 12/04/2012)